

JE! MAISHA YAKO

YANAISTAHILI INJILI?

 Na tuendeleo kusimama kidogo, wakati tukiinamisha vichwa vyetu sasa na kumwelekea Bwana. Kama kuna haja zozote za kujulikana kwa Mungu, naomba sasa hivi tu umwinulie mkono wako, namna *hiyo*, na ushikilie moyoni mwako kile unachotaka.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya siku nyingine. Na sasa imeanza kujitokeza; itakuwa ni historia. Ibada za asubuhi ya leo zimepita tayari. Maneno ambayo yamesemwa yako hewani, kwenye kanda, na itatubidi kukutana nayo siku moja. Itabidi yawe ni ya kweli ama ni ya uongo. Na sisi—sisi tunaamini ya kwamba ni ya kweli, kwa sababu kwamba ni Neno Lako.

³ Sasa, tunaomba ya kwamba Wewe utatujalia, usiku wa leo, haja tunazomba. Mikono yetu, tunaiinua, tukiomba haja. Wewe ulijua yale tuliyohitaji, na yale tunayoomba. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba utatujibu, Bwana, na kutupa shauku ya moyo wetu, hiyo ni kusema, kama tunaweza kuzitumia kukuhashimu. Tujalie, Bwana.

⁴ Yaponye magonjwa yaliyo miongoni mwetu. Ondoa dhambi yote na kutokuamini. Tupe ninii Yako . . . sehemu ya baraka Zako tena, usiku wa leo, Bwana, tunapotafakari juu ya Neno, na wakati tunaishi. Tumekusanyika pamoja, Baba, si kwa kusudi lingine ila kujaribu kujifunza jinsi ya kuishi vizuri zaidi, na kuishi karibu zaidi na Wewe. Kwa maana tunaona ile siku ikikaribia, nasi hatuna budi kukusanyika pamoja mara kwa mara, na kupata maagizo kutoka Kwako. Lijalie, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

Asanteni. Mwaweza kuketi.

⁵ Ninajua kuna joto sana, na mahali hapa pamejaa sana jinsi hii. Na kwa hiyo tunasikitika hatuna ninii . . . viyoyozi vyovyote. Na mimi . . . Labda hiyo itakuwa ni . . . Kuna mambo mawili ninayotaka kulifanyia kanisa, mara ninapoweza kurudi jinsi ninavyotaka kurudi, kama nikirudi kwenye mikutano vizuri. Ninataka pi—piano, ambapo limekaa *hivi*, namna kwamba mpiga piano atakuwa ameliangalia kusanyiko. Ninataka kinanda upande *huu*; na kiyoyozi. Ndipo ninaona kwa jinsi hiyo itakuwa ni sawa. Na kwa hiyo tunaninii . . . Tutamtumaini Bwana, na tunajua ya kwamba Yeye atatujalia.

⁶ Ninaamini, wao waliniambia, Ndugu Hickerson ndiyo kwanza atoe *hili* kutoka kwenye gazeti. Aliliweka kwenye

dawati langu huko nyuma. Hilo ni lile kundi la Malaika lililo kwenye gazeti ambalo lilinenwa habari zake. Mnaona umbo la piramidi? Mwangalieni Huyu aliye upande *huu*, ubawa uliochongoka, akija na kifua Chake kilichotokeza namna hiyo, kwenye upande wa mkono wangu wa kulia. Kama nilivyosema kutoka kwenye mimbara hii, miezi na miezi na miezi iliyopita, unaona, Hilo hapo. Nalo gaze-la *Look* . . . Ama, gazeti la *Life* lina Hilo, toleo la—la Mei, Mei 17, ninaamini ndilo. Hiyo ni kweli? Mei 17, toleo. Bibi Wood alikuwa akiniambia leo ya kwamba wengi walimpigia simu na kumuuliza. Hilo liko kwenye toleo la Mei, Mei 17.

⁷ Ni wingu la siri. Wingu hilo liko maili ishirini na sita kwenda juu na maili thelathini mlalo. Na hilo ndilo tulilokuwa tukizungumza juu yake hapa. Hapo ndipo Malaika wa Bwana aliposhuka na kupatikisa mahali hapo. Na ninii yote . . . Iitoa sauti kubwa zaidi . . .

⁸ Ninajua kuna mtu mmoja, kama . . . Nafikiri, Ndugu Sothmann, nilimwona muda mfupi uliopita, mahali fulani. Yeye yupo hapa. Alikuwa amesimama . . . Naam. Papa *hapa* nyuma. Alikuwa amesimama hapo karibu wakati hilo lilipotukia. Nadhani sikuwa mbali sana naye. Ndiyo kwanza nimwone, nikajaribu kumwashiria. Ila tu, nilikuwa na darubini yake. Ambapo, wale—wale wanyama, mahali tulipokuwa tukiwindia, palikuwa . . . Hawakuwa kwenye kilima hiki. Sasa wao walipanda kwenye kilima hicho kingine. Niliwaona, siku iliyotangulia, na nikawaambia mahali pa kwenda. Mimi nikaenda *huku*, ambako, kama wakija huku, ningepiga tu risasi hewani na kuwafukuza warudi upande waliko, kusudi waweze kuwapata wa—wa—wanyama wao. Kwa hiyo, ilikuwa ni nguruwe mwitu.

⁹ Na kwa hiyo nikaenda huku, upande huu, nao hawakuwako. Hawakuwako upande wowote. Nikamwona Ndugu Fred akitoka, nao hawakuwako. Akarudi, na Ndugu Norman akapanda kile kilima. Na nikageuka, nikashuka kwenye genge dogo na nikapanda, peke yangu tu, yapata maili moja na nusu kupitia kwenye nchi ya mawemawe sana. Na nilikuwa nimeketi chini na nilikuwa tu nikiangalia pande zote. Kulikuwa kunapambazuka.

Nami nilikuwa nikitoa hizo, tunazojiita kule, vichwa-mbuzi. Ni kitu kama mbegu zenye miiba. Nikizitoa kwenye mguu wa suruali yangu, za aina ile ile hasa nilizojiona nikizitoa nilipokuwa hapa nikiwaambia kuhusu lile ono, karibu, miezi sita, kabla halijatukia. Nikasema, “Hilo ni la ajabu. Angalia jinsi nilivyo kaskazini mwa Tucson kikamilifu, kitu kama kaskazini-mashariki. Inafanya . . .

“Tucson,” kumbukeni, nilisema, “kidogo kusini-magharibi.”

Ndipo nikasema, “Hilo ni la ajabu.” Nilikuwa nikiangalia mbegu hizo zenye miiba, namna *hii*, nikizitoa kwenye ninii yangu. . . nyingi za hizo, kutoka kwenye miguu ya suruali yangu. Kama hujapata kuwa kule, hiyo ni nchi ya jangwa. Si kama hii, hata kidogo. Ni angavu mara ishirini zaidi; wala hakuna miti na kadhalika kama ilivyo hapa. Ni mipungate tu na mchanga.

¹⁰ Kwa hiyo ni—nilikuwa tu nikiziangalia, namna hiyo. Niliyainua tu macho yangu juu. Na kama, ningesema, nusu maili kutoka kwangu, nikaona kichwa kizima cha . . . kundi zima la nguruwe mwitu, limekaa, likitokea pale mwishoni, mahali walipokuwa wakila majani filarii. Na nikawazia, “Sasa, laiti ningeweza kuwaelezea Ndugu Fred na Ndugu Norman pale, pale ndipo mahali penyewe hasa.”

¹¹ Na jioni iliyotangulia, Roho Mtakatifu alikuwa akitenda kazi sana kambini, hata alikuwa akiniambia mambo yaliyokuwa yametukia na yaliyokuwa yakitukia. Ilinibidi kuamka na kuondoka kambini mwangu.

Halafu basi, kesho yake asubuhi, nilikuwa nimepanda kwenda kule juu. Na nikaanza. . . Nikasema, “Sasa, kama ninaweza kufika kwa Ndugu Fred, nitampata nyuma ya mlima huu,” ambao ni kama ma—maili moja kwenda *hivi*. Ilinibidi kwenda kama—kama maili moja upande *huu*. Ilinibidi kwenda kama—kama maili mbili, ama zaidi, nimchukue, labda tatu. Nirudi *hivi*, nishuke nipitie mahali tunapoita mgongo wa nguruwe, nipande hivi, juu ya milima hii ya magengemagenge, yaliyochongoka, kisha nishuke mbio *hivi*, nikate na kuja huku, kisha nishuke kwenda upande *huu* na kumchukua. Ndipo itambidi kushuka moja kwa moja mpaka chini ya kilima hicho, kumchukua Ndugu Norman, ambazo zingekuwa labda ni maili nne ama tano, kisha warudi. Na nilikuwa nikitaka kuweka ki—kipande cha Klineksi ambacho nilikuwa niende kukitundika kwenye kipande cha—cha mpungate pale, nipate kujielekezea kwamba ningetokea kwenye kigongo kipi nitakaporudi.

¹² Nami nikatoka tu juu ya kigongo kidogo ambapo kuna miamba mingi iliyochongoka, na kuna m—mburuzo wa paa unaoshuka upande mwingine, karibu, loo, yadi arobaini, hamsini chini ya mtelemko wa jabali. Ilikuwa ni kama, loo, kulikuwa kumekwisha kupambazuka, ningesema saa mbili, ama tatu. Ungewazia kitu kama hicho, Ndugu Fred, labda saa tatu, kitu kama hicho? Nikakimbia upande *huu*, upesi, hao nguruwe mwitu wasije wakaniona. Wao ni nguruwe dume wa mwitu, mwajua, nao ni waoga sana.

¹³ Kwa hiyo ni—nikapanda kilima *hivi*, na kukata, nikaanza, nikapanda mbio kilimani. Na nikakimbia tu, kwenye ninii, tunachoita, mwendo shoti wa mbwa. Na kwa ghafla, nchi nzima ikalipuka. Kamwe sijapata kusikia mlipuko wenye kutisha jinsi hiyo! Ulitikisa tu, na miamba ikafingirika. Nami nikajisikia

kana kwamba hapana budi ni—nilikuwa nimeruka futi tano kutoka ardhini, ilivyoonekana. I—ilinitisha. Nikawazia, “Loo, jamani!” Nilifikiri nilikuwa nimepigwa risasi. Ya kwamba mtu fulani. . . Nilikuwa nimevaa kofia nyeusi. Nilifikiri pengine walidhani ilikuwa ni nguruwe mwitu akipanda mbio mlimani, mtu fulani alikuwa amenipiga risasi. Iitoa sauti kubwa sana, moja kwa moja juu yangu, namna hiyo. Halafu, mara, Kitu Fulani kikasema, “Angalia juu.” Ilikuwa ndiyo hiyo. Ndipo Yeye akaniambia, “Ni kule kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba. Rudi nyumbani.” Kwa hiyo, mimi huyu hapa ninakuja.

¹⁴ Nikakutana na Ndugu Fred na Ndugu Norman, kama saa moja baadaye, wakati nilipowapata. Walikuwa wameshikwa na kiwewe na wakinena habari zake. Ilikuwa ndiyo hiyo. Nayo sayansi inasema ya kwamba haiwezekani kwa—kwa namna yoyote ya—ya umande ama chochote kupanda juu hivyo, ukungu, mvuke. Unaona? Utaenda tu ninii. . . Nisingejua. Mimi—Mimi. . .

¹⁵ Sisi, tunapoenda katika nchi za ng’ambo, tunasafiri futi elfu tisa. Hiyo ni juu ya tufani. Hiyo ni karibu maili nne. Na tuseme, hebu tuseme, labda ni maili kumi na tano ambapo huwezi kupata tena ukungu. Lakini hizi ni maili ishirini na sita, nalo lilining’inia kule siku nzima. Mnaona? Hawajui ni kitu gani. Lakini, Bwana ashukuriwe, sisi tunajua.

Asante, Ndugu Hickerson. Nitaliweka kwenye dawati langu kule ndani. Na tutakapokiandika kile kitabu, mbona, basi tunaweza kuichukua.

¹⁶ Nina muhtasari mdogo hapa niliopewa. Ninaamini kumekuwako na ongezeko katika hesabu yetu tangu nilipokuwa hapa mara ya mwisho. Ninafikiri jina lake ni—ni. . . angalau, jina la baba yake, David West. Nao wana jamaa mdogo hapa ambaye wanataka kumweka wakfu kwa Bwana. Je! hiyo ni kweli? Ilikuwa ni usiku wa leo, ama ilikuwa ni Jumatano usiku? Sijui. Haina budi. . . Usiku wa leo? Hilo ni sawa. Vema, vipi kuhusu. . . Wewe ni David, sivyo? Hivyo ndivyo nilivyowazia unaitwa. Vema. Vipi kuhusu kumleta jamaa huyu mdogo huku?

Kama dada yetu atakuja hapa kwenye piano hili, na atupe wimbo wa *Waleteni*. Mchungaji, akipenda, aje hapa, na tutamweka mvulana huyu mdogo wakfu kwa Bwana. Sasa, sisi hujaribu kuliweka Kimaandiko.

¹⁷ Huyu ni mjukuu wako, Ndugu West. Halionekani linawezekana; sivyo? Dada West, unaonaje juu ya jambo hilo? Hivi haininii. . . Mnajua ninavyowazia, hata hivyo? Mwajua, mimi ni babu, pia.

Inanikumbusha juu ya Ndugu Demas Shakarian. Alikuwa amesimama mbele ya umati mkubwa wa watu. Yeye huchanganyikiwa na kila kitu kama mimi, mwajua. Alikuwa amesimama pale. Akasema, “Mwajua,” kasema,

“Ni—nilimwambia Rose, nilijisikia,” huyo ni mkewe, kasema, “nilijihisi kuwa mzee zaidi kwa kuwa nilikuwa nyanya.” Akasema, “La. Ninamaanisha ba- . . .” Mwajua, mimi. . .

¹⁸ Huko peke yako, Ndugu West. Kuna wengi sana wa hao humu ndani. Na ni sawa. Nafikiri tunaweza kweli kuwafurahia wajukuu wetu. Hili halininii. . . Natumaini hili halisikiki ni baya. Lakini tunaweza kuwa na wakati zaidi nao, ninaamini, kuliko tulivyokuwa pamoja na watoto we—wetu. Nilimuuliza mke wangu hilo, hivi majuzi. Kasema, “Hakika. Unawapenda kwa kitambo kidogo, unawarudisha kwa mama yao, na kuendelea.”

¹⁹ Vema, nina mjukuu mdogo kule nyuma. Yeye alisema, “Papa, hubiri. Papa, hubiri.” Nao wakachukua matoleo Jumapili iliyopita usiku, na wakayaweka mezani. Wakamleta ndani, huko nyuma, na—na akanisikia kupitia maikrofoni. Akasema, “Papa, hubiri. Papa, hubiri.”

Na Billy akasema, “Naam, huko *juu*.”

Akasema, “La.” Na sadaka ikatapakaa kote sakafuni. A—alitaka kuja huku, unajua. Na daima ananipigia makelele, unajua, akiniona kwenye mkutano wowote. Anapiga makelele, “Papa, hubiri.” Akapiga makelele kwa sauti kubwa sana. Kwa hiyo ninajua wao ni wazuri sana.

Aisee, sijui kama ningeweza kuazima baadhi ya hizo nywele? Hazihitaji sasa hivi. Ninazihitaji. Jina lake ni nani? [Dada West anasema, “David Jonathan.”—Mh.] David Jonathan. Hilo si ni jina zuri? Vema, ninatumaini maisha yake yatafanana na ya yule aliyepewa jina lake. Daudi, yule mfalme, Daudi; ambaye, Kristo ataketi kwenye kiti chake cha enzi; na pia Yonathani, rafiki mpendwa. Na—nawaambia, wao ni jamaa wadogo wa kupendeza. Tunawathamini, sana. Mimi. . . Yeye anaamka. Naye anaweza—anaweza kusema kwa sauti kuu “amina” vizuri tu kama hao wengine, unajua, kwa hiyo hatutaliacha litusumbue. Tunamweka wakfu kwa Bwana.

Ninafikiri ni vizuri sana, kuwa na bwana na bibi wenye umri mdogo, ambao Mungu ameweka katika ulinzi wao jamaa mdogo kama huyu, na wanakuja kumtoa kwa Bwana. Na unapofanya hivyo, inaonyesha ya kwamba wewe si ninii. . . ya kwamba unamrudishia Mungu kile Mungu alichokupa. Mungu ambariki.

Sasa, ukitaka kumshika, ninaamini labda mama kidogo angeweza kumshika vizuri zaidi kuliko ningalimshika. Na vipi kuhusu sisi kumwekea mikono tu? Unaona ni afadhali ufanye hivyo? Maana, ninahofu nitamwangusha ama, sio kumwangusha, kumvunja ama kitu kama hicho, mwajua. Nami daima ninahofu kuwavunja, mwajua. Yangu—yangu. . .

Meda alisema, huko nyuma. . . Ninafikiri hii ni kazi moja jukwaani ambayo kwa namna fulani ananionea wivu, mwajua. Yeye anapenda kuwashika nanii. . .

Vema, angalia hapa, yeye ataniangalia. Ni jamaa mzuri. Naam, bwana. Labda ningeweza kumshika. Sijui. Loo, dada, usininii. . . Natumaini hataanguka. Hapa, si hilo ni zuri? Hilo ni zuri? U hali gani? Vema, sasa, mpenzi.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

Bwana Yesu, miaka mingi iliyopita, wakati Ukristo ulipozaliwa katika umbo la Mtu aliyemitwa Kristo, Masihi aliyetiwa mafuta, Jina Lake lilikuwa ni Yesu. Watu walimletea watoto wao wachanga, ili apate kuwawekea mikono na kuwabariki. Na Yeye akasema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie, kwa kuwa walio kama hao Ufalme wa Mbinguni ni wao." Maskini mume huyu na mke, babu zao na hao wengine wamekuwa ni wafuasi wa kweli wa Neno.

Bwana Yesu, ninaleta, na kumkabidhi Kwako, usiku wa leo, mimi pamoja na mchungaji, mtoto huyu wa kupendeza David Jonathan West. Ninamtoa Kwako, kutoka kwa mama na baba. Ninamtoa Kwako, Bwana, kwa afya, nguvu, maisha marefu ya huduma, kumwadhimisha Mwenyezi Mungu, ambaye alimleta humu ulimwenguni. Jalia baraka za Mungu zikae juu yake. Jalia Roho Mtakatifu akae juu ya mtoto huyu. Kama kuna kesho, jalia aiendeleze Injili ambayo wazazi wake na babu zake wanaithamini sana leo. Lijalie, Bwana. Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninakupa mtoto huyu, katika kuwekwa wakfu kwa maisha yake. Amina.

Ninaamini wanataka kupiga picha ya maskini jamaa huyu mdogo. [Kamera inaalika—Mh.] Niliruka, pia.

Mungu akubariki, dada. Na ujaliwe daima kumpenda na kumthamini Bwana Yesu, na jamaa huyu mdogo alelewe katika maonyo ya Mungu, na mwe na mvulana mdogo mzuri sana. Nina hakika. Mungu awe pamoja nanyi.

Ninaamini alianguka maskini kitulizi chake? Walikipata? Loo, jamani!

Sasa hebu na tuimbe huo wimbo mfupi, *Waleteni*. Kila mtu pamoja sasa, kwa ajili ya mvulana huyu mdogo. Vema, dada.

Waleteni, waleteni,

Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

²⁰ Sijui mikono mizuri zaidi ya kuwawekea. Nanyi je? Mikono ya Bwana Yesu!

²¹ Sasa, ninajua kuna joto huko nje. Ninataka kumwambia bawabu, ndugu yangu, Doc, ama mwingine, hao wanaoishughulikia. Baadhi ya akina dada wanaharibu sketi zao kwa—kwa grisi iliyo kwenye kiti. Ni wangapi wamepakwa hiyo? Ninajua, kuna mke wangu, binti zangu wawili, mtoto Betty Collins, Bibi Beeler, baadhi yao. Ni kitu fulani, grisi iliyo pale. Naomba uiangalie, Doc, uwezapo. Ni, ninaamini, ni mahali waliponinii. . . Ni grisi ama rangi, ama kitu fulani, papo hapo

mahali wanapofanyia kazi huku na huku, viti. Na ati hamna? [Ndugu Edgar “Doc” Branham anasema, “Hamna grisi juu ya hivyo, ya kutolewa.”—Mh.] Vema, si—sijui ni kitu gani, basi. Kitu fulani nilichoninii tu. . . Niliambiwa jambo hilo, nami nikasema nitalifikisha kwa—kwa Doc. Vema.

Sasa, mkutano wa maombi wa Jumatano usiku. Kuna mwingine? Mmeutangaza? Mmeleta matangazo yenu, Ndugu Neville? Matangazo yote yameletwa.

²² Sasa, Bwana akipenda, Jumapili ijayo asubuhi, ninataka kuzungumza juu ya somo la kukishtaki kizazi hiki kwa kumsulibisha Kristo. Mnasema, “Kizazi hiki kisingeweza kufanya hivyo.” Tutaona kama walifanya hivyo, ama hawakufanya, kulingana na Neno. Sasa, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda. Kama, sasa, kama—kama—kama jambo fulani likitukia. . .

²³ Ninapaswa kuwa huko Houston juma hili, pia, katika mkutano, ambao utanichukua hadi Jumapili, kwa hiyo sijui kama nitaweza ama sitaweza. Lakini tuna Jumapili zingine zaidi za kufanya shughuli zingine, kabla ya hapo, hata hivyo. Baadaye tutaenda Chicago kwa ajili ya mkutano, ama mkutano huko Chicago, juma la mwisho katika mwezi huu. Na halafu inanibidi kuirudisha familia Arizona, kwa—kwa kuwa likizo yao imekwisha na watoto hawana budi kurudi shuleni.

²⁴ Sasa, ni wangapi waliofurahia kusomwa kwa Neno, na baraka za Bwana? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sote tunafurahia, sana.

²⁵ Sasa, kuna joto, nami ninajua baadhi yenu mnarudi nyumbani usiku wa leo. Ninajua Ndugu Rodney na Charlie, na hao wengine, inawabidi kuendesha magari kusafiri mbali sana. Na hebu kidogo, mko likizoni, sivyo? Vema, ninasikia mnaenda kuvua samaki.

“Bwana hamhesabii mtu umri wakati anapovua samaki. Huzeeki hata kidogo wakati ukivua samaki.” Kwa hiyo, sasa, ninyi wasichana ambataneni nao. Mnaona? Nami nitashuka nije nijiunge nanyi, nikiweza. Na mnajua, “Bwana mwema,” walisema, “hamhesabii mtu umri wakati akivua samaki.” Vua sana wakati unaponinii—unapojisikia umechanganyikiwa sana. Ndilo jambo lililo zuri sana la kujiburudisha nalo, nililopata kuona maishani mwangu, ni kwenda kuvua samaki.

²⁶ Nilikuwa na kadi ndogo, wakati mmoja, kutoka kwa Bw. Troutman. Kuna mtu yeyote anayemkumbuka Bw. Troutman, ile kampuni ya barafu huko New Albany? Alikuwa na kadi ndogo kule, kasema, “Huko nje kuvua samaki.” Na ikaendelea, ikisema, “Mwanamume aliye na. . . Kila mwanamume, ndugu zake, nje kwenye kuvua samaki. Pamoja na msaidizi, sikuzote wataenda, nje kuvua samaki.” Alikuwa na kama vitu vinane ama kumi mbalimbali. Na alipofikia chini, akasema, “Mwanadamu yuko

karibu zaidi na Mungu wakati anapovua samaki.” Kwa hiyo ninafikiri hiyo ni kama ni kweli. “Matajiri na maskini wote ni sawa, huko nje wakivua samaki.” Mnaona? “Anayesaidia, daima ataenda, huko nje kuvua samaki.” Na kila kitu kilikuwa ni kuhusu “Huko nje kuvua samaki.”

²⁷ Vema, nitawaambia juu ya kuvua kwingine nimekuwa nikivua kwa karibu miaka thelathini na mitatu iliyopita, nimekuwa nikivua nafsi za watu. Bwana na atusaidie kumleta kila mmoja tuwezaye kumpata.

²⁸ Sasa, usiku wa leo, huu unarekodiwa. Sasa, asubuhi ya leo, (kama Jim yupo hapa, ama anarekodi), mimi—mimi nafikiri, kwenye kanda, mtu fulani alinifahamisha jambo hilo, nilisema, “Kutoka kwa pili.” Sikumaanisha kwa *pili*. Ni, “Kutoka kwa tatu.”

Roho Mtakatifu katika umbo la Nguzo ya Moto, Mungu akishuka katika dhihirisho, alileta kutoka kwa kwanza, na—na huko nyuma katika . . . akawatoa Israeli kutoka Misri.

Kutoka kwa pili kulikuwa ni Kristo akilitoa Kanisa kutoka katika dini ya Kiyahudi.

Na, *Kutoka Kwa Tatu*, ni wakati Nguzo ile ile ya Moto inapomtoa Bibi-arusi kutoka kwenye kanisa. Unaona? Kutoka kwa ya kimwili; kutoka kwa ya kiroho; na ya Kiroho kutoka kwa ya kiroho. Hizo tatu, unaona, ya Kiroho kutoka kwa kanisa, hasa. Ndipo tunazipata hizo tatu, zile nyakati tatu zake.

²⁹ Sasa, usiku wa leo, nilitaka kurekodi kanda nyingine, na hiyo iliitwa *Je! Maisha Yako Yanaistahili Injili?* Labda haitachukua muda mrefu sana. Vema, ni Maandiko machache tu na mihtasari niliyo nayo hapa, lakini kwanza tunataka kusoma Neno la Mungu. Kabla hatujafanya hivyo, tuviinamishe mioyo yetu Kwake kwa dakika moja.

³⁰ Bwana Yesu, mtu yeyote, kimwili, ama mwanamke, ama mtoto, anaweza kuzifungua kurasa za Biblia hii, bali hakuna mtu anayeweza kuifunua ila Wewe. Ninaomba, Bwana, ninapolichukua fungu hili jinsi lilivyowekwa moyoni mwangu na kulituma kote katika mataifa, kwa ajili ya watu, wapate kujua ni maisha ya aina gani wanayopaswa kuishi. Kwa maana, wengi sana wameniliza, “Je! maisha ya Kikristo ni maisha ya ibada ya kanisani? Ni kuwasaidia maskini, wahitaji? Ama ni kuwa mfuasi wa kudumu? Je! ni uaminifu halisi kwa kanisa?” na maswali kama hayo. Baba, jibu halisi na lije, usiku wa leo, kupitia maneno haya, tunapojitahidi ku—kuyaleta kwa watu. Katika Jina lake Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

³¹ Sasa fungueni kwenye Biblia zenu, kwenye Kitabu cha Luka Mtakatifu, na tutaanzia kwenye mlango wa 14 na kifungu cha 16, kusoma Maandiko machache tupate mahali pa kusimamia, kwa ajili ya msingi, kwa ajili ya jambo hili ambalo tutajaribu kulipa

kama dakika thelathini ama arobaini. Sasa, kifungu cha 16 cha mlango wa 14 wa Luka Mtakatifu.

Akamwambia, Mtu mmoja alifanya karamu kubwa akaalika watu wengi,

Akawatuma watumwa wake saa ya chakula awaambie wale walioalikwa, Njoni, kwa—kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari.

Wakaanza wote kutoa udhuru kwa nia moja. Wa kwanza alimwambia, Mimi...nimenunua shamba, sharti niende nikalitazame; tafadhali unisamehe.

Mwingine akasema, Nimenunua ng'ombe jozi tano, ninakwenda kuwajaribu, tafadhali unisamehe.

...Mwingine akasema, Nimeoa mke, na kwa sababu hiyo siwezi kuja.

Yule mtumwa akaenda, akampa bwana wake habari ya mambo hayo yote. Basi, yule mwenye nyumba akakasirika, akamwambia mtumwa wake,...

Angalia, si watumwa. "Mtumwa."

...Toka upesi, uende katika njia kuu na vichorochoro vya miji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na viwete, na vipofu.

Mtumwa akasema, Bwana, hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa ingaliko nafasi.

...Bwana kamwambia mtumwa, Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa.

Maana nawaambia, Kwamba katika wale walioalikwa, hapana hata mmoja atakayeionja karamu yangu.

³² Sasa, mlima, kulikuwako na mivuto mitatu, ama duru tatu, za jambo hilo? Walipotoka, kwanza, na kuwaita wale waliokuwa...ama walioalikwa waje, wala hawakuja. Kwa hiyo kukaja kampeni ya uponyaji, ikatoka kwenda kuwaleta vipofu na viwete. Na bado nafasi ilikuwapo, kwa hiyo akatoka akaenda na kuwashurutisha walio wema, wabaya, na wasiojali; wanapaswa kuingia.

³³ Sasa, mnasoma mfano mwingine wa jambo hili, kinachofanana nalo, katika Mathayo 22:1 hadi 10, kama mngetaka kulisoma, baadaye. Lakini mimi—mimi nilitoa somo hili kutoka hapo: *Je! Maisha Yako Yanaistahili Injili?*

³⁴ Sasa, Yesu hapa anasema...Mwanadamu daima amejaribu kutoa udhuru, kusudi asilipokee Neno la Mungu la mwaliko Wake. Hata likithibitishwa kwao kwa dhati, ya kwamba ni—yaani ni Karamu Yake na mwaliko Wake, lakini mwanadamu daima anatoa udhuru. Na kama ukisoma Mathayo Mtakatifu

22, utaona ya kwamba udhuru ulitolewa pale, pia. Na—na wao wanajaribu. . .

³⁵ Iirudi nyuma kwenye nyakati zote. Iirudi kwenye wakati huo, na ikasema mtu aliwaalika, na—na alikuwa na shamba la mizabibu. Na tunaona mfano huo. Na jinsi ambavyo aliwatuma watumishi wake wakakusanye kutoka kwenye shamba hili la mizabibu. Mtumishi wa kwanza alikuja, wao walifanya nini? Walimfukuza. Mtumishi mwingine akaja, pia wakampiga mawe. Na wakamfukuza mtumishi baada ya mtumishi; hao watu wakatili. Mfalme akamtuma, hatimaye, mwanawe. Na mwanawe alipokuja, tunaona, ya kwamba, “Wao walisema, ‘Huyu ni mrithi. Tutamwua, ndipo tutarithi vitu vyote.’” Ndipo Yesu akawaambia, “Huyo mfalme alituma na kuwaua wauaji hao wote, na kuiteketeza miji yao.”

³⁶ Sasa, tunaona, wakati Mungu anapompa mtu mwaliko, na mtu afanye jambo fulani, ama kupokea mwaliko ambao Yeye amempa, naye anaukataa, basi hakuna kitu kilichosalia, baada ya rehema kukataliwa, bali hukumu. Ukivuka mipaka ya rehema, basi kuna jambo moja tu lililosalia, na hilo ni hukumu. Na tunaona ya kwamba Mwanadamu amefanya hivyo katika nyakati zote. Limetukia, karibu kila wakati, katika Biblia.

³⁷ Mungu alipomtuma Nuhu, mtumishi Wake, na kufanya njia ya kuepukia kwa watu wote waliotaka ku—kuokolewa. Bali watu hao walimcheka tu na kumdhihaki Nuhu. Lakini Mungu alifanya njia, bali walikuwa na udhuru. Haikuwa ni kulingana na ninii yao—na mawazo yao ya kisasa. Haikuninii. . . Haikuwa ni vile walivyoitaka, kwa hiyo wakatoa udhuru katika siku za Nuhu.

³⁸ Walitoa udhuru katika siku za Musa. Walitoa udhuru katika siku za Eliya. Walitoa udhuru katika siku za Kristo. Na wanatoa udhuru siku hizi.

³⁹ Sasa, Yeye akizungumza moja kwa moja na Israeli, wale walioitwa kwenye karamu, ambayo ningeitumia kwa watu siku hizi, kanisa, ambao wamealikwa kuja kwenye karamu, wala hawatakuja, karamu ya kiroho ya Bwana. Wala hawatafanya hivyo. Hawataki kuja. Wana mambo mengine ya kufanya. Wanatafuta udhuru.

⁴⁰ Sasa, kama Israeli, miaka elfu mbili iliyopita, wangalikubali mwaliko waliopewa, wasingekuwa kama walivyo siku hizi. Miaka elfu mbili iliyopita, Israeli waliukataa mwaliko wa kuja kwenye karamu ya arusi, na waliukataa na wakaingia hukumuni. Lakini, kama Yesu alivyosema, waliwapiga mawe na kuwaua manabii waliotumiwa, kwa kutoa udhuru, sasa, udhuru waliotoa katika kila siku.

⁴¹ Tunaona, katika siku za Yesu, ya kwamba Yeye hakuninii—Yeye hakujiunga na hata mmoja wao. Walisema, “Mtu huyu alipata elimu hii lini? Ametoka kwenye shule gani? Huyu si

Mwana wa yule seremala? Mama Yake si anaitwa Mariamu? Ndugu zake, ni Yusufu na Yakobo, na kadhalika? Na si dada Zake wako pamoja nasi? Basi mtu huyu alipata wapi mamlaka ya kufanya hivi?” Unaona? Kwa maneno mengine, Yeye hakushirikiana nao. Kwa hiyo wakasema, “Yeye ni Beelizebuli. Yeye ni Msamaria. Ana pepo, na Yeye ni mwendawazimu. Yeye ni—Yeye ni. . . Yeye ni mtu aliye na pepo mchafu, katika mambo ya dini, na imemtia kichaa. Na ndivyo ilivyo. Yuko huko nje kama mtu mkorofi. Msimjali.” Nasi tunajua lililowapata Israeli. Nao wakupaza sauti. Walikuwa na hakika sana kwamba mtu huyo alikuwa amekosea, mpaka, loo, wakati walipomhukumu, alisema—alisema, “Damu Yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu.” Nayo imekuwa juu yao tangu wakati huo.

⁴² Yesu alikuwa akijaribu kuwaambia ya kwamba udhuru wao ndio uliowaua manabii, na ndio uliowaua watu wenye haki waliokuja. Walikubali kanuni zao za imani walizopewa na wanadamu, badala ya kulichukua Neno la Mungu. Na, kwa kufanya hivyo, walikuwa wamelitangua Neno la Mungu.

⁴³ Sasa, ama inakubidi kusema, katika jambo hili, ya kwamba *Haya* ni mapenzi ya Mungu na shauku ya Mungu, au ama ni kitu kingine unachoweza kujibunia, kilicho bora kuliko Hili lilivyo. Sasa, inakubidi kuchukua moja ama jingine. Huwezi kumtumikia Mungu na mali. Na inakubidi kusema, “Hii ni ile Kweli,” ama “Hiyo ni sehemu ya ile Kweli,” ama “Yote si Kweli,” ama “Hayajawekwa pamoja vizuri,” ama “Hayajafasiriwa sawasawa.”

Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, “Neno la Mungu si la kufasiriwa apendavyo mtu yeyote.” Hakuna mtu mwingine anayepaswa kuweka fasiri Kwake, Hilo limeandikwa jinsi tu Mungu anavyotaka lifasiriwe. Vile tu lisemavyo, Kwamba, hivyo ndivyo linavyopaswa kuwa. Lichukue tu jinsi lilivyosema, jinsi lilivyoandikwa Hapa.

⁴⁴ Sasa, wanakubali kanuni zao za imani. Wanazitangua ahadi za Mungu kwao. Wanaliruka Hilo. Wataruka mbali na Hilo.

⁴⁵ Sasa, kama Urusi ingaliikubali Baraka ya pentekoste, miaka sabini na mitano iliyopita, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka Urusi, wasingekuwa ni wakomunisti leo hii. Sasa, miaka sabini na mitano iliyopita, walikuwa na uamsho mkubwa sana Urusi. Mungu alishuka miongoni mwao, na walikuwa na miamsho mikubwa, mpaka huko ndani Siberia. Nao walifanya nini? Waliukataa. Na siku hizi, nchi hiyo imekwisha, na makanisa hayawezi kufanya ibada, ila kwa ruhusa tu. Nao wameamriwa hukumu. Wameingia kwenye wazimu huu wa ghadhabu ya ukomunisti; wamejiuza kwa ibilisi.

⁴⁶ Miaka hamsini iliyopita, Roho Mtakatifu alishuka Uingereza. Mara baada ya hapo akaja George Jeffreys, na F.F. Bosworth, na Charles Price, Smith Wigglesworth, hao mashujaa

maarufu wa imani, miaka hamsini iliyopita, na wakailitea Uingereza uamsho wa Roho Mtakatifu. Lakini walifanya nini? Waliwacheka, wakawatia gereza, wakawaita wendawazimu, walidhani walikuwa wameingia kichaa. Mekanisa yaliwakataza watu kuja kuwasikiliza. Na wakawaponya wagonjwa, na kutoa pepo, na kufanya kazi kuu. Na kwa kuwa Uingereza, kama taifa, liliikataa Injili, dhambi za—zake zinajulikana kote ulimwenguni. Ni vigumu kupata taifa asi za—zaidi ulimwenguni kote, hata pamoja na Roma na Ufaransa, kuliko Uingereza. Ni mama wa uasi. Mumo humo ambamo Finney na wengi wa watu mashuhuri walimohubiri, kwenye—kwenye Soko la Nyasi Kavu, na Charles G. Finney, na Wesley, na wote hao, nalo likaikataa.

⁴⁷ Na sasa, hata juma lililopita, ama mawili, kwenye magazeti, mliona ambapo wanaume wake mashuhuri wamedhoofika sana kwenye—kwenye mapenzi ya wanawake, mpaka wapelelezi wakaingia humo. Na kiongozi wao aliwapata wengine zaidi. Magazeti yameliandika. Dhambi zao za kashfa, moja kwa moja katika serikali yao, zimesambaza jina la aibu kote ulimwenguni. Kwa nini? Ilikataa ile Kweli. Ilikuwa na udhuru wake, nayo imekwisha. Uingereza imekwisha kabisa, kwa swala la Mungu, muda mrefu uliopita. Kama . . .

⁴⁸ Marekani, miaka kumi na mitano iliyopita, wakati ule uamsho mkuu wa uponyaji ulipoendelea kutoka pentekoste, uliibuka nchini, na kulikuwako na miamsho katika makao makuu, Washington DC. Marais, makamu wa marais, watu mashuhuri, magavana; mambo makuu yalitukia, magavana na—na watu waliponywa. Kama vile, Mbunge Upshaw alikuwa kiwete kwa—kwa miaka sitini na sita, wala wasingeweza kugeuza uso wao na kusema haikutendeka. Ulikuwa papo hapo mbele zao, bali wakaukataa.

⁴⁹ Na, usiku wa leo, hiyo ndiyo sababu taifa hili linadumu. Limeamriwa maangamizi. Hakuna matumaini kwake, hata kidogo. Limevuka mstari kati ya hukumu na rehema. Nalo limekusudiwa katika yale lililo nayo hapa, kulitawala taifa hili. Nalo limeoza, kabisa. Siasa zake zimeoza. Uadilifu wa taifa hili ni duni kuliko chochote ninachoweza kuwazia. Na mfumo wake wa kidini umeoza kuliko uadilifu. Linakuwa, katika kufanya jambo hili, sasa limejiunganisha lenyewe, makanisa haya yote, na ya taifa, katika muungano wa makanisa, na limechukua alama ya mnyama. Ni kitu cha jinsi gani! Mbona? Kristo aliwapa nafasi, “Njoni kwenye karamu Yangu,” karamu ya pentekoste, ambayo inamaanisha “hamsini.”

⁵⁰ Wakati Roho aliposhuka Urusi, waliitwa kwenye karamu ya pentekoste, karamu ya kiroho, nao wakaikataa. Uingereza, Roho Mtakatifu alimwagwa juu yao, nao wakamkataa. Amerika, Roho Mtakatifu alimwagwa juu yao, nao wakamkataa.

⁵¹ Yeye alialika mara tatu. Mara tatu, alitoa mwaliko, wala hawakuisikiliza karamu hiyo. Ndipo akaalika tena, Naye akasema, “Nendeni mkawashurutishe watu hao waje.” Meza haina budi kuandaliwa. Meza iko tayari. Kungali kuna nafasi.” Nami ninaamini, ya kwamba, labda, labda mnamo miezi michahe ijayo, ama kitu kama hicho, ama mwaka mmoja, ama chochote kile, Mungu atatuma tetemeko jingine kote nchini, kwa maana bado kuna mtu fulani aliyeko huko nje, mahali fulani, ambaye ni Uzao uliokusudiwa tangu asili, ambao hauna budi kushukiwa na ile Nuru, mahali fulani, mahali fulani ulimwenguni. Taifa hili, lenyewe, limekwisha.

⁵² Nilikuwa nikiangalia kwenye gazeti la *Life* la juma hili; huko kwenye, vema, huko chini Little Rock, hivi majuzi, ama, hasa, Hot Springs. Na hapo nikaona, ninaamini ilikuwa ni gavana wa mkoa wa New York, pamoja na namna fulani ya kipusa mvua nguo huko Honolulu, akicheza dansi naye. Sasa... Na hapa, chini ya hapo, palikuwapo na mtu mwingine mashuhuri. Loo, ni fedheha ya jinsi gani! Angalia taifa letu leo. Angalia hali ya ninii yetu—ya taifa letu. Angalia mahali lilikoelekea, jinsi lilivyoanguka chini sana.

⁵³ Angalia mfumo wetu wa kidini siku hizi. Inawezekanaje ya kwamba makanisa yanaweza kuingia katika hali yaliyomo sasa? Ni kwa sababu wamekataa na kuasi Ujumbe wa Mungu, ule mwaliko wa kuja kwenye karamu. Je! ungeweza kusema kuwa maisha kama hayo yanaistahili Injili? Ungeweza kuyaita maisha, ambayo yangeketi na kuwaruhusu watu wa—wao kufanya mambo hayo, kuvuta sigara?

⁵⁴ Hivi majuzi, huku chini, kanisa fulani, timu ndogo ya ligi ilikuwa ikicheza hapa chini kwenye kiwanja cha michezo, na mvulana mdogo wa shemeji yangu ni mtupa mpira wa moja ya timu hizo. Na kwa hiyo alikuwa huko nje akitupa mpira, na kulikuwako na ligi ya kanisa iliyokuwa ikicheza. Na kulikuwako na mchungaji, akiwa pamoja na jamaa hawa wadogo huko nje uwanjani, wakicheza. Naye mchungaji alivuta sigara baada ya sigara, wa kanisa jirani yetu kabisa papa hapa karibu nasi. Na je! ungeweza kuwazia mtu... Na hata watu walioketi kwenye wasikilizaji waliliona jambo hilo. Lakini imefikia mahali ambapo hata hawajali jambo hilo.

⁵⁵ Kanisa fulani kuu, kanisa la Kibaptisti, nilijualo, huwaachilia watu watoke kwenye shule ya Jumapili, dakika kumi na tano za ziada, ili kwamba mchungaji pamoja na hao wote waweze kusimama nje na kuvuta sigara, kabla hawajarudi ndani kutumikia kazi ya Bwana. John Smith, mwanzilishi wa kanisa hilo, aliomba kwa bidii sana, kwamba Mungu atume uamsho, hata macho yake yakavimba yakijifunga usiku, naye mke wake ilimlazimu kumwongoza mezani na kumlisha kwa kijiko. Kama... Mtu huyo angepinduka kaburini mwake kama alijua ya kwamba kanisa lake limeingia katika hali hiyo. Ni

kitu gani? Walialikwa waje, nao wakaukataa. Hilo ndilo jambo pekee. Nanyi mnakumbuka, Yesu alisema, hapa ndani, ya kwamba, “Hao walioalikwa, nao wakaukataa, hawataionja karamu Yake.”

⁵⁶ Wakati Mungu anapomtuma Roho Mtakatifu na kubisha mlangoni mwa mtu, naye anamkataa maksudi, siku moja atamkataa kwa mara ya mwisho, ndipo hutakuwa mtu aliyejaliwa. Unaweza kuketi kanisani na kuisikiliza Injili, na kukubaliana na Injili hiyo. Ungeweza kiasi hata na kusema, “Ninajua ni kweli,” lakini kamwe usiweke kidole juu Yake, kulisaidia, wewe mwenyewe. Unaona? Unaisikiliza tu, maana unasema, “Ninaamini ni kweli.” Huko ni kukubaliana tu nayo.

Ningeweza kusema, “Ninaamini *hizo* ni dola elfu kumi.” Hilo halimaanishi ninazo. Unaona? Ningeweza kusema, “*Hayo* ni maji mazuri baridi,” bali nikatae kuyanywa. Mnajua ninalomaanisha?

Nao huu ni Uzima wa Milele. Na kukataa kufanya hivyo, siku moja utavuka mstari kati ya hukumu na rehema, ndipo hutakuwa na majaliwa ya kuja na kulipokea.

⁵⁷ Kwenu ninyi watu mnaohudhuria hapa. Mimi siwajibiki kwa wale ambao... ama—ama wale wanaohubiriwa na wahudumu wengine. Lakini, kama ni kweli, mnawiwa uhai wenu kwa jambo Hilo. Ungeweza kupata nini zaidi, ambacho kingekuwa na manufaa zaidi kwako, kuliko kujua ya kwamba unaweza kuwa na Uzima wa Milele?

⁵⁸ Vipi kama nilikuwa nikitoa vidonge hapa, ambavyo, imethibitishwa kisayansi, imethibitishwa kisayansi ya kwamba kidonge hiki kingekufanya uishi kwa muda wa miaka elfu? Vema, i—ingenilazimu kuwaleta wanajeshi hapa, kuwasukumia mbali na mahali hapo. Isingekubidi kufanya wito wa madhabahuni kwa hilo. Itakulazimu kuwafukuzia mbali, kuishi kwa muda wa miaka elfu moja.

Na, hata hivyo, imethibitishwa kisayansi ya kwamba Mungu wa Milele, nguvu Zake zote za kufufuka Kwake, ambazo zilikuahidi Uzima wa Milele, naye Shetani ataweka majeshi yake huko nje kukuzuia usiukaribie. Unaona? Hata hivyo, unaweza kuangalia, na uwe na hisi ya kutosha kuangalia katika uso Wake na kuona kwamba ni kweli, hata hivyo basi unaukataa. Unaona?

⁵⁹ Kitu fulani, namna fulani ya udhuru. “Kuna joto sana. Nimechoka sana. Nitafanya hivyo, kesho.” Namna fulani tu ya udhuru, hivyo tu ndivyo wanavyofanya. Kwa kuikataa siku ya kuzuriwa, inakutenganisha na Mungu.

⁶⁰ Sasa, tunaona. Na, katika Agano la Kale, walikuwa na kile kilichoitwa mwaka wa yubile. Hiyo ilikuwa ni wakati watu wote, waliokuwa ni watumwa, wangeweza kuwekwa huru wakati yubile ilipopigwa. Ndipo kama mtu hakutoka, kama kulikuwako na udhuru fulani ambao angeweza kutoa, kwamba hakutaka

kurudi kwenye nchi yake, basi ilibidi atiwe alama kwenye sikio, kwa uma, penye mwimo hekaluni. Ndipo basi haidhuru ni yubile ngapi zilizokuja, mtu huyo alikuwa ameuzwa kabisa. Kamwe asingeweza kurudi kama raia wa Israeli, tena. Alifanya nini? Aliukataa mwaliko wake. Haikumlazimu kulipa chochote. Deni ya utumwa wake ilikuwa imekwisha. Familia yake ilikuwa huru. Angeweza kurudi moja kwa moja kwenye nchi ya uenyeji wake na kuchukua mali yake. Lakini kama alikataa kufanya jambo hilo, basi hakuhesabiwa tena na Israeli, na mali yake ilipewa mwingine.

⁶¹ Sasa, jambo lile lile katika mambo ya kawaida linatumika kwenye ya kiroho. Hiyo ni kusema, kama sisi, kama warithi wa Uzima wa Milele, nasi tunaisikia Injili na kujua ya kwamba Hiyo ni kweli, nasi tunaikataa, na kukataa kufanya hivyo ama kuisikiliza, tunachukua alama ya mnyama.

⁶² Sasa, mtu fulani alisema, “Sasa, kutakuwako na a—alama ya mnyama, itakuja siku moja.” Hebu niwaambie. Imekuja tayari. Mnaona? Mara Roho Mtakatifu alipoanza kushuka, alama ya mnyama ilianza kutukia. Mnaona?

⁶³ Una mambo mawili tu. Moja ya hayo, ni, kulikubali, unatiwa Muhuri wa Mungu. Kulikataa, unatiwa alama ya mnyama. Kuukataa Muhuri wa Mungu ni kuichukua alama ya mnyama. Kila mtu anafahamu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kuukataa Muhuri wa Mungu ni kuichukua alama ya mnyama. Kwa kuwa, Biblia ilisema, “Wote ambao hawakutiwa muhuri kwa Muhuri wa Mungu waliichukua alama ya mnyama.”

⁶⁴ Wakati baragumu ilipopigwa, basi wote waliotaka kuwa huru wangeweza kuondoka. Wale ambao hawakutaka, walitiwa alama.

Sasa, mnaona, alama ya mnyama, kama tukinena juu yake katika siku za usoni, ni wakati itakapodhihirishwa, wakati utakapotambua ni jambo ambalo tayari umelifanya. Unaona? Na ndivyo ilivyo kwa Roho Mtakatifu, Atadhihirishwa. Tutakapomwona Bwana Yesu akija katika utukufu, na kuihisi hiyo nguvu ya kubadilishwa, na kuwaona wafu wakifufuka kutoka kaburini, na kujua, katika sekunde moja zaidi, tutabadilishwa na kuwa na mwili kama Wake. Itadhihirishwa. Ndipo, kuwaona wale waliolikataa, wataachwa chini, nje.

⁶⁵ Hivi Yesu hakusema wanawali walitoka wakaenda kumlaki Kristo? Baadhi yao walilala usingizi, zamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, hadi zamu ya saba. Lakini, kwenye zamu ya saba, ndipo sauti ikatokea. “Tazama, Bwana Arusi yuaja. Haya tokeni mwende mkamlaki.” Na wale waliokuwa wamelala, wakaamka. Wakati huo wote huko nyuma, mpaka Pentekoste, wakaamka. Mnaona? Kutoka wakati wa saba, wakati wa saba wa kanisa, kote kote huko nyuma,

wakaamka. Na hawa waliokuwa kwenye wakati huu wa kanisa, waliokuwa hai, walibadilishwa. Nao wakaingia.

Wakati ule ule walipoingia, wanawali waliolala walikuja na kusema, “Tunataka kununua Mafuta yenu kidogo.”

⁶⁶ Bali wakasema, “Tuna ya kututosha tu sisi wenyewe. Nendeni kwa wale wanaoyauza.”

“Na wakati walipokuwa wakijaribu kuyapokea Mafuta haya, Bwana-arusi akaja.” Hapajakuwapo na wakati katika historia ya ulimwengu, ambapo Waepiskopali, Wabaptisti, Wamethodisti, Wapresbiteri...Magazeti yamejaa. Magazeti ya kidini yanamsifu Mungu, ya kwamba wale wanawali waliolala sasa wanajaribu kuipokea pentekoste, wanajaribu kumpokea Roho Mtakatifu. Na je! hao watu hawatambui ya kwamba halitatendeka, kulingana na Neno la Mungu? “Walipokuwa wakijaribu kurudi, Bwana-arusi alikuja na kumchukua Bibi-arusi kwenda naye. Nao wakatupwa kwenye giza la nje, kwa ajili ya hukumu,” kwa maana waliukataa mwaliko wao.

⁶⁷ Watu wote wanaalikwa kuja. Mungu, katika kila wakati, ameituma Nuru Yake, na imekataliwa.

⁶⁸ Na, sasa, siku hizi si tofauti na siku nyingine yoyote, kuikataa siku ya kuzuriwa. Wakati Mungu anapolitembelea Kanisa na watu, lipokeeni basi. Usiliahirishe mpaka mwaka ujao, uamsho ujao. Huo ndio wakati, “Leo hii ndiyo siku ya wokovu.”

⁶⁹ Pia kumbukeni, Mungu kamwe hajapata kutuma Ujumbe, katika siku yoyote, ila ule Yeye aliouthibitisha kwa mambo ya kimbinguni. Yesu alisema, Mwenyewe, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Bali kama nikizitenda zile kazi, ziaminini kazi hizo kama hamwezi kuniamini Mimi,” na wakati mnapoziona zimeonyeshwa wazi na—na kudhihirishwa.

⁷⁰ Sasa wakati umewadia ambapo linalikataa, ndipo linatobolewa sikio kwa uma, ndipo kamwe halitalisikia. Sasa linajipeleka kwenye muungano wa makanisa, kwenda kuingia moja kwa moja kuichukua alama ya mnyama.

⁷¹ “Moja la malengo makuu,” mtu fulani ndiyo kwanza anipe gazeti sasa hivi, papa huyu mpya amesema, “ni kuyaunganisha makanisa pamoja.” Watafanya hivyo kwa hakika tu kama ninavyosimama hapa. Na Waprotestanti wanalihusudu. Unaona? Kwa sababu, kanisa...Biblia ilisema, Paulo, yule nabii wa Bwana, alisema, “Siku hiyo haitakuja usipokuja ule ukengeufu, kwanza, na halafu nanii...kabla ya yule mtu wa kuasi kufunuliwa. Yeye aketiye katika hekalu la Mungu, akijifanya mwenyewe, yote yaliyo juu ya Mungu; yeye, kama Mungu,” akisamehe dhambi duniani, na kadhalika. Jinsi ambavyo kitu hiki kilivyotukia! Bali kisingetukia mpaka ule ukengeufu, mpaka kanisa litakapoanza kuondoka kwenye ile

karamu ya kiroho, lijiondoe na kujiundia dhehebu. Halafu ufunuo haukudumu pamoja na kanisa.

⁷² Kumbukeni, Israeli walitembea, mchana na usiku, kwa ile Nguzo ya Moto. Wakati ile Nguzo ya Moto iliposogea, waliifuata. Pia kumbukeni, ilikuwa ni Moto usiku, na Wingu mchana. Kwa hiyo iliweza kuja, mchana ama usiku, wakati wowote. Lakini, popote ilipokuwa, upatanisho ulifanywa, kwamba hawangekosa kuiona. Ilikuwa ni Nuru usiku, na Wingu wakati wa mchana, nao wakaifuata. Naam, bwana. Jambo lile lile!

⁷³ Martin Luther aliiona. Yeye alifanya nini? Alitoka katika Ukatoliki. Bali wao walifanya nini? Walijenga ua mdogo wakajizungushia, kasema, “Sisi ni Walutheri. Haya basi.”

⁷⁴ Ndipo Wesley akaiona ikiondoka hapo. Akaenda. Wao wakafanya nini? Wakajenga ua mdogo wakajizungushia, wakasema, “Hili ndilo lenyewe.” Hiyo Nuru ilifanya nini? Ikasonga mbele moja kwa moja, tena.

⁷⁵ Wapentekoste waliiona. Wakafanya nini? Wakatoka kwa Wawesley na Wanazarayo, na kadhalika. Wanafanya nini? Wanajenga ua mdogo kulizunguka, linaloitwa, “Sisi ni wa umoja,” na “Sisi ni utatu,” na “Sisi ni United,” na yote haya. Yeye alifanya nini? Mungu alienda mbele moja kwa moja akatoka humo. Unaona?

⁷⁶ Hatuwezi kufanya hivyo. Inatubidi kufuata, kila siku, kila saa ya siku, kila hatua ya njia. Inatupasa kuongozwa na Bwana Yesu Kristo. Tusipoongozwa, tunayachukua maisha ya kimadhehebu. Na maisha yasiyomfuata Kristo, kila siku, hayastahili.

⁷⁷ Mtu ambaye ni Mkristo Jumapili, naye anaenda kanisani, anaketi huko nyuma na anafikiri kanisa ni mali yake kwa sababu yeye hufanya *hili*, *lile* ama *lingine*, na Jumatatu ataiba na kudanganya. Na wanawake watakaenda nje kwenye ufuko wa umma, na—na huko nje mitaani, wamevaa nguo zinifu!

⁷⁸ Niliwazia juu ya—ya mama wa taifa, hata asingejipodoa, kwenda mbele za papa; na anarudi, na kuanzisha shamrashamra za mtindo wa kukata nywele kichwa-maji kwa wanawake humu nchini. Na nguo hizi zote, ambazo, wakati akiwa mja mzito, kila mwanamke nchini anataka kuvaa moja ya hizo nguo za namna ya mama sasa. Hiyo ni kweli. Ni mifano. Na wanajua ya kwamba watu hao wangepanya jambo hilo. Wanaichukua roho ya ulimwengu. Na hilo si la Kanisa la Mungu aliye hai.

⁷⁹ Wanawake wanapaswa kumwangalia Yesu Kristo. Mnapaswa kumwangalia Sara na hao wengine wa Agano la Kale.

⁸⁰ Sasa, wamefikia mahali ambapo. . . Nilikuwa nikihubiri hivi majuzi usiku, mahali fulani, kuhusu wanawake kuwatii waume zao. Ati kutii? Naam. Hilo liliondolewa kwenye kawaida za ndoa,

muda mrefu uliopita. Lakini hawatafanya hivyo. La, bwana. Wanaishi Marekani, nao wanakufanya ujue hivyo. Hawatatii. Lakini, mradi tu hufanyi hivyo, kamwe usijaribu kujiita Mkristo, maana wewe siye. Sijali unacheza jinsi gani na kunena kwa lugha, kama humtii mume wako, wewe uko nje ya mapenzi ya Mungu.

⁸¹ Mwanamke anayevaa kaptura na kufanya mambo haya anayofanya mtaani, usijiite Mkristo. Unataka kuukumbatia ulimwengu na bado uushikilie ushuhuda wako. Huwezi kufanya hivyo Mbele za Mungu, wakati ukijua yaliyo bora zaidi ya kufanya jambo hilo.

⁸² Angalia, “kutobolewa sikio,” kutiwa alama, ndipo kamwe hutasikia. Kumbuka, hiyo ni ishara ya kuyafunga maskio. Hutalisikia tena. Hutasikiliza. Kamwe hutaweza tena, kufanya hivyo tena.

⁸³ Loo! “Yeye haamini *Hilo*.” Loo, jamani! “Usimwambie. Yeye analiamini.” La. “Anakwambia moja kwa moja. . .” Hajui. Bi—bibi angeweza. . . Nawauliza tu, bibi angeweza. . .

Kama nilivyohubiri Jumapili, Jumapili iliyopita usiku, juma moja lililopita usiku wa leo, juu ya “kimulimuli chekundu kinachomulika,” jinsi ambavyo u—u—ukoo wa wanawake umekuwa mrembo zaidi kuliko ulivyopata kuwa. Sasa, hilo si kitu—si kuwapinga wanawake, sasa, hilo ni niniii tu. . . lakini jinsi anavyoudhibiti huo. Unaona? Ninii. . . Amekuwa hivyo, kumweka kwenye jaribio, kama vile Hawa alivyowekwa mbele ya ule mti.

⁸⁴ Kila mtu, kila mwana amjiaye Mungu, hana budi kupitia kwenye wakati huo wa majaribio. Huu ni wakati wa wanawake, taifa hili ndivyo lilivyo, ambapo halina budi kupitia kwenye majaribio. Kama anaweza kuwa mwanamke mrembo, na kuenenda kama dada, baraka za Bwana juu yake. Lakini wakati anapoweza kujifanya ku—kujua jambo hili, na kujianika, inaonyesha kabisa ya kwamba ana ro—roho mbaya juu yake. Hokusudii kuwa hivyo, sidhani, wengi wao hawakusudii. Bali hawatambui jambo hilo.

⁸⁵ Ungeweza kuniambia ya kwamba mwanamke mwadilifu, mwenye akili angeweza kujivalisha, maskini nguo hizi fupi wanazovaa huko nje mtaani?

⁸⁶ Ninao wasichana wawili wadogo wanaoketi hapa. Sijui matokeo ya watoto hao yatakuwaje. Ninawaombea tu. Watoto, leo, mimi sininii. . . Huwezi kujua. Sijui. Hawana kinga kwa jambo hilo. Inawabidi wenyewe kusimama kwa miguu yao miwili, mbele za Yesu Kristo, na kutoa jibu. Hawawezi kuingia juu ya yale. . . juu ya—juu ya yale ninayoamini, na yale mama yao anayoamini. Sijui wanafanya nini. Lakini kwa kweli ninaamini, katika saa hii, kama hao wasichana walienda mtaani, wamevaa nguo za aina hiyo, na mwanamume awatukane, wamevaa nguo

za namna hiyo, siamini, kama ningalikuwa na nafasi, ningeweza hata kumlaumu mwanamume huyo. Hiyo ni kweli. Nawalaumu hao wasichana. Hawakupaswa kufanya hivyo.

⁸⁷ Sikilizeni. Kama mwanamume anafikiri, na wanafundisha ya kwamba, “Mwanadamu si zaidi ya mnyama. Alitokana na jamii ya wanyama.” Na angalieni, basi, hebu mweke huko nje kama...

⁸⁸ Hebu mpeleke mbwa kwa maskini jike kwenye wakati fulani, huyoo kupitia nyua na chochote kile, kwa sababu hilo jike liko kwenye hali hiyo; nguruwe, ng’ombe, kila mnyama mwingine. Na kama sisi ni uhai wa wanyama; ambao, ndivyo tulivyo, sehemu ya mwili. Na basi wakati mwanamke anapojianika jinsi hiyo, anathibitisha ya kwamba yeye ni kitu kile kile alichio maskini mbwa huyo, ama kitu kile kile, sawasawa kabisa, kwa kuwa asingekuwa akifanya jambo hilo. Yeye anajua. Maumbile yanamfundisha ya kwamba mwanamume atamwalia. Na Biblia ilisema, “Kila atakayemwalia mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake.”

⁸⁹ Hilo linaweka wakati wa kujaribiwa. Naye ibilisi anawarembesha hao wanawake, na kuwavua nguo, na kuwaanika kule nje, kukujaribu. Enyi wanaume, geuzeni vichwa vyenu. Iweni wana wa Mungu. Wanawake, ninyi vaeni kama binti za Mungu. Msiwajibike kwa uzinzi huko ng’ambo kwenye Siku ile.

⁹⁰ Kama mwanamke huyo, haidhuru ni jinsi gani asivyo na hatia...Huenda ikawa kamwe hajafanya kosa lolote, hata kamwe hajawazia niani mwake kufanya kosa. Bali wakati huyo mwenye dhambi anapoliangalia umbo hilo linalovutia la mwanamke huyo, akijua ya kwamba yeye ni mwanamume; na jinsia ya kike imo kwenye tezi moja, na moja, ya kiume, kwenye hiyo nyingine; na huyo mwenye dhambi itamlazimu kujibu kwa jambo hilo kwenye Siku ya Hukumu, ni nani aliyetenda jambo hilo, ni nani mwenye hatia? Si mwanamume. Ni wewe. Haya basi, uzinzi.

⁹¹ Hebu angalia taifa hili. Ilikuwa, wakati wao—wao walipokuwa na nguo zinazofikia magotini ambazo wanawake waliwaa, ilibidi tuagizie huko Paris ili kuzipata. Leo hii, Paris huagizia huku wazipate. Limekuwa ni chafu sana mpaka Paris haiwezi kushindana na jambo hilo. Hiyo ni kweli. Ninii yote... Kwa nini? Kuikataa Injili. Kwa nini?

Paris haikuwa Nalo. Ni asilimia mia moja Ukatoliki. Waprotestanti hata hawawezi kuingia kule. Hebu mwangalie Billy Graham. Nadhani kuna Wakristo mia sita tu huko Paris, kutoka kwa mamilioni, Wakristo mia sita, Waprotestanti. Hao si waliojazwa na Roho Mtakatifu. Hao ni Waprotestanti tu, mia

sita wa hao, kutoka katika mamilioni mara mamilioni. Wao hawakupata nafasi ya kulikataa.

⁹² Lakini watu hawa wana Injili. Na wanapoondoka kwenye Ujumbe na Injili ambayo wameiona ikionyeshwa, wanaidhihaki kwa sababu maskini fundisho fulani la kikahaba limewageuza; na mchungaji fulani akisimama mimbarani, akiwazia zaidi kuhusu dola na riziki kuliko anavyowazia juu ya nafsi, watu ambao anawahubiria, hiyo ni kweli, hilo ndilo limeyasababisha. Sasa linauongoza ulimwengu.

⁹³ Mnakumbuka, sio muda mrefu uliopita, kwenye maskani hii. Nilihubiri juu ya somo moja, karibu miaka ishirini iliyopita, “Nitawaonyesha mungu mke wa Marekani,” na tulikuwa na maskini mrembo hapa, ameketi nalo pale. Hivyo ndivyo ilivyo. Sasa hata wananini, wanalipata. Wanapata kile walichoomba. Nao watakipata. Hivyo tu.

⁹⁴ La. Hawataliamini. La, bwana. Wanakufanya ujue ya kwamba wao ni raia wa Marekani, nao wana haki ya ku—kufanya vyovyote watakavyo. Laiti. . .

⁹⁵ Hebu niwaambie. Nitawaambia sasa. La, bwana, siasa kamwe hazitafaa kitu. La, bwana, demokrasia kamwe haitafaa kitu. Demokrasia imeoza, kabisa. Kama ingeendeshwa miongoni mwa kundi la Wakristo, ingekuwa ni sawa. Bali unapoiweka huko nje ulimwenguni, inakuwa ni kupiga domo tu. Kweli kabisa.

⁹⁶ Angalieni hapa, siku hizi. Chochote chaweza kutukia, nao watakuwa ninii tu. . . Chochote, ingiza siasa kidogo, nao wataepuka mauaji.

⁹⁷ Nilipohubiri huko chini, usiku ule kujaribu kuyaokoa maisha ya hao watoto wawili. Wao wana hatia kama hatia iwezavyo kuwa. Hata yule mwanasheria aliinuka nyuma yangu pale, na akasema, “Ni sawa.” Akasema, “Siamini katika kuyaondoa maisha ya watu.” Akasema, “Kama ukiangalia kwenye taarifa zako za uhalifu, ni nani anayeuawa kwenye kiti cha umeme na kadhalika? Sio matajiri. Yeye anaweza kugharimia mwanasheria na kubuni, ujanja mchafu, na magurudumu fulani *hapa*, na mengine *hapa*, na kutoa hongo.” Akasema, “Ni watoto maskini kama hao, ambao hawana fedha za kutosha kujinunulia chakula kizuri, hao ndio wanaonyongwa. Hao ndio wanaowaua kwa umeme, mtu fulani aliye kama wanaowaita kundi la watu wajinga, nao wanashikilia tu jina lao la hukumu ya kifo.”

⁹⁸ Nikasema, “Mauaji ya kwanza yaliyopata kufanywa ulimwenguni, ndugu mmoja alimwua mwingine, wala Mungu hakuyachukua maisha yake kwa ajili ya hilo. Alimtia alama, ili yeyote asimwue. Kweli. Huyo Ndiye Hakimu Mkuu.

Naona waliwaondolea hukumu hiyo. Sasa watafanyiwa kesi nyingine. Hakika, watapata kifungo cha maisha sasa, ambacho

kitakuwa ni miaka kumi na moja, na labda wapewe kifungo cha nje. Wana hatia. Hakika. Wana hatia. Wanapaswa kufungwa gereza, kifungo cha maisha, bali si uhai wao kuondolewa. Hakuna mtu aliye na haki ya kuutoa uhai wa mwingine. La, bwana. Siamini jambo hilo. La, hashu.

⁹⁹ Loo! Wao wanasema... Mbona, hawaamini ya kwamba wako nje ya mapenzi ya Bwana, kwa sababu hayo tu ndiyo wajuayo, yote wanayotaka kusikia habari zake. Waliyafunga maskio yao wasisikie ile Kweli, mle ndani.

¹⁰⁰ Wala Wamisri hawakutaka kujua ya kwamba lile kundi la watakatifu wanaojifingirisha kule chini lilikuwa ni mapenzi ya Bwana. Wangetakaje kujua ya kwamba mtu fulani mwendawazimu alikuja kule, kutoka nyikani, mwenye masharubu yanayoning'ina chini namna *hii*, na kusema, “Farao, naja katika Jina la Bwana. Waachilie hao wana.”

Farao angesema, “Ati nani, mimi? Mtupe nje.” Unaona? “Ati mimi?”

“Usipofanya hivyo, Bwana Mungu atalipiga taifa hili.”

¹⁰¹ Bado, “Maskini wazimu huyo, mwondoshe umpeleke mahali fulani. Acha aende. Jua kwa namna fulani limeiunguza akili yake.” Unaona? Lakini lilileta hukumu, kwa sababu mtu huyo alikuwa ni nabii na alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Kweli kabisa. Hawakutaka kuamini jambo hilo.

Roma haikutaka kuliadini, pia, bali lilitukia haidhuru.

¹⁰² Israeli haikutaka kuamini ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi. “Wangewezaje, kundi la—kundi la Wagalilaya?” Wakisema, “Hawa wote si ni Wagalilaya? Walitoka wapi? Anaambatana na kundi la namna gani? Lililo maskini sana linaloweza kukusanywa pamoja, hilo ndilo kundi analoshirikiana nalo. Hao ndio wanaokuja kumsikiliza, ni watu maskini, hao watu wasiojua kitu. Hawajateuliwa. Hao si—hao si aina ya watu wenye elimu kama sisi. Wao ni kundi la maskini.” Mnasikia ikisemwa juu ya uamsho katika siku hii. “Ni kundi la namna gani linalowasikiliza? Ni watu wa aina gani wanaohudhuria mikutano hii? Hao ni watu wa aina gani?”

¹⁰³ Nilimsikia jamaa mmoja akisema, si muda mrefu uliopita... Vema, kwa namna fulani alikuwa... Alikuwa ni baba wa kambo wa Hope. Nami nilikuwa nikimwambia juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Akasema, “Sasa, ni nani angeamini kitu kama hicho, isipokuwa liwe ni kundi kama mlilo nalo huko juu?” Akasema, “Hebu acha *Nanii*, mfanya biashara hapa mjini, mwovu kama wote, hebu na aseme eti amempokea Roho Mtakatifu, ndipo ningeliadini.”

¹⁰⁴ Nikasema, “Usijali. Kamwe hatasema hilo.” Mtu huyo alikufa mara moja, bila Mungu. Unaona?

Kuwa mwangalifu kile unachofanya. Kuwa mwangalifu kwa yale unayosema. Unataka maisha yanayoistahili Injili. Kweli.

¹⁰⁵ Israeli hawakuamini jambo hilo, kundi hilo la watu. “Huyo mwendawazimu, Jina Lake Yesu wa Nazareti, aliyezaliwa,” walidhani, “mwanaharamu.” Na watu waliamini jambo hilo. Kwa maana, wao walisema, “Huyo hakuwa ni wake. Mbona, baba Yake ni Yusufu, na Mariamu alikuwa amzae Mtoto huyu mchanga kabla hata hawajaninii. . . Alizaliwa, mbona, ni haramu. Na Yeye ni nini? Ni mwendawazimu tu. Ni mmoja wa hao jamaa wa ajabu-ajabu. Msiende kumsikiliza.” Wao walifanya nini? Walikuwa wakizipeleka nafsi zao kuzimu. Walichukua. . .

¹⁰⁶ Yesu alisema, “Waacheni. Kipofu akimwongoza kipofu, hivi wote hawaanguki shimoni?” Hiyo ni kweli. Hawakujua jambo hilo. Wasingeliamini. Wasingeweza.

¹⁰⁷ Wasingeweza kuona jinsi ambavyo watu duni wenye Ujumbe rahisi, wa kukataliwa, wangeweza kusababisha taifa kuu kuangamia. Sasa sikilizeni. Wasingeweza kuelewa jambo hilo: kundi la watu duni, hafifu. Unajua, Biblia ilisema ya kwamba, “Watu wa kawaida walimsikia Yesu kwa furaha.”

¹⁰⁸ Nilikuwa na jambo fulani dogo lililotukia huko Meksiko, si muda mrefu uliopita. Jemadari Valderna, mteule wa Mungu, Nuru ilianga njiani mwake wakati mmoja, katika mmoja wa mikutano hiyo. Huyo shujaa mashuhuri Mkatoliki, mmoja wa jemadari wakubwa sana huko Meksiko, alikuja kwa unyenyekevu madhabahuni na kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Alirudi huko Meksiko. Alidumu kunisihi sana, nishuke niende kule. Hatimaye, nikaamua kushuka kwenda kule. Bwana aliniongoza, nilipata ono. Nikamwambia mke wangu. Nikashuka nikaenda kule.

Na alipofanya hivyo, yeye akiwa ni mmoja wa majemadari wao wakubwa, jemadari mwenye nyota nne, alienda hadi makao makuu, serikalini. Na, wao, ni wakali sana dhidi ya Waprotestanti kule chini, mwajua. Kwa hiyo walijua huu utakuwa ni mkutano mkubwa mno, kwa hiyo alishuka akaenda kule na kupata ulinzi wa jeshi. Na walipofanya hivyo, wakapata uwanja mkubwa. Nao walikuwa waniingize namna hiyo. Serikali ilikuwa inaniingiza.

Kwa hiyo, walipofanya hivyo, a—askofu, mmoja wa maaskofu wakubwa wa kanisa Katoliki, alimwendea, akaenda kwa gavana, na kusema, “Bwana, nasikia ya kwamba umemwalika mtu asiye Mkatoliki.”

Kasema, “Naam. Kwani kuna shida gani?”

“Mbona,” akasema, “huwezi kumleta mtu kama huyo hapa. Serikali hii haijajulikana kufanya jambo kama hilo.”

109 “Lakini,” kasema, “tumefanya hivyo sasa.” Akasema, “Mbona,” kasema “mtu huyo ni mtu mwenye sifa nzuri. Ninasikia ya kwamba maelfu ya watu huja kumsikiliza. Jemadari Valderna, yeye ni rafiki yangu msiri.” Akasema... Naye alikuwa na... Rais mwenyewe ni Mprotestanti, mwajua, Mmethodisti. Kwa hiyo akasema—akasema, “Mtu huyo ni mtu mwenye sifa njema, nijuavyo mimi.” Kasema, “Jemadari Valderna hapa, yeye ameongoka chini ya mtu huyu.” Kasema, “Mbona, yeye ni, nijuavyo mimi, mtu mwenye sifa njema.” Kasema, “Maelfu ya watu, wao wanadai, watakuja kumsikiliza.”

Ndipo askofu huyu akasema, “Ni watu wa aina gani, bwana? Wajinga tu. Hao ndio wanaoenda, kumsikia mtu kama huyo.”

110 Rais akasema, “Bwana, mmekuwa nao kwa muda wa miaka mia tano, ni kwa nini wao ni wajinga?” Hilo lilitosha. Hili lilitatua mambo. Loo, jamani! Hilo liliwang’oa pembe. Naam, bwana. Naam.

111 Ndipo wakati yule mtoto mchanga alipofufuliwa katika wafu, nilimtuma mjumbe nyuma ya mtu huyo. Mama huyo alikuwa akisema, katika Kihispaniola, “Mtoto huyo mchanga alikufa, asubuhi ya leo saa tatu.” Na ilikuwa ikinyesha sana, mvua. Tukiwa na karibu waongofu elfu kumi kwa Kristo, kila usiku.

Usiku uliotangulia, maskini mwanamume kipofu alikuwa amepokea kuona kwake jukwaani. Loo, mara tatu ama nne ya ukubwa wa maskani hii, na urefu kama *huyu*, wa shali zilizochakaa na kofia zilizowekwa hapo. Na nilinii tu... .

112 Walinishusha kwa kamba, katika duara, wapate kuniingiza ndani. Nilienda pale tu na kuanza kuhubiri, kwa imani.

Billy alikuja, kasema, “Baba, itakubidi kufanya jambo fulani, mwanamke huyo.” Kasema, “Nina mabawabu mia tatu wamesimama pale. Hawawezi kumzuia maskini mwanamke mdogo sana, mwenye uzito wa ratili mia moja, karibu.” Na mama mdogo mrembo, urefu kama *huyu*, karibu, loo, labda mtoto wake wa kwanza. Ningesema ana umri wa miaka ishirini na mitatu ama ishirini na mitano.

113 Naye alikuwa amesimama pale, na nywele zake zikining’inia chini, na akimshika mtoto mchanga. Naye angeruka ghafla kwenye mstari huo. Wanaume wangemsukuma nyuma. Angepanda juu yao, mtoto huyo akiwa pajani mwake, kwa njia yoyote, akaingia katikati ya miguu yao, ama chochote kile. Wangempeleka kule juu, na iliwalazimu kumwondoa kwa nguvu jukwaani.

114 Wala hawakuwa na kadi yoyote ya maombi ya kumpa. Akasema, “Kama nikimruhusu aingie mle, baba, na mtoto huyo aliyekufa, bila kadi ya maombi, na... .” Kasema, “Hao wengine waliosimama pale, wamesimama hapa kwa muda wa siku mbili

ama tatu, katika mvua hiyo na jua. Na kumfanya awatangulie,” kasema, “litasababisha vu—vurugu kule chini.”

¹¹⁵ Nikasema, “Ni vyema.” Ndugu Moore alikuwa pale, naye kwa namna fulani ana kipara kama mimi. Basi nikasema, “Yeye hajui nani ni nani, watu wengi sana.” Nikasema, “Tuma...” Na—na baadhi ya ndugu, mmoja wa ndugu kutoka hapa maskanini, ambaye ameenda Utukufuni sasa. Siwezi kukumbuka jina lake kwa wakati huu. Lakini alikuwa amesimama pale nyuma. Kwa hiyo nikasema, “Ndugu Moore, shuka uende kule, ukamwombee mtoto huyo. Kamwe hatajua ni nani, kama ni mimi ama ni wewe. Shuka tu uende. Wala hawezi kuzungumza Kiingereza.”

Na kwa hiyo Ndugu Moore akasema, “Vema, Ndugu Branham.”

¹¹⁶ Akaanza kutembea kwenda. Nikasema, “Kama nilivyokuwa nikisema, ba-...” Ndipo nikamwona mtoto mchanga, maskini mtoto wa Kimeksiko ameketi mbele yangu, akicheka tu. Nikasema, “Ngoja kidogo.” Kisha nikasema, “Mpisheni maskini mama huyo.”

Billy akasema, “Siwezi kufanya hivyo, baba. Yeye...”

Nikasema, “Niliona ono, Billy.”

Kasema, “Loo, hilo ni tofauti.”

¹¹⁷ Kwa hiyo tukaufungua umati namna hiyo na kumpisha. Huyu hapa anakuja, akipiga magoti yake, akiwa ameshika rozari mkononi mwake. Nikasema, “Simama.”

Kwa hiyo nikasema, “Baba wa Mbinguni, sasa sijui utakalofanya. Sijui kama unanitaka tu nimridhishe mwanamke huyu kwa kumwombee mtoto huyo mchanga, ama kitu gani. Lakini,” nikasema, “ninaweka mikono yangu juu ya mtoto huyu mchanga, katika Jina la Bwana Yesu.” Kama tu jambo lile lile nililomfanyia Ndugu Way, akilala pale sakafuni, amekufa, hivi majuzi. Ndipo lile blanketi likapigwa teke, na maskini mtoto huyo mchanga akaanza kulia kwa nguvu. Na akawa hai. Wakati...

¹¹⁸ Nikamtuma mjumbe, Ndugu Espinosa, kwenda pamoja na huyo mama kwa daktari, na apewe hati ya kiapo iliyoapiwa kutoka kwa daktari, “Mtoto huyo mchanga alikufa.” Hiyo ilikuwa kama saa nne usiku huo. “Alikufa asubuhi hiyo saa tatu, ofisini mwake, kwa nimonia.” Akapata taarifa iliyoapiwa kutoka kwa daktari.

Magazeti hayangelinyamazia hilo, mwajua, kwa hiyo iliwabidi kuja huko. Wakanihoji. Nao wakaniambia, akasema, “Unafikiri watakatifu wetu wangeweza kufanya hivyo, pia?”

Nikasema, “Ikiwa wako hai.”

“Loo,” akasema, “huwezi kuwa mtakatifu mpaka umekufa.” Haya basi. Unaona? Na hao watu. . .

¹¹⁹ Unaona, hivi majuzi, ambapo walikuwa na huyu mtawa waliyemtukuza, katika gazeti? Kwa hiyo, mtakatifu mwingine alikufa, loo, miaka mia moja iliyopita, ama kitu kama hicho, nao wakafanya. . . wamemtakatifuza sasa, wakamfanya mtakatifu. Nao walisema ya kwamba—ya kwamba yeye alifufuka kutoka kwa wafu na kumwomba mtu mgonjwa aliyekuwa na lukemia. Sivyo? Ilikuwa kwenye moja ya magazeti. Wazia tu jinsi wanavyoadhimisha jambo hilo, na ambapo kuna mamia na mamia ya matukio papa hapa mbele za watu hapa. Kitu hicho ni nini? Ni kitu cha kulifanya kanisa la Kiprotestanti lingie kwake, unaona, kulifanya liwazie jambo fulani.

Na halafu kazi halisi za Bwana, ambapo zimethibitishwa kikamilifu, zikahakikishwa, hawathubutu kuzigusia kwenye gazeti. Haya basi. Walipokea mwaliko wakaukataa. Naam, bwana.

¹²⁰ Hawawezi kufahamu jinsi Ujumbe rahisi, watu rahisi, kukataa jambo kama hilo lingewafanya kuingia katika machafuko.

¹²¹ Mwanamke fulani aliniambia, Grant’s Pass, Oregon, wakati fulani uliopita, msichana Mkatoliki alikuja hapo kuhukumu na kuandika. Alikuwa ni ripota wa magazeti, pakiti ya sigara mkononi mwake. Naye akasema, “Ninataka kuzungumza na wewe.”

Nikasema, “Unataka kusema kitu gani?”

Akasema, “Nilitaka kukuuliza maswali kadhaa kuhusu hii dini yako.”

Nami nikasema, “Ni kitu gani unachotaka kuuliza?”

Naye akasema, “Unafanya mambo haya kwa mamlaka gani?”

¹²² Nikasema, “Katika Jina la Yesu Kristo, kwa wito wa Kiungu.” Naye akaendelea, akijifanya mwerevu. Nikasema, “Hebu kidogo.”

Akasema, “Kama ilinibidi kushirikiana na kundi hilo la wajinga kule juu,” akasema, “hata nisingetaka kuwa Mkristo.” Akasema, “Na endapo hao. . . Wanasema ya kwamba watu hao wataitawala nchi siku moja.” Akasema, “Ninatumaini sitakuwapo hapa.”

Nikasema, “Usijali. Hutakuwapo.” Nikasema, “Wewe. . . kuwa na wasiwasi juu ya hilo.”

“Mbona,” akasema, “huko kupiga kote makelele na mayowe!”

Nikasema, “Na unadai kuwa ni Mkatoliki?”

Akasema, “Ndivyo nilivyo.”

123 Nikasema, “Je! ulijua ya kwamba ilimbidi bikira Mariamu mwenye heri kumpokea Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha, na kucheza katika Roho, vile vile walivyofanya, kabla Mungu hajampokea? Mnamwita mama wa Mungu.”

Akasema, “Huo ni upuuzi.”

Nikasema, “Hebu kidogo. Mimi . . .”

“Sipaswi kuiangalia Biblia.”

124 Nikasema, “Basi utajua je yaliyo kweli ama yasiyo?”

Akasema, “Mimi hulichukua neno la kanisa langu.”

125 Nikasema, “Hili ni Neno la Mungu. Hili hapa papa hapa. Ninakupa changamoto uliangalie. Na Mariamu alikuwa pamoja nao huko juu kwenye chumba cha juu, na akaupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kama hao wengine walivyofanya. Nanyi mnamwita mama wa Mungu.” Nikasema, “Halafu unawaita hao, ‘Kundi la takataka; kinyaa?’” Nikasema, “Usijali. Hutakuwako. Huna mengi ya kuhofia, kama hayo ndiyo tu unayopaswa kuhofia. Afadhali uihofie nafsi yako mwenyewe yenye dhambi, ewe msichana.” Na nikamwacha aende.

126 Sasa wazieni haya yote, aliye rahisi. Mungu hulifanya rahisi sana.

Ahabu angewezeje, Yezebeli angewezeje, hao watu waliodhani Eliya alikuwa ni mchawi, waliodhani yeye alikuwa akiwasiliana na mizimu wangewezeje? Hata Ahabu alisema, “Huyu hapa mtu ambaye amesababisha shida hizi zote kwa Israeli.”

Akasema, “Wewe ndiwe umewataabisha Israeli.”

127 Taifa hilo lingewezeje kuwazia, ya kwamba, kuukataa ujumbe wa mtu aliyejaa ndevu jinsi hiyo, hajavaa nguo za kikasisi, na kadhalika, kungekuwa ndiko hukumu yake?

Misri ingewezeje, iliyoutawala ulimwengu, mafarao, na tabaka lake na heshima? Ulimwengu haujapata kufikia mahali hapo tena, katika sayansi na kadhalika. Wangewezeje kuwazia, kumkataa nabii mzee mwenye umri wa miaka themanini, mwenye ndevu zilizoning’inia chini, nywele zenye mvi, akienda huko nje kwa kishindo, mtoro? Na akatoka nje akiwa na ujumbe, “Ama utawaachilia waende, au Mungu ataliangamiza taifa hili.” Farao angewezeje? “Utanitii, ewe Farao.”

128 Farao akasema, “Ati kutii?” Loo, yeye, Farao! Na mzee, “Mzee fulani mwendawazimu,” waliwazia, “ati kumkatalia jamaa kama huyo, kutaliangamiza taifa?” Lakini kuliliangamiza. Loo, jamani!

Hebu tuache, tukome kwa dakika chache na tuombe, na tuwazie. Tunaishi katika siku gani? Tuko wapi? Wakati mwingine wa kisasa, wa kisayansi. Afadhali tuwazie. Labda, simameni, enyi watu simameni na muombe kidogo kwa muda

kidogo, na kuwazia kidogo, mngejisikia vizuri zaidi baada ya kumaliza kufanya hivyo. Hiyo ni kweli.

¹²⁹ Mkristo si chombo, ama namna fulani ya spana malaya ya mfumo mkubwa mno wa kidini. Hiyo ni kweli. Mkristo si namna fulani ya chombo kinacholiendeleza dhehebu la kidini. Mkristo, huyo si Mkristo. Mkristo anapaswa kuwa kama Kristo. Na Mkristo hawezi kuwa Mkristo mpaka Kristo aingie ndani ya mtu huyo, maisha ya Kristo yakiwa ndani yake. Ndipo yanaleta maisha aliyoishi Kristo, nawe unafanya mambo aliyofanya Kristo.

¹³⁰ Ninazungumza juu ya kitu gani? Uhusiano wa kibinafsi na Kristo. Ni kitu gani? Je! Maisha Yako Yanaistahili Injili?

Sasa ninajaribu kuweka msingi huo hapo, kuwaonyesha ya kwamba, wanaume na wanawake waliokuwa ni wanawake wenye sifa, wanaume.

¹³¹ Biblia ilisema. Je! mliona? Jumapili iliyopita usiku, jambo fulani nililosahau kuingiza, Mwanzo mlango wa 6 na kifungu cha 4. “Hao wanaume waliojitwalia wanawake, kama wake, walikuwa ni watu wa zamani, wenye sifa.” Watu wenye sifa, wametabiriwa kuja tena. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu.” “Wanaume wenye sifa wakiwachukua wanawake,” sio wake, “wanawake; wakiyafuata mambo ya mwili yasiyo ya asili.”

¹³² Angalia Uingereza, majuma machache yaliyopita. Angalia Marekani. Angalia kila mahali, kumejaa umalaya. Watu mashuhuri, wakuu, nyadhifa kuu, wakiliaibisha taifa, wakifukuzia wanawake. Yule mtu mashuhuri kule Uingereza, kitu kama jemadari wa vita, kitu kama hicho, mbona, mliona, yeye alikuwa na mke mrembo. Picha yake ilikuwa pale, imeambatanishwa. Mwangelie huyo kahaba wa Kirusi, lakini alikuwa amealia kizinifu kabisa, na kujianika huko, kuuanika mwili wake wa kike. Naye mwanamume akaanguka kwa hilo.

¹³³ Tunachohitaji siku hizi ni wana wa Mungu. Tunahitaji watu serikalini, ambao ni wana wa Mungu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, Mfalme mzuri, mcha Mungu angeukomesha upuuzi huu wote. Kusingekuwako na mbinu zozote. Kama vile Daudi alivyofanya, alikomesha jambo hilo. Hakika alilikomesha, maana yeye alikuwa ni mfalme. Na kulikuwako tu na . . .

¹³⁴ Njia halisi, ni, Mungu awe Ndiye Mfalme, na Mungu humtuma nabii. Hivi Samweli hakuwaambia kabla hawajapata kuwa na mfalme? Alisema, “Mungu Ndiye Mfalme wenu. Nimewahi kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana ila lililotimia?”

Wakasema, “La. Hiyo ni kweli.”

“Nimepata kuwaombaomba riziki yenu?”

“La. Kamwe hujapata kutuombaomba riziki.”

“Sijapata kuwaambia jambo lolote ila lililokuwa ni la kweli, mbele za Bwana.” Kasema, “Mungu Ndiye Mfalme wenu.”

¹³⁵ “Loo, tunatambua jambo hilo. Pia tunajua wewe ni mtu mzuri, Samweli. Tunaamini Neno la Bwana hukujia wewe, bali tunataka mfalme, hata hivyo.” Unaona? Hilo ndilo wanalopata.

¹³⁶ Pentekoste ilitaka dhehebu, kwa vyovyote vile. Ikalipata. Hiyo ni kweli. Walitaka kuwa kama makanisa hayo mengine. Ndivyo mlivyo. Endeleeni, hiyo, hilo ndilo linalohitajika. Bali Mungu ndiye Mfalme wetu. Mungu ndiye Mfalme wetu. Naam, bwana.

¹³⁷ Ni kitu gani? Ni kwa sababu kwamba watu, kama walivyofanya katika siku za Kristo, kama walivyofanya katika kila wakati, wanatafuta udhuru. Wana kanuni zao wenyewe za imani. Huenda usitake kusema, “Ni—nilinunua ng’ombe, na sina budi kwenda kuona kama a—atafanya kazi ama hatafanya, ama kutoa maziwa, ama—ama ni wa ukoo gani.” Huenda usiwe na udhuru huo.

Lakini huu hapa aina ya udhuru ambao watu wangeweza kuutoa, “Mimi ni Mpresbiteri. Hatuamini Hilo. Mimi ni Mbaptisti. Hatuamini katika upuuzi kama Huo. Vema, mimi ni Mlutheri.” Vema, hilo halina uhusiano wowote na Hilo. Hilo halimaanishi ya kwamba wewe ni Mkristo. Hilo linamaanisha ya kwamba wewe ni mfuasi wa kundi la watu waliojiundia dhehebu. Nawe ni mwanachama wa nyumba ya kupanga ya Kilutheri, nyumba ya kupanga ya Kibaptisti, nyumba ya kupanga ya Kipentekoste. Hakuna kitu kama Kanisa la Kipentekoste. Hakuna kitu kama Kanisa la Kibaptisti. Ni nyumba ya kupanga ya Kibaptisti, nyumba ya kupanga ya Kipentekoste, nyumba ya kupanga ya Kipresbiteri.

Bali kuna Kanisa moja tu. Na kuna njia moja tu unayoweza kuliingia, na hiyo ni kwa Kuzaliwa. Unazaliwa katika Kanisa la Yesu Kristo, na kuwa mshiriki wa Mwili Wake, wa ujumbe wa kiroho wa Mbinguni. Ndipo ishara, ya kwamba Kristo yuko pamoja nawe, zinaishi kupitia kwako.

¹³⁸ Wakristo, loo, hamna budi kuwa na uhusiano wa kibinafsi na Mungu. Kusudi uwe mwana wa Mungu, huna budi kuwa na uhusiano na Mungu. Yeye hana budi kuwa ni Baba yako, kusudi wewe upate kuwa mwana. Na wana na binti Zake tu ndio wanaokolewa, sio wafuasi wa kanisa, bali wana na binti. Kuna kitu kimoja tu kitakachosababisha hilo, hicho ni Kuzaliwa Upya. Kuzaliwa upya ndicho kitu pekee kitakachosababisha uhusiano na Mungu. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wana na binti. Ndipo jambo hili linapotukia, basi wanaume. . .

¹³⁹ Hili hapa swali ninalotaka kuwaletea. Mtu huyo anasema, “Tunafanya nini basi baada ya kuzaliwa mara ya pili?” Wengi sana huniuliza swali hilo. “Nifanye nini basi, Ndugu Branham?”

Kama umezaliwa mara ya pili, asili yako yote imebadilishwa. Umekufa kwa mambo yale uliyoyawazia wakati mmoja.

¹⁴⁰ “Vema,” unasema, “Ndugu Branham, wakati nilipojiunga na kansia, nilipata hilo.”

Vema, basi, wakati, Mungu aliposema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Angali anawaponya wagonjwa. Angali anaonyesha ono.”

“Lakini, Ndugu Branham, kanisa langu!” Sasa, hujazaliwa mara ya pili. Unaona? Huwezi; kwa kuwa, kama Mungu yeye yule, kama maisha Yake yamo ndani yako, kama vile ulivyo katika maisha ya baba yako, na, kama Uzima wenyewe wa Mungu umo ndani yako, Roho yule yule aliyekuwamo katika Kristo, yuko ndani yako, Roho anawezaje kuishi katika Yesu Kristo na kuandika *Hili*, halafu arudi ndani yako na kulikana Hilo? Unaona? Hawezi kufanya hivyo. Ataitikia kila Neno kwamba ni kweli.

¹⁴¹ Halafu, kama ukisema, “Vema, mimi ni mfuasi mzuri wa kanisa.” Hilo halina uhusiano wowote Nalo.

Ninawajua makafiri. Huko chini Afrika, miongoni mwa ndugu zangu weusi huko, ninaona uadilifu wa hao watu ukiwa wa hali ya juu zaidi kuliko—kuliko asilimia tisini ya Wamarekani. Mbona, katika baadhi ya makabila kule, kama msichana hajaolewa mpaka amefikia umri fulani, ama anapokuwa na kimo fulani wala hakuna mtu amemchukua bado, wanajua kuna kasoro. Wanamfukuza. Anaondoa rangi ya kikabila, na anaenda mjini, ndipo anakuwa tu mwasi. Na anapoolewa, anachunguzwa ubikira wake. Kama ule utaji mdogo wa ubikira umevunjwa, basi hana budi kusema ni nani aliyevunja. Nao wanawaua wote wawili, pamoja. Hivi kusingekuwako na mauaji mengi Marekani kama hilo lingefanyika? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Unaona? Halafu ati mnawaita makafiri? Loo, jamani! Wanaweza kuja kuwafundisha watu, wanaojiita wenyewe wafuasi wa kanisa, jinsi ya kuishi maisha safi. Hiyo ni kweli.

¹⁴² Kamwe hatukupata kisa kimoja cha magonjwa ya zinaa kwenye ziara yote ya Afrika Kusini. Hawana kitu kama hicho. Haya basi. Unaona? Ni njia zetu wenyewe zilizo chafu, kama wazungu. Hiyo ni kweli. Tulimwacha Mungu.

¹⁴³ Wakati hili litakapotukia, jambo utakalofanya basi, utaona ya kwamba Roho anayeingia ndani yako, kutokana na Kuzaliwa upya, utaamini na kufanya kila kitu ambacho Mungu anasema ufanye katika Neno Lake. Na kila kitu ambacho Biblia inakunukulia kulifanya, utaliitikia kwa “amina.” Na hutakoma, mchana na usiku, mpaka utakapolipokea. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Na wakati huu wote, hakika, juu ya kila kitu, utazaa tunda la Roho.

¹⁴⁴ Unasema, “Je! nitanena kwa lugha?” Huenda ukafanya hivyo, na huenda usifanye. “Nitapaza sauti?” Huenda ukafanya hivyo. Huenda usifanye.

Bali kuna jambo la hakika utakalofanya. Utazaa tunda la Roho. Na tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uaminifu, uvumilivu, unyenyekevu, upole, saburi. Hasira yako haitakuwapo, “Looo!” Kumbuka tu, ukiwa na hiyo, hiyo inamtia sumu Roho Mtakatifu anakuacha. Unaona? Unapofikia mahali ambapo unataka kuzozana na kila mtu unayemkaribia, kuna kasoro. Unapofikia mahali ambapo ninii . . . mhudumu atasoma kutoka katika Biblia, kwamba ni makosa kufanya jambo fulani, na, utaninii . . . Kumbuka tu, hamna Ukristo hapo hata kidogo. Hiyo sasa, hiyo, “Kwa matunda yao mtawatambua.” Hivyo ndivyo Yesu alivyosema. Unaona?

¹⁴⁵ Kama ni Neno, na Mungu alisema hivyo, Roho huyo aliye ndani yako atakubaliana na hilo Neno, kila wakati. Maana, Roho Mtakatifu halisi atakubaliana na Neno, maana Neno ni Uzima na Roho. Yesu alisema, “Maneno Yangu ni Uzima.” Na kama una Uzima wa Milele, na Yeye ni Neno, Neno linawezaje kulikana Neno? Unaona? Ungemfanya Mungu kuwa mtu wa aina gani? Hilo ni jambo moja la kujua, ya kwamba wewe ni Mkristo, wakati unapoweza kukubaliana na kila Neno la Mungu.

¹⁴⁶ Nawe unajikuta ukipendana na adui zako. Mtu fulani akisema, “Vema, yeye si kitu ila mtakatifu anayejifingirisha.” Nawe unaanza kuwa . . . Kuwa mwangalifu. Kuwa Mwangalifu. Lakini wakati unapoweza kujikuta kweli, wewe mwenyewe, ya kwamba unampenda! Haidhuru wanafanya nini, ungali unawapenda. Unaona?

¹⁴⁷ Ndipo unaanza kupata, na saburi yako inatoka kwa karibu urefu *huo*, mpaka hata haina mwisho. Mtu yeyote anaendelea tu kusema mambo kukuhusu wewe, “Vema, sijali unasema nini!” Hukasiriki. Kama ukikasirika, afadhali uingie katika maombi kwanza, kabla hujazungumza nao tena. Naam. Naam.

Usiingie katika mabishano. Usipende kujiingiza katika ubishi; kama ukitaka kumwona mtu fulani akiinuka kanisani, aseme, “Mnajua nini? Hebu niwaambie, *Nanii* alifanya *hivi na vile*.”

Unasema, “Sasa ndugu, jionee aibu.”

¹⁴⁸ Kama ukisema, “Loo, ni hivyo?” Usikilize kashifa hiyo? Kuwa macho.

Roho Mtakatifu si shimo la maji machafu. Unaona? La, la. La, la. Moyo umekaliwa na Roho Mtakatifu, umejaa utakatifu, usafi. “Hauwazii maovu, haufanyi maovu; unaamini mambo yote; unavumilia, mvumilivu.” Unaona?

¹⁴⁹ Usibishane. Familia inapoanza ubishi, usibishane nao. Mama yako alisema, “Sikuruhusu kwenda kule juu, kanisa lile

la kale, tena. Vema, wewe, yote unayofikiria sasa, unaachilia nywele zako zikue sana. Unaonekana kama bibi kizee.” Usibishane na yeye.

Sema, “Sawa, mama. Ni sawa. Ninakupenda, vivyo hivyo tu. Na nitakuwa nikikuombea mradi tu ningali hai.” Unaona?

¹⁵⁰ Sasa, usibishane. Unaona? Hasira huzaa hasira. Muda si muda wajua, unamhuzunisha Roho Mtakatifu anakuacha, utarudisha ubishi tena. Ndipo Roho Mtakatifu anaruka anaenda zake. Hasira huzaa hasira.

Na upendo huzaa upendo. Jazweni na upendo. Yesu alisema, “Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo, ninyi kwa ninyi.” Hilo ndilo tunda la Roho Mtakatifu, upendo.

¹⁵¹ Na je! ulijua, wewe ni muumbaji mdogo, wewe mwenyewe? Unajua hilo? Hakika. Umeona watu unaopenda tu kuwa karibu nao. Hujui ni kwa nini. Mtu tu wa aina ya kupenda. Mmeona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni mwenye fadhili tu, hapo, unapenda kuwa karibu nao. Hiyo ni... Wao huumba mazingira hayo, kwa maisha wanayoishi, jinsi wanavyozungumza, mazungumzo yao.

Halafu, umewaona wale ambao, kila wakati, u—unawaepa. Wakati wote, wanapenda kuzungumza juu ya jambo oву, na kuzungumza juu ya mtu fulani. Unasema, “Loo, jamani! Hao hapo wanakuja. Wanaenda kumkosoa mtu fulani pale. Yupo hapa ndani sasa, ataenda kuzungumza juu ya mtu *huyu*. Yote watakayofanya ni kuzungumza mizaha michafu, ama kitu fulani juu ya wanawake, ama kitu kama hicho.” Unachukia tu kuwa karibu nao. Unaona? Wanaumba. Inaonekana, ni watu wazuri sana, lakini wanaumba mazingira hayo.

Na mambo unayowazia, mambo ufanyayo, matendo, mambo unayozungumza habari zake, huumba mazingira.

¹⁵² Niliingia kwenye ofisi ya mtu fulani, hapa kwenye jiji hili. Na mtu huyo ni mdhamini, ama shemasi, ndiyo, kwenye kanisa zuri. Niliingia mle kumwona mtu huyo kuhusu shughuli fulani. Na kuna radio kule, inaimba huo roki ama twisti, chochote kile, kwa nguvu sana ilivyoweza. Na nadhani kulikuwa na picha arobaini zilizobandikwa ofisini mwake, za wanawake walio uchi. Sasa, huwezi kuniambia ni shemasi kiasi gani, ama chochote zaidi. Hebu nione kile unachoangalia, na kile unachosoma, na aina ya muziki unaosikiliza, umati wa watu unaojikusisha nao, nami nitakwambia una roho wa aina gani. Unaona? Naam.

¹⁵³ Unamsikia jamaa fulani akisema, “Ati mimi nifanye *ninii*?” Kundi hilo... Kumbuka tu, sijali anasema nini. Maneno yake yananena kwa sauti kuu zaidi. Matendo yake yananena kwa sauti kuu zaidi kuliko yale chochote kingeweza kusema. Angeweza kushuhudia, aseme yeye ni Mkristo, hakika, na labda

afanye jambo lolote. Bali wewe angalia tu aina ya maisha anayoishi. Hayo yanaonyesha kile alichu.

¹⁵⁴ Sasa, ungeweza kuwazia hilo, mtu mwenye maisha ambayo yangesema, “Kuamini katika uponyaji wa Kiungu, hiyo ni kazi ya ndege. Hiyo ilikuwa ni miaka ya nyuma. Hakuna kitu kama hicho siku hizi”? Hayo ni maisha yanayoistahili Injili, kwamba, “Kristo alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa”? Unasema, “Lakini mimi ni shemasi.” Sijali. Huenda ukawa ni askofu.

¹⁵⁵ Nilipomsikia Askofu Sheen akisema, kama miaka miwili iliyopita, nikishuka kuja huku; kamwe sikuifungulia kumsikiliza tena. Wakati aliposema, “Mtu ambaye angeamini na kujaribu kuishi kwa hiyo Biblia, alikuwa ni kama mtu anayejaribu kupitia kwenye maji ya matope.” Askofu Sheen, kisha akageuka, kasema, “Nitakapofika Mbinguni, mnajua nini? Nitakapokutana na Yesu, nitamwambia, ‘Mimi ni Askofu Sheen,’ Naye atasema, ‘Loo, naam, nilimsikia mama Yangu akizungumzia habari zako.’” Upagani, watu ambao wangelikufuru hilo Neno. Mungu aturehemu. Mimi si hakimu. Unaona?

Neno hilo ndilo Kweli. Hakika. Na Roho wa Mungu atayatambua Maandiko Yake Mwenyewe. Yeye hutambulishwa na Maandiko Yake. Hayo—hayo—yananena habari Zake. Nawe unatambulishwa kwa kuliadini, na Hilo linakupata hati ya utambulisho wako.

¹⁵⁶ Usibishane na wengine. Wala usinii—na usiwe na ugomvi huu wa familia, kama nilivyosema. Upendo huzaa upendo. Na hasira huzaa hasira.

¹⁵⁷ Sasa, sasa hebu na tuangalie. Mwangalie Yesu, kwa dakika moja. Yeye alikuwa ni mfano wako. Natumaini hamchoki kupita kiasi. Angalieni. Hebu na tumwangelieni Yesu, kwa dakika moja. Yeye alikuwa ni mfano wetu. Alisema hivyo. “Kwa kuwa nimewapa mfano, kwamba mnapaswa kuwafanyia wengine kama nilivyowafanyia ninyi.”

¹⁵⁸ Sasa angalieni. Wakati alipokuja ulimwenguni, wakati kulikuwapo na zaidi, kutokuamini kwingi duniani wakati huo kadiri kulivyowahi kuwa, hata hakukumpunguzia mwendo. Aliendelea moja kwa moja kuhubiri vivyo hivyo, na kuponya vivyo hivyo. Hakukumsumbua. Kulikuwako na wakosoaji. Mtu huyo alikosolewa tangu alipokuwa mtoto mchanga mpaka alipokufa msalabani. Je! hilo lilimzuia? La, bwana. Lengo Lake lilikuwa ni nini? “Kufanya sikuzote yale Baba ameandika. Kufanya daima yale yanayompendeza.”

¹⁵⁹ Mwangalieni Yesu. Nena kuhusu sisi kujinyenyekeza? Wakati Mungu Mwenyewe alipofanyika mtoto mchanga, badala ya kuja katika ki—kitanda kidogo cha mtoto mahali fulani katika nyumba nzuri, alizaliwa huko nje juu ya lundo la samadi

horini, miongoni mwa ndama wa ng'ombe waliokuwa wakilia. Walimfunga nguo za kitoto, zilizotoka kwenye shingo ya nira ya maksai. Maskini kuliko maskini wote, na, hata hivyo, ni Muumba wa mbingu na nchi.

¹⁶⁰ Usiku mmoja baridi, wenye mvua, walisema, “Bwana, tutaenda nyumbani pamoja na Wewe.”

¹⁶¹ Akasema, “Mbweha wana mapango, na ndege wana viota, bali sina hata mahali pa kulaza kichwa Changu.”

Mungu, Yehova, alijinyenyekeza na kuwa Mwanadamu; akawakilishwa katika mwili wa dhambi, kukukomboza wewe na mimi. Sisi ni akina nani basi? Yeye alikuwa ni mfano wetu. Mimi ni nani? Si kitu.

¹⁶² Nilikuwa nikimwambia mtu fulani, alasiri ya leo, katika mkutano mdogo. Nikasema, “Kila mwana aliyezaliwa na Mungu hana budi kujaribiwa, kwanza, kurudiwa.” Ninakumbuka wakati nilipopata yangu, ama saa yangu iliyo kuu kabisa. Wakati mtu—wakati mtu anapozaliwa mara ya pili, kuna sehemu ndogo, kama ukubwa wa ukucha wa kidole chake, ambamo Mungu hutia ndani yake, mfumo, nao unaingia moyoni mwake na kutia nanga hapo. Kisha Shetani anamfanya athibitishe jambo hilo. Na kama huo haumo mle, umekwisha.

¹⁶³ Ninakumbuka kule hospitalini, nilikuwa na umri wa kama miaka ishirini na miwili, ishirini na mitatu, labda, kitu kama hicho, nilikuwa ni kijana mwanamume. Na baba yangu, akifia mikononi mwangu, na mimi nikizungumza na Mungu kama mponyaji. Na baba yangu mwenyewe ameshikwa na ugonjwa wa kushtuka moyo, ameweka kichwa chake mkononi mwangu, nami nikimwomba; na kumwona akiyageuza hayo macho na kuniangalia, na akalala, akaenda kukutana na Mungu. Nilimpeleka huko na kumzika karibu na ndugu yangu, na maua yalikuwa yangali mapya kaburini mwake, na huku mimi nikihubiri juu ya Mungu anayewaponya wagonjwa. Nikifanya kazi kwenye Kampuni ya Utumishi wa Umma, kwa senti ishirini kwa saa, na mke wangu akifanya kazi huku kwenye kiwanda cha shati, kutusaidia kumpatia mvulana wetu mwenye umri wa miezi kumi na minane riziki, Billy Paul, na mtoto wa miezi minane aliyekuwa akimbeba.

Nimemwona Dada Wilson akitikisa kichwa chake. Yeye anakumbuka jambo hilo; Roy Slaughter na baadhi ya watu wa zamani.

¹⁶⁴ Nilifanya nini? Nilitembea mitaani, nikiwa na sambusa mkononi mwangu, nikashuka kutoka kwenye mlingoti, na kumshuhudia kila mtu niliyekutana naye, juu ya upendo wa Yesu Kristo. Nikaenda kwenye gereji yao na kuwauliza kama ningeweza kuitumia, kuzungumza na makanika. Nikaingia mle, nikasema, “Enyi watu, mmepata kuokolewa hadi sasa? Nilipata kitu fulani moyoni mwangu.” Nikaingia madukani

usiku. Ninarudi nyumbani saa nane ama tisa alfajiri, kutokana na kuwatembelea wagonjwa usiku kucha. Nisingeninii... Nikaketi tu chini, nikabadilisha na kuvaa nguo zangu za kazi. Na nikaketi pale kitini na kupumzika mpaka kwenye mapambazuko, nikaamka nikaenda. Huku nimekonda sana, kutokana na kufunga na kuomba, mpaka ilinibidi kuomba nipate kuvaa vichokoo vyangu, nipate kupanda mlingoti. Nikihubiri, na kuhubiri, "Mungu alikuwa mkuu, Mungu alikuwa ni rehema, Mungu alikuwa ni upendo," kwa watu.

Na, hapa, baba yangu akifia mikononi mwangu. Nao ndugu zangu walikufa, aliuawa wakati nimesimama mimbarani hapa chini kwenye kanisa hili dogo la Kipentekoste la watu weusi, nikihubiri. Wakaja wakaniambia, "Ndugu yako aliuawa huko kwenye barabara kuu. Gari lilimonga na kumwua." Damu ya ndugu yake mwenyewe ikitiririka kutoka kwenye shati lake, ambapo alimwokota barabarani. Mara baada ya mimi kumzika, baba yangu akafa. Halafu, huyo hapo mke wangu amelala huko nje.

¹⁶⁵ Ndipo nikaenda, nikaja hapa kwenye maskani hii. Kutoka kwenye hili, ambapo jukwaa hili limesimama, nikawaambia watu, miezi sita kabla halijatukia, "Mafuriko yatakuja. Nami nilimwona Malaika akichukua fimbo, na kupima, 'Futi ishirini na mbili juu ya Barabara ya Spring.'"

Sandy Davis na hao wengine wameketi hapa, wakacheka, wakasema, "Ilikuwa tu ni kama inchi nane ama kumi mwaka wa 1884, kijana. Unazungumziwa na kitu gani?"

¹⁶⁶ Nikasema, "Itakuwa. Kwa sababu, nimeona moja ya njozi hizo, nayo iliniambia hivyo. Nayo yatakuwako." Na kuna alama kwenye Barabara ya Spring, leo, kwenye futi ishirini na mbili za maji. Nikasema, "Niliendesha mtumbwi juu ya maskani hii." Na niliendesha.

¹⁶⁷ Kwenye wakati huo, mke wangu akawa mgonjwa. Nikamwombea. Kisha nikaja maskanini, watu walikuwa wakimngojea. Nikasema, "Anakufa."

"Loo, ni mke wako tu, huyo."

¹⁶⁸ Nikasema, "Anakufa."

Nikaenda huko juu na kuomba na kuomba na kuomba. Na ningeinua mikono yangu. Yeye aliushika mkono wangu. Akasema, "Billy, nitakulaki asubuhi, nitasimama Kule." Kasema, "Wakusanye watoto mkanilaki Langoni."

¹⁶⁹ Nikasema, "Anza tu kuita kwa sauti kuu, 'Bill.' Nitakuwa Hapo." Unaona? Ndipo akatuacha. Nikamweka kule chini kwenye nyumba ya maiti.

Nikapanda nikaenda nyumbani, kulala. Na nilipofanya hivyo... Mtoto Billy Paul alikuwa akikaa na Bibi Broy na hao wengine, ni mgonjwa sana. Daktari alitarajia afe wakati wowote.

Mimi nikimwombea Billy. Na huyu hapa Ndugu Frank anakuja na kunipata. Kasema, “Mtoto wako anakufa, yule msichana mdogo.”

¹⁷⁰ Nikatoka nikaenda hospitalini. Daktari Adair asingeniruhusu kuingia, kasema, “Ana homa ya uti wa mgongo. Utakwenda kumwambukiza Billy Paul.” Akamwagiza nesi anipe namna fulani ya kitu chekundu ninywe, kama namna fulani ya nusukaputi, ya kitu cha kunituliza. Nami nikaacha waondohe humo chumbani, nikaitupa nje ya dirisha. Nikapitia kisiri kwenye mlango wa nyuma, nikashuka nikaingia chumba cha chini.

Huyo hapo huyo mtoto mchanga, mbele ya hospitali, wodi ya waliotengwa, nzi wote kwenye macho yake madogo namna hiyo. Nikachukua ubao wa kale wa chandarua, nikawafukuza, kisha nikakiweka juu yake. Nikapiga magoti, nikasema, “Mungu, wale pale baba na ndugu yangu wamelala, pale, na maua kwenye kaburi lao. Yule pale Hope, amelala pale. Naye huyu hapa mtoto wangu mchanga, akifa. Usimchukue, Bwana.”

¹⁷¹ Yeye alishusha tu pazia chini, kana kwamba kusema, “Nyamaza. Sitaki kukusikia, hata kidogo.” Hata asingezungumza nami.

¹⁷² Basi, kama asingezungumza na mimi, ulikuwa ni wakati wa Shetani. Akasema, “Na nilifikiri ulisema Yeye ni Mungu mwema. Ni nini haya yote unayopigia makelele? Wewe ni mvulana tu. Angalia kotekote, juu ya mji. Kila msichana na kila mvulana uliyepata kushirikiana naye anafikiri umerukwa na akili. Umerukwa.” Sasa, yeye asingeweza kuniambia hakuna Mungu, maana tayari nilikuwa nimemwona. Bali aliniambia ya kwamba Yeye hakunijali.

¹⁷³ Nikaketi usiku kucha, siku nzima. Nikamwambia Mungu hivyo, “Kwani nimefanya nini? Nionyeshe, Bwana. Usiache wasio na hatia wateseke kwa ajili yangu, endapo nimefanya makosa.” Sikujua alikuwa akinijaribu. Bali kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa. Nikasema, “Niambie kile nimefanya. Nitakirekebisha. Nimefanya nini ila kuhubiri siku nzima, usiku kucha, na kumtolea tu maisha yangu, daima? Nimefanya nini?”

Shetani akasema, “Hiyo ni kweli. Unaona, sasa, inapokuhusu wewe, na umewaambia wote ya kwamba unaamini ya kwamba Yeye ni mponyaji mkuu, na huko mtoto wako mchanga amelala pale, akifa. Yeye anakataa hata kusikia. Mke wako alikufa kwa kifua kikuu cha nimonia. Ulisema Yeye angeweza kuiponya kansa, na ndiye Huyo hapo. Sasa, unanena juu ya Yeye kuwa mwema, na jinsi alivyo mwema kwa watu. Na wewe je?”

¹⁷⁴ Ndipo nikaanza kumsikiliza. Huko ni kuhoji. Nikawaza, “Hiyo ni kweli.”

Kasema, “Yeye anaweza kutamka. Haimbidi kunena Neno. Ni *kumwangelia* tu mtoto wako, naye angeishi.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

“Na kadiri ulivyomfanyia kazi, na hata hivyo hivyo ndivyo anavyokufanyia.”

¹⁷⁵ Nikasema, “Hiyo ni kweli.” Nikaanza kuwaza. “Vema, ati nini?” Unaona? Kila kitu kikaanza kuvunjika, inapofikia kutoa hoja. Lakini, inapofikia kwenye Hilo, Hilo lilishikilia. Lilikaa pale. Nilikuwa tu karibu kusema, “Basi nitaacha.”

Lakini ilipofikia ambapo nguvu zote za kuhoji zilikuwa zimetoweka, ndipo ikafika kwenye ule Uzima wa Milele, kule Kuzaliwa upya. Vipi kama usingalikuwapo? Vipi kama haukuwa upo? Tusingefahamiana jinsi tunavyofahamiana sasa. Kanisa hili lisingalikuwa hapa namna hii, yale maelfu na mamilioni kote ulimwenguni. Lakini, Mungu ashukuriwe, ulikuwapo.

¹⁷⁶ Ndipo wakati nilipowazia, “Ati nini? Mimi ni nani, hata hivyo? Mimi ni nani, kumswali Mwenyezi? Mimi ni nani, kumswali Muumba aliyenipa uhai wangu wenyewe hapa duniani? Nilimpata wapi mtoto huyo? Ni nani aliyenipa huyo? Si wangu, hata hivyo. Yeye alinikopesha tu, kwa muda kidogo.”

Nikasema, “Ewe Shetani, ondoka kwangu.” Nikaenda kule, nikaweka mkono wangu juu ya mtoto huyo mchanga. Nikasema, “Mungu akubariki, kipenzi. Katika dakika moja, baba atakupeleka huko chini, akuweke mikononi mwa mama. Malaika wataibeba maskini nafsi yako. Nami nitakutana nawe kwenye ile asubuhi.”

Nikasema, “Bwana, ulinipa huyu. Unamchukua. Hata ukiniua, kama vile Ayubu alivyosema, bado, ninakupenda na ninakuamini Wewe. Kama ukinipeleka kuzimu, nitakupenda, hata hivyo. Siwezi kuachana nalo.” Haya basi.

Kama ingalikuwa ni mambo ya akili tu, yote yangevurugika. Bali huna budi kuwa na uhusiano wa kibinafsi. Inakubidi kuzaliwa mara ya pili.

¹⁷⁷ Hiyo ndiyo sababu wahudumu huondoka, majukumu makubwa na kadhalika. Wanasema, “Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna kitu kama mambo haya.” Kamwe hawajapata kuwa kwenye mahali pale patakatifu, kama nilivyokuwa nikisema asubuhi ya leo. Hawajui lolote kupahusu. Wanawezaje kusema ya kwamba wao ni watoto wa Mungu, na kulikana Neno la Mungu? Unawezaje kufanya jambo hilo, kumkana Roho Mtakatifu yeye yule aliyekununua?

¹⁷⁸ Loo, kumbukeni tu, Yesu alijinyenyekeza, hata mauti, kwa ajili yako. Yeye hakuzozana. Wakati walipoutemea mate uso Wake, Yeye hakuwatemea. Walipozing’oa ndevu Zake, Yeye hakuzing’oa zao. Wakati walipompiga kofi upande mmoja wa uso Wake, huo mwingine, Yeye hakuwapiga makofi.

Aliwaombea, akasonga mbele, kwa unyenyekevu. Yeye alikuwa ni mfano wa unyenyekevu.

¹⁷⁹ Alikuwa amejaa imani. Kwa nini? Alijua Maneno Yake yasingeweza kushindwa. Aliishi kwa Neno sana mpaka akawa ni Neno.

Ee Mungu! Jalia nishikilie mikono yangu miwili kwa Mungu, mbele ya wasikilizaji hawa. Jalia niishi jinsi hiyo. Jalia Neno hili lifanyike sana, hata mimi na Neno hili tuwe kitu kimoja. Jalia maneno yangu yawe Neno hili; jalia kutafakari kwa moyo wangu. Jalia awe moyoni mwangu, niani mwangu. Afunge amri Zake kwenye nguzo ya akili zangu. Azifunge kwenye nguzo ya moyo wangu. Hebu nimwone Yeye tu. Wakati majaribio yanapoibuka, hebu nimwone Kristo. Mambo yanapoharibika, jalia nimwone tu Yeye. Ninapokuwa tayari, na adui anajaribu kunifanya nikasirike, jalia nimwone Yesu. Yeye angefanya nini?

¹⁸⁰ Yeye alikuwa katika Neno sana, mpaka Yeye na Neno wakawa kitu kile kile. Angalieni.

¹⁸¹ Haikumlazimu kuzozana. Alijua Yeye na Neno walikuwa sawa. Alijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, na kwamba amri ya Mungu hatimaye ingeushinda ulimwengu. Alijua hivyo, Neno Lake. Alikuwa na imani. Alijua mahali alipokuwa. Haikumbidi kujadiliana, na kusema, “Hapa, unaweza kuja *hapa*.”

¹⁸² Ibilisi alisema, “Sasa, angalia, unaweza kufanya miujiza. Unajua Wewe una imani kuu. Unaweza kufanya miujiza. Nitakujengea jengo, kubwa mara mbili zaidi kuliko la Oral Roberts. Maana, watu wote... Ja—jambo pekee linalokupasa kufanya, waonyeshe. Ruka kutoka kwenye jengo hili hapa, uanguke moja kwa moja chini, kwa kuwa imeandikwa, unaona, ‘Malaika watakuchukua, ili usije wakati wowote ukajikwaa mguu wako kwenye jiwe.’” Unaona?

Yeye alijua alikuwa na nguvu. Alijua ya kwamba angeweza kufanya hivyo. Alijua hilo lilikuwa ndani Yake, bali hakutaka kuitumia mpaka Mungu alipomwambia aitumie. Unaona? Anataka iwe ni Mungu ndani Yake, iwe ni Neno katika yote. Na alijua ya kwamba, aliponena chochote, ni kwamba kilikuwa ni Neno la Mungu; na ingawa mbingu na nchi zitapita, Neno hilo siku moja litashinda.

¹⁸³ Yeye hakuwa mbishi wala mwenye hamaki. Yeye alinena tu Maneno ya Mungu. Kila Neno lililotoka kwenye kinywa Chake lilikuwa ni Neno la Mungu lililotiwa mafuta.

Hivi lisingekuwa ni jambo zuri sana kama tungeweza kusema kwamba, “Neno langu na Neno la Mungu ni kitu kimoja. Ninachosema, Yeye hukiheshimu, kwa kuwa sifanyi neno lolote mpaka Yeye aniambie kwanza”? Loo, huo hapo mfano wako. Hayo hapo maisha yanayoistahili Injili.

¹⁸⁴ Sio wale makuhani waliokuwa wameelimika sana na kuadibika, na kuwa na vyeo hivyo vyote vikuu, na kusimama na kusali sala ndefu, na kula nyumba za wajane, na kunyakua viti vya juu katika—katika kusanyiko, mambo haya yote pale. Walikuwa . . . Hayo hayakuwa ni maisha yanayoistahili Injili.

Lakini Yeye alikuwa anastahili Injili, sana, hata Mungu akasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu, ambaye ninapendezwa kuishi ndani Yake. Msikieni Yeye. Neno Langu ni Yeye. Yeye ni Neno Langu. Mimi na Yeye ni mmoja.”

¹⁸⁵ Alijua, angalieni jambo hili sasa. Yeye alijua ya kwamba Neno Lake hatimaye lingeushinda ulimwengu. Yeye alijua mahali Neno Lake lilikotoka. Alijua lisingeweza kushindwa, hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe.” Unaona? Yeye angeweza kusema jambo hilo. Huyu alikuwa ni Mtu Ambaye Yeye na Neno la Mungu walifanyika mmoja. Aliwaambia . . .

“Mnapaswa kufanya *hili* na *lile*.”

¹⁸⁶ Yeye alisema, “Ni nani anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi? Ni nani anayeweza kunihukumu?” *Dhambi* ni “kutokuamini.” “Ikiwa Mimi, kwa kidole cha Mungu, ninawatoa pepo, wana wenu huwatoa kwa mamlaka ya nani?” Unaona? Sivyo ilivyokuwa, kwa hivyo ilibidi iwe ni kitu kingine. Mnaona? “Ikiwa Mimi . . .

Wao walisema, “Vema, tumewatoa pepo.”

¹⁸⁷ Akasema, “Kama nikifanya jambo hilo kwa kidole cha Mungu, Neno lililothibitishwa la Mungu, basi wana wenu huwatoa kwa mamlaka ya nani? Basi iweni mwamuzi.”

¹⁸⁸ Watu wa siku Zake, na hao watu walimdhahiki, wakaongea juu Yake. Lakini, Yeye, walimdhaliisha, kila njia waliyoweza. Wakamnena kila namna ya uovu, dhidi yake, bali Yeye aliendelea.

Sasa ninataka kufunga kwa dakika moja, kwa kusema hivi.

¹⁸⁹ Watu wa siku hizi ni kundi la wendawazimu. Watu wa siku hizi ni kundi la wendawazimu. Wanaogopa kuzichukua ahadi za Mungu. Watu wa kanisa, shirika la kanisa, mashirika ya kanisa yanaogopa kuchukua changamoto ya Maandiko ya Mungu ya siku hizi. Wanatambua. Wanatambua ya kwamba hali zao za kisasa na injili yao ya kijamii wanayoihubiri haitakabiliana na changamoto ya wakati huu, si zaidi ya vile Samsoni angaliweza kuikabili katika hali yake. Ilihitaji Mungu.

Na hapa pana utaratibu ulioahidi jambo hilo. Nitalifikia hilo hivi punde.

¹⁹⁰ Ninataka kulishikilia Neno hilo, kwa dakika moja. Ingawa wanajiita Wakristo, wanachukua kanuni za imani, kanuni za kujibunia, kupachukua mahali pa Neno la Mungu. Kwa hiyo, wanaweza kuchukua kanuni ya imani, kwa kuwa

mwanadamu aliibuni. Lakini wanaogopa kuweka imani yao huko nje kwa Mungu wanayedai kwamba wanampenda. Hiyo ni kweli. Na halafu unasema ati maisha hayo yanaistahili Injili? Haiwezekani, hata wakiwa ni wafuasi wa kanisa. Lakini hayo hayaistahili Injili. La, hashu.

¹⁹¹ Injili! Yesu alisema, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafutatana na waaminio.”

Na unapokataa hizo kuwafuata waaminio, unaweza kuwa na maisha... Haidhuru, huenda kamwe usiseme neno baya, huenda ukatimiza amri zote kumi, hilo halitakuwa na uhusiano wowote nayo. Yangali hayaistahili Injili. Unaona? Yasingeweza.

Hao makuhani walizitimiza hizo, na wangali hawakustahili. Yeye alisema, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi.” Ni nani angaliweza kumwelekezea kidole mmoja wa hao watu? Doa moja la hatia, nao walipigwa mawe bila rehema. Watu watakatifu! Naye Yesu alisema, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi,” wakati Injili ilipoingia.

¹⁹² Ingawa wanajiita Wakristo, wanapenda kushikilia kanuni za imani, kanuni zao za imani. Loo! Kanuni hizo huanzisha na kutimiza mawazo ya watu wa kisasa wa siku hizi. Na mtu ambaye atafanikiwa katika siku hizi, hana budi kuambatana na mwelekeo wa kisasa wa mawazo. Hebu niseme hilo vizuri na dhahiri. Unaona? Mtu, kama utafanikiwa, inakubidi kuambatana na mawazo ya kisasa ya siku hizi. Inaninii... Wao wanazunguka, wanasema, “Loo, hivi yeye si ni kipenzi? Hivi yeye si ni wa ajabu? Anaweza kusimama pale wima sana, wala kamwe hatuweki kwa zaidi ya dakika kumi na tano. Naye mchungaji wetu hatukemei sikuzote kuhusu mambo haya.”

Aibu kwa huyo mchungaji. Mtu yeyote anayeweza kusimama mimbarani na kuiangalia dhambi ya siku hizi, wala asiikemee, kuna kasoro fulani na mtu huyo. Yeye haistahili Injili anayodai anaihubiri. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo, wanajitolea udhuru, wakisema, “Sasa, angalia, kusanyiko langu!”

¹⁹³ M—mtu mmoja alikuja hapa, si muda mrefu uliopita, kwenye kanisa fulani kuu, naye alikuwa akiandika tasnifu. Naye akasema, “Ninaandika juu ya uponyaji wa Kiungu.” Kasema, “Ndugu Branham, tunakupenda, katika dhehebu letu.” Moja ya madhehebu makubwa sana, moja ya yaliyo makubwa sana nchini, ama duniani. Naye akasema, “Tunakupenda, katika dhehebu hili.” Alikuwa papa hapa kwenye Jefferson Villa. Lakini, kasema, “Nimekuja kuchunguza huu uponyaji wa Kiungu.” Akasema, “Kuna kosa moja tu ambalo kanisa langu kweli linaona.” Unaona? Akasema, “Unashirikiana sana na Wapentekoste.”

Nikasema, “Vema, sasa, unajua, hiyo ni kweli.” Nikasema, “Hiyo ni kweli. Unajua, daima nimetamani kuwa na nafasi ya kuwaacha.” Nikasema, “Hebu nikwambie. Nitakuja mjini mwako, wewe liambie kanisa lako linidhamini.”

“Loo,” akasema, “wasingekudhamini.”

Nikasema, “Hivyo ndivyo nilivyowazia. Hivyo ndivyo nilivyowazia.”

¹⁹⁴ Kasema, “Unaona dhehebu langu halitalivumilia jambo hilo.” Huo ni udhuru kadiri ya, “Nimeoa mke,” ama “nimenunua jozi ya ng’ombe.” Sijali una digrii ngapi za udaktari, na jinsi unavyotegemewa, na dhehebu lako. Huduma ya aina hiyo haiistahili Injili iliyoandikwa katika Kitabu hiki. Kweli.

¹⁹⁵ Mfuasi yeyote wa kanisa atakayeunga mkono upuuzi kama huo, na kujiita wenyewe Mkristo! Na kutoka kwenda hapa nje na kuishi. . . Na wanawake wakikata nywele zao, na kuvaa nguo ambazo Biblia inasema wasizivae. Wanaume wakifanya jinsi wanavyofanya sasa, “mfano wa utauwa,” wakinywa vileo na kuvuta sigara, na kuoa mara kadhaa na kuwa mashemasi wa kanisa na hata wachungaji, na kadhalika. Na watu wanaovumilia upuuzi kama huo, maisha ya aina hiyo hayaistahili Injili.

¹⁹⁶ Mwanamke atakayetembea, na kushika simu na kupiga umbeya, na kuanza kuleta misukosuko kanisani, na mambo kama hayo, hayo si maisha yanayoistahili Injili ambayo tutaiwakilisha. Mtu yeyote atakayelivunja kanisa, na kuanzisha ugomvi kati ya watu, na mambo kama hayo, haistahili Injili tunayohubiri. Kweli kabisa. “Ni mfano wa utauwa, akikana nguvu zake,” nguvu za Mungu ambazo zinakuzuia kufanya hivyo.

¹⁹⁷ Angalia, sasa, hawafanyi jambo hilo. Hawatalifanya kabisa. Wana udhuru, kwamba, kanisa lao haliadini Hilo. Wao. . .

Vema, lakini, Yesu angesema—angemwambia mtu, usiku wa leo, angenena na moyo wake na kusema, “Ninakutaka uende, ukaihubiri Injili yote.”

“Kanisa langu haliadini Hilo, Bwana. Samahani, tafadhali. Nina jukumu zuri. Mimi—mimi—mimi, unajua, mimi ni mchungaji, moja ya makanisa yaliyo makubwa mno humu mjini, Bwana. Loo, tunalisifu Jina Lako kule chini! Naam, bwana. Hakika tunalisifu. Siwezi kufanya hivyo.” Udhuru ule ule, jambo lile lile. Kwa hiyo hawaji kwenye karamu ya kiroho ya Neno Lake la ahadi, lililothibitishwa.

¹⁹⁸ Je! hivi Yesu hakusema, “Palipo na mzoga, ndipo watakapokutanika tai”? “Tai,” si mwewe, sasa. Tai! Mahali yalipo matapiko, na ninii—na ninii—nyama iliyooza, basi mwewe wanakutanika. Lakini palipo na Nyama safi, ya leo,

tai watakutanika. Unaona? Hakika. Ambapo Neno, Chakula cha tai, watakutanika.

¹⁹⁹ Kwa hiyo hawaji kwenye karamu ya kiroho walikoalikwa. Je! mnaamini ya kwamba Mungu ameipa Marekani mwaliko, miaka kumi na mitano iliyopita, kwenye uamsho mkuu, kwenye karamu ya kiroho? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! walikuja? La, bwana. La, bwana. Basi, kukataa kuja, je! maisha hayo yanaistahili Injili, ingawa wanajiita hivyo?

²⁰⁰ Wakati mtu mmoja aliponijia, si muda mrefu uliopita, na kuketi mezani, na kusema, “Ndugu Branham, ninataka kuunyosha mkono mezani,” mtu mashuhuri, “ninataka kuushika mkono wako. Ninakupenda.” Nilikuwa kanisani na nikamsikia akihubiri. Kasema, “Ninakupenda. Ninaamini wewe ni mtumishi wa Mungu.”

Nikasema, “Asante, daktari. Ninakupenda, pia.”

Akasema, “Ninataka kukwambia jinsi ninavyokupenda, kama ndugu.” Kisha kasema, “Je! unamwona maskini malkia wangu anayeketi hapa, mke wangu? Je! unamkumbuka?”

Nikasema, “Namkumbuka.”

Kasema, “Daktari alimpa majuma mawili ya kuishi, akiwa na bonge la kansa ya kufisha. Nawe ukaja mjini na kumwombea. Kisha ukaangalia juu, na kuona ono. Ukageuka na kuniambia, ‘BWANA ASEMA HIVI, ataponywa.’” Doa kubwa mgongoni mwake, lililodidimia namna *hiyo*, lilionekana kama ninii kubwa mno...kama sehemu ya ziwa la mwanamke lililobonyezwa ndani, mgongoni mwake, papo hapo kwenye uti wake wa mgongo. Hamna hata alama yake, leo. Kasema, “Huyo hapo malkia wangu ameketi, anaishi leo.” Kasema, “Ningefanya kitu gani ila kukupenda, kwa ajili ya kuomba ombi hilo la imani? Nitaachaje kukuamini wewe kuwa u m—mtumishi wa Bwana, wakati uliponiona, na kuniambia kile hasa kitakachotukia?” Akasema, “Sasa nina jambo fulani kwa ajili yako, Ndugu Branham.” Akasema, “Mimi ni mfuasi wa shirika kubwa sana la Kipentekoste lililopo.”

Nikasema, “Naam, bwana. Ninajua jambo hilo.”

Akasema, “Nilizungumza na ndugu hao, sio muda mrefu uliopita, nao wakaniambia niwasiliane nawe, na nikwambie ya kwamba ni aibu kwamba uliichukua huduma iliyotoka kwa Mungu ukaipeleka kwa kundi la watu ng’ambo ya mto na kote namna hiyo.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli?”

Akasema, “Naam.” Kasema, “Mungu aliituma huduma hiyo kulenga zile sehemu muhimu sana za ndani, sehemu kubwa, mambo muhimu.”

²⁰¹ Nikamwona ibilisi akizungumza papo hapo. Nikawaza, “Naam. ‘Ruka chini kutoka kwenye mlima huu, na uonyeshe, wajua, kutoka kwenye jengo hili.’” Unaona? Unaona?

Nikawaza, “Hebu mwongoze tu mbele kidogo.” Mama yangu mkongwe alizoea kusema, “Mpe ng’ombe kamba ya kutosha, atajinyonga mwenyewe.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli?”

“Naam.” Kasema, “Ni aibu, nunua kile uwezacho?” Kasema, “Wewe ni kitu gani? Siku hizi ni vigumu mtu kujinunulia mlo.” Kisha kasema, “Waangalie Oral Roberts na hao wengine, walioingia ndani, nao wakatoka huko wakiwa na sehemu moja ya mia moja ya huduma uliyo nayo. Angalia walicho nacho.”

Nikasema, “Naam. Hiyo ni kweli.” Unaona?

Ndipo akasema, “Kundi langu litakuchukua. Tutakuingiza moja kwa moja ndani, kama—kama mmoja wa ndugu zetu. Wote watakuunga mkono katika ushirika, na tutakodi ndege, na kukupa mshahara wako wa mia tano kwa juma, ama zaidi ukitaka. Na tutakutuma katika kila mji mkubwa nchini.” Hili lilitendeka moja kwa moja huko Phoenix, Arizona, papo hapo tukiangaliana mezani. Naye akasema, “Nasi tutalipia ninii yako...” Kasema, “Basi acha ulimwengu, ulimwengu wa nje, acha wenye vyeo, watu wakubwa, walio shamiri...” Kasema, “Daima unazungumza juu ya watu hohehahe. Tuna wa tabaka la juu sana.” Kasema, “Acha wauone mkono wa Bwana. Kisha nitawaacha wamchukue mke wangu waende naye, na wengine, wanaoweza kuthibitisha kwamba mambo hayo unayosema hutimia.”

²⁰² Kasema, “Naam, bwana. Hilo lingekuwa ni jambo zuri sana.”

Sasa, unaona, mtu huyo, katika kiwango cha D.L., L.L.D., mwandishi wa vitabu, unaona, daktari wa fasihi, mwandishi mzuri, mtu mzuri. Unaona? Hakujajua Maandiko.

Je! mnajua yule Malaika aliyefanya kazi za aina hiyo kamwe hakuenda Sodoma? Yeye alikaa na kundi la walioitwa watoke, Ibrahimu.

Kamwe hakujua jambo hilo. Niliachana tu naye, nilikaa tu hapo kidogo. Ninataka tu kujua mtego ulikuwa ni nini. Nikasema, “Vema, itanibidi kufanya nini?”

Kasema, “Vema, Ndugu Branham, jambo pekee walilosema... Tulilijadili, mambo machache, mambo madogo-madogo yasiyo muhimu unayofundisha, kwamba uyaweke kando.”

Nikasema, “Kwa mfano, yapi, ndugu?”

“Loo,” akasema, “ubatizo wako, unajua. Unajua, kwa namna fulani wewe unabatiza kama wa umoja, kitu kama hicho.” Kasema, “Mambo madogo kama hayo.”

Nikasema, “Kumbe?” Nikaendelea.

Naye akasema, “Ushahidi wa kwanza; na wahubiri wanawake; na mambo machache madogo tu kama hayo.”

²⁰³ Nikasema, “A-ha?” Nikasema, “Unajua, ninashangaa ya kwamba mtumishi mmoja wa Mungu angemshawishi mtumishi mwingine wa Mungu, baada ya kunisifu mimi jinsi ulivyonisifu, na kuniita nabii, na ukijua ya kwamba Neno la Bwana, ama ufunuo wa Neno, humjia nabii. Kisha unageuka, Daktari Pope, (halishuhudii akili yako nzuri), na ungesema na kunishawishi, mtumishi mmoja wa Mungu, unamsihi mtumishi mwingine wa Mungu apatane juu ya jambo ambalo . . . ? . . . linamaanisha zaidi kwake kuliko uhai wenyewe.” Nikasema, “La, bwana, Ndugu Pope. Kamwe siwezi kufanya jambo hilo. La, bwana.”

Ni kitu gani? Kuna chembe ya Uzima wa Milele; uishi ama ufe, uwe mtu mkubwa ama si mtu mkubwa.

²⁰⁴ Nilipitia hapo, hivi majuzi . . . Sio kuwadhara watu hawa wawili. Nikaangalia huko, na kulikuwako na picha kubwa mno hapo Tulsa, Oklahoma; makazi mapya ya Oral Roberts yanakuja, seminari ya kuwaelimishia wahudumu. Yatakuwa ni ya gharama kubwa. Na ninajua Demos Shakarian, Ndugu Carl Williams, na wengineo walio kwenye Baraza la wadhamini wa hilo. Dola milioni hamsini, pamoja na jengo la dola milioni tatu; mvulana Mpentekoste, hayo ni mambo makubwa mno ambayo Mungu amemfanyia.

²⁰⁵ Nawazia, “Ati mimi, niwe na seminari? Ninaipinga, kwanza kabisa.”

²⁰⁶ Nayo ilisema, “Makao ya baadaye ya seminari kuu ya Oral Roberts.” Nikaendelea kushuka kwenda barabarani, kulikuwako na kitu kikubwa sana cha kisasa. Na Oral Roberts, akiwa katika hema dogo kuu kuu, alikuja kwenye mkutano wangu huko kwenye Jiji la Kansas, Kansas.

Ilisema, “Makao ya usoni ya Tommy Osborn,” loo, jamani, mahali pa karibu dola milioni tatu ama nne pakijengwa namna hiyo.

Na hapo, Tommy Osborn, mmoja wa Wakristo walio bora sana. Yeye ni mtu halisi, mtu halisi aliyetumwa na Mungu. Alisimama upande wa pili wa barabara pale; maskini mvulana mdogo, mwenye wasiwasi, mvulana mdogo na msichana mdogo kwenye gari; akaja mbio, akatoka. Kasema, “Ndugu Branham, nilikuwapo pale wakati nilipomwona yule mwendawazimu akitoka nje mbio. Nami nilikuona ukikielekeza kidole chako usoni mwake, na kusema, ‘Katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yake.’ Nilimwona akianguka kuikingama miguu yako; baada ya kutoa unabii wake, aliposema, ‘Usiku huu, nitakupiga nikurushe nje miongoni mwa lile kusanyiko la watu elfu sita na mia tano.’” Kisha kasema, “Nilikuona ukisimama pale, hukuinua kabisa sauti, na kusema, ‘Katika Jina la Bwana, kwa kuwa umempa

changamoto Roho wa Mungu, usiku huu, utaanguka miguuni pangu.’ Akasema, ‘Nitakuonyesha nitaangukia kwenye miguu ya nani.’”

²⁰⁷ Na nikasema, “Toka ndani yake, Shetani.” Alianguka tu nyuma na kuikandamiza miguu yangu sakafuni.

Akasema, “Mungu ni Mungu, Ndugu Branham. Hivyo tu.” Kasema, “Nilijifungia nyumbani kwa siku mbili ama tatu.” Yeye hachezi. Yeye atasimulia jambo hilo. Halionei aibu. Kasema, “Je! unafikiri nina karama ya uponyaji?”

²⁰⁸ Nikasema, “Sahau hiyo, Tommy. Ulitumwa ukaihubiri Injili. Nenda, ukaihubiri. Ambatana na Ndugu Bosworth kule.”

²⁰⁹ Nikaangalia pale, na nikaona. Nilianza mbele ya hao wawili.

Nikawazia, “Huyo hapo Oral Roberts akiwa na mitambo mia tano, ambapo hakuna hata mkono wa mwanadamu unaozigusa barua; dola milioni nne kwa barua, mwaka jana.” Milioni nne; robo ya fedha zote zilizochangwa, katika ulimwengu mzima wa Ukristo, kote. Robo moja ya fedha zote katika Ukristo wote zinaingia kwa mtu mmoja. Ni mahali pa jinsi gani! Nilitoka nikaenda kule kupaona.

²¹⁰ Na, sasa, Oral ni ndugu yangu. Jamani! Nampenda. Yeye ni jamaa halisi, mtu halisi, nami nampenda. Naye ananiheshimu kupindukia, nami namheshimu vivyo hivyo, pia. Ni kwamba tu hatukubaliani juu ya—juu ya Maandiko.

Na, Tommy Osborn, sio bora zaidi. Ninamheshimu kupindukia. Ni mmoja wa watu walio wazuri sana niliowahi kukutana nao, Tommy Osborn.

“Na hao watu,” nikawazia, “nilipoingia ofisini mwao na kuona yale waliyokuwa nayo, nafikiri ningeona aibu wao kuja, kuona yangu: maskini mashine moja ndogo ya chapa, nasi tukijaribu kuzituma barua. Na ni kitu cha jinsi gani! Imewekwa mwishoni mwa trela, wakati huo. Nikawazia, “Hicho kingekuwa ni nini?”

Ndipo nikatoka nje. Nikawaza, “Vema, ‘Makao ya usoni ya Oral Roberts.’ ‘Makao ya baadaye ya Tommy Osborn.’ Mmoja haongei na huyo mwingine.”

Kwa hiyo, nikashuka kwenda barabarani. Nikawaza, “Lakini na mimi je?”

²¹¹ Ndipo Kitu Fulani kikasema, “Angalia juu.”

²¹² Nikawaza, “Naam, Bwana, nijalie niweke hazina zangu Mbinguni, kwa kuwa huko ndiko uliko moyo wangu.” Sasa, sisemi hayo kwa kujionea huruma. Ninasema jambo hilo kwa maana lilitukia, na Mungu anajua ya kwamba hayo ni kweli. Unaona?

²¹³ Hazina zako ziko wapi? Je! unataka kuwa mtu fulani mkubwa? Kama ndivyo ulivyo, wewe hu chochote. Unafikia

mahali ambapo hata hutaki kuwa mtu mkuu. Unataka kuwa maskini mtumishi mdogo mnyenyekevu wa Kristo. Hiyo ndiyo njia ifaayo. Hivyo tu.

²¹⁴ Ndugu Boze na hao wengine wanaanzisha kanisa huko Chicago. Iliwalazimu kuliacha kanisa la Philadelphia kwa dhehebu hilo. Sasa walikuwa wakizungumza juu ya kumpata mtu fulani mwenye koti lililokunjwa namna *hii*, DD fulani. Nikasema, “Mnaelekea kupotea. Kama mnataka kumpata mchungaji halisi kwa ajili ya kanisa hilo, mchukueni maskini jamaa mzee ambaye karibu hawezi kulisoma jina lake, na moyo wake unawaka moto kwa ajili ya Mungu. Mchukueni tu jamaa huyo. Huyo ndiye mnayepaswa kumchukua, mtu fulani ambaye hayajui mambo haya yote, mtu ambaye hatalazimisha na kusukuma, na kuwaingiza kwenye kila namna ya madeni, chochote kile, na atawalisha tu kwa Neno la Mungu. Mtu wa aina hiyo ndiye mnayepaswa kumchukua.”

Kwa hiyo, hawatakuja kwenye karamu ya kiroho. Sina budi kufunga. Nimepita wakati sasa. Mnamo kama dakika sita, tutawaruhusu mwondoke, Bwana akipenda.

²¹⁵ Ninawasikia wengine wakisema, “Lakini, Ndugu Branham, afadhali ughairi tamshi hilo.” Wakisema, “Watu si wendawazimu. Watu hawa si wendawazimu. Wameelimika tu.” Wao ni wendawazimu walioelimika, basi. Hiyo ni kweli. Naam. “Wao si wendawazimu. Wameelimika.”

Basi ninataka kuwaulizeni swali. Mnaona? Mnaelewa. Ninataka kuwaulizeni swali basi. Naomba myaeleeze matendo yao ya siku hizi, kama wao si wendawazimu. Niambieni ni kitu gani kinachowafanya kufanya jinsi wafanyavyo, kama wao si wendawazimu; mnaona, kila mtu akilitetea dhehebu lake, walafi. Yesu hakuwa hivyo. Yeye hakuwa na haraka ya chochote. Mnaona? Hakuwa mlafi. Alikuwa ni mfano wetu.

²¹⁶ Uhalifu, taifa, taifa lina uhalifu mwingi kuliko lilivyowahi kuwa nao. Kuna shida gani? Matineja, wafuasi wa kanisa, wakiyatao maisha, wanaume wakiwapiga risasi wake zao na familia, na kuwachoma moto watoto wao. Pia angalia wimbi la uhalifu. Ati wao si wendawazimu? Basi kuna shida gani? Wana matendo gani?

Mataifa yaliyoingwiwa na kichaa cha uongozi, kila moja likitaka kuiteka kila...hayo mengine na kuyafanya bendera moja, taifa moja, hiyo iwe ndiyo bendera yao na taifa lao. Kichaa cha uongozi!

²¹⁷ Utovu wa uadilifu, mbona, ulimwengu una utovu wa uadilifu mwingi kuliko ulivyowahi kuwa. Wanawake walio uchi mitaani, wanawake walio uchi, na mnasema ati wana akili timamu? Hawawezi kuwa. Hawawezi kuwa kabisa.

²¹⁸ Sikilizeni. Kulikuwa na mtu mmoja katika Biblia aliyevua nguo zake, huyo alikuwa ni yule Jeshi. Alikuwa amerukwa na

akili zake. Wakati Yesu alipompata na kumrejeshea akili zake timamu, alivaa nguo zake. Ni kweli.

Ni kitu gani kinachokufanya uvue nguo zako? Ibilisi. Hiyo ni kweli. Halafu msembe ati wao si wendawazimu? Hebu anza kuendesha motokaa hapa chini mtaani, uendeshe majengo manne ya mji bila kumwona mwanamke aliye uchi, kisha urudi uniambie. Vema. Tafuta kujua.

²¹⁹ Halafu msembe ati hao si walioharibikiwa na akili? Basi kuna shida gani? Hawawezi kuwa na akili timamu. Mwanamke mwenye akili timamu asingefanya hivyo; ana akili bora zaidi. Anajua mahali anajianika huko nje. Kundi la pepo waliojaa tamaa mbaya huko nje, wanaume wachafu tu, wenye kinyaa, wenye najisi walevi, wauaji, kila kitu. Mnasema . . .

²²⁰ Dunia inakunywa pombe nyingi zaidi siku hizi. Wanatumia fedha nyingi zaidi kwa pombe, Marekani, kuliko wanavyotumia kwa vyakula. Nafikiri ni...Ninasahau deni la pombe linagharimu mara ngapi zaidi kila mwaka, humu nchini, kuliko lilivyokuwa. Na unywaji pombe unafanya nini? Unakupeleka kwenye hospitali ya wendawazimu.

²²¹ Kansa. Wakati madaktari wa tiba kutoka kote duniani wanaandika kwenye magazeti, na kuwaambia, "Kansa chungu nzima." Sigara. Zikiwekwa juu ya panya, na wamethibitisha ya kwamba zinakupa kansa ya mapafu. Asilimia sabini yao wanapata kansa ya mapafu kutokana na kuvuta sigara. Na hao wanawake na wanaume watazivuta moja kwa moja na kuzipulizia usoni mwako. Iwapo huo sio wendawazimu, wendawazimu ni nini basi?

²²² Wakati, Injili ya Yesu Kristo inaweza kuhubiriwa na kuthibitishwa, na Mungu wa Mbinguni katika umbo la Nguzo Yake ya Moto anapeperuka juu ya watu na kuonyesha ya kwamba Yesu Kristo yuko katika sehemu ya mwisho ya kuja Kwake, akiwapa ishara ya mwisho. Na wanacheka Hiyo na kuidhihaki, na kujiita washiriki wa kanisa; halafu msembe ya kwamba wao si wendawazimu? Elezeni jambo hilo. Wakati wangu unazidi kwenda. Lakini ulizeni tu kama hao si wendawazimu. Hakika. Wao ni wendawazimu wenye elimu. Hiyo ni kweli kabisa. Elezeeni hali yao. Hamwezi.

²²³ Wanakata nywele zao, wanavaa nguo za kilimwengu, wanatembea nje mitaani jinsi hiyo. Na Biblia ya Mungu inaonya dhidi ya jambo hilo, hata inamkataza mwanamke hata kuomba akiwa amekata nywele. Na inasema ya kwamba mwanamume. . . Na yeye anafanya hivyo. Anadai, mwenyewe, kwa mumewe, ya kwamba yeye ni mzinzi, mwenyewe, naye ana haki kamili ya kumpa talaka na kumfukuza kwake. Hilo ni sawa kabisa. Neno la Mungu likinena hivyo, na wanawake watasikia hilo, na kuendelea kukata nywele, naye ajiite Mkristo. Kama huo si wendawazimu, wendawazimu ni nini? Ninataka

mtu fulani aniambie wendawazimu ni kitu gani, basi. Naam. Wao ni wendawazimu.

²²⁴ Wenye elimu kubwa mno, madigrii, chuoni! Tunaweka wakati mwingi zaidi katika kuwaelimisha watoto wetu, kwa—kwa aljebra na biolojia, kuliko tunavyofanya kwa Biblia na Yesu Kristo. Hakuna mtoto humu nchini asiyeweza kukwambia David Crockett ni nani. Hakuna theluthi moja yao inayoweza kukwambia kwamba Yesu Kristo ni nani. Halafu, ati si wendawazimu? Hakika, ni wendawazimu. Jinsi tungeweza kuendelea mbele zaidi na zaidi, jinsi wanavyofanya!

²²⁵ Kumbukeni tu. Nayo makanisa yanaidhinisha jambo hilo, wakati Biblia inalihukumu. Hivi huduma ni wendawazimu? Wendawazimu wenye elimu. Hiyo ni kweli kabisa. Makanisa yanaliidhinisha.

²²⁶ Mkumbukeni Lutu. Yeye alikuwa ni mtu mwerevu. Mwangalieni, kwa dakika moja tu sasa. Msininii—msininii... Hebu tusininii...

Samahani kwa kupitisha kidogo dakika kadhaa. Hili ni—hili ni muhimu sana. Litasambazwa kwenye... Mmekuja kunisikia nikiirekodi kanda hii.

²²⁷ Angalieni. Angalieni. Sasa, hebu kidogo tu. Ombeni kwa sekunde moja tu, moyoni mwako, “Bwana, jalia nilione.” Fungua ufahamu wako. Mungu na aufungue. Angalia kwenye... Lichukue tu taifa hili, pekee. Hebu na tuseme yale Mungu aliyosema.

²²⁸ Biblia ilisema, ya kwamba, “Dhambi za Sodoma ziliitesa roho yenye haki ya Lutu siku baada ya siku.” Yeye hakuwa tu na ujasiri wa kutosha kuzikemea. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Asingeweza kuzikemea, kwa kuwa yeye alikuwa ndiye meya wa jiji hilo. Asingelizikemea. Lakini Biblia ilisema, ya kwamba, “Dhambi za—za Wasodoma ziliitesa nafsi yake.” Alijua ilikuwa ni makosa, bali hakuwa na ujasiri wa kufanya hivyo, kuzipinga.

²²⁹ Sasa angalia. Ni Lutu wangapi Marekani, jana, wakisoma Biblia yao, kuuandaa ujumbe wao wa siku hiyo, nao walikabiliwa na ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo? Ni wangapi wao walikabiliana na ubatizo wa Roho Mtakatifu? “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele”? Marko 16, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio”? Yohana 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya”? “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo nalo litatendwa”? Ni Lutu wangapi walioliona Hilo? Lakini, kwa sababu ya udhuru wao, wa dhehebu lao! Ninii... Waliangalia na kuona katika Biblia.

²³⁰ Angalia kusanyiko lao la wanawake waliokata nywele zao, nao wanajua Biblia inahukumu jambo hilo. Angalia wakishuka kwenda mtaani, wafuasi wao wa kanisa wakishuka kwenda

mtaani, wamevaa kaptura, nao wanajua Neno linapinga jambo hilo. Bali hawana ujasiri wa kulikemea. Lakini, hata hivyo, mtu anayekiri kuwa ni Mkristo, nafsi yake iliyo ndani yake inalia dhidi ya jambo hilo, bali hana ujasiri. Kama hiyo si Sodoma mamboleo, iko wapi basi?

Mungu, tupe mtu atakayelikemea. Hiyo ni kweli. Kama Yohana Mbatizaji alivyosema, “Shoka limekwisha kuwekwa penye shina la mti.” Hilo ndilo tunalohitaji siku hizi.

²³¹ Angalia. Wao ni Sodoma mamboleo. Kumbukeni. Unaona? Nchi nzima imekuwa Sodoma na Gomora mamboleo. Lutu mara nyingine tena akiishi humo. La . . . Akiishi mara nyingine tena, kwa maana imani zake nyofu zinamwambia kwa Neno ya kwamba amekosea.

²³² Angalieni Chicago, Chicago ya juu, wakati hao wahubiri mia tatu walipoketi pale. Na Bwana akaniambia usiku huo yale watakayofanya. Walikuwa wameniwekea mtego. Mimi, niende kule. Nilienda nikamwambia Ndugu Carlson. Nikasema, “Hamtaufanyia kwenye hoteli hiyo. Itawabidi kuupeleka mahali pengine, napo patakuwa ni katika chumba cha kijani kibichi. Nao wameniwekea mtego, sivyo, Ndugu Carlson?” Akainamisha kichwa chake.

Aliketi pale ofisini mwangu, siku chache zilizopita, ili nije, mkutano wa Chicago. Kasema, “Kamwe sitasahau jambo hilo, Ndugu Branham.”

Nami nikasema, “Wameniwekea mtego. Ni kwa nini, Ndugu Carlson? Hivi unaogopa kuniambia ni kwa nini, wewe na Tommy Hicks?” Wakakiinamisha kichwa chao. Nikasema, “Tommy, mbona usiende ukahubiri?”

Akasema, “Nisingeweza kufanya jambo hilo.”

Nikasema, “Nilifikiri ulisema ungenitendea jambo jema.”

²³³ Nikasema, “Jana usiku Bwana aliniambia. Utashuka kwenda kule leo, nawe utaona ya kwamba hamtapata jengo hilo. Mtaenda kwenye jengo lingine. Daktari Mead atakuwa ameketi upande *huu*. Yule mtu mweusi, mke wake, ambaye huimba, watakuwa wameketi papa *hapa*, na kadhalika, mahali wote watakapokuwa wameketi.” Nikasema, “Kutakuwako na kasisi wa Kibudha pale.” Kisha nikasema, “Sasa hakikisheni hilo. Wananichukia maana ninahubiri ubatizo wa maji katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Wananichukia kwa kuwa ninahubiri uzao wa nyoka; na dhidi ya ushahidi, ya kwamba, kila mtu anayenena kwa lugha ana Roho Mtakatifu, na kadhalika.” Nikasema, “Shukeni mje mkamwone Mungu.”

²³⁴ Kufika kule; wakashuka kwenda kule, na saa mbili hasa tangu wakati huo, ama na zaidi, wakati fulani alasiri hiyo, walimpigia simu Ndugu Carlson. Naye akasema, “Jamaa aliyemkodisha hilo, na akalipa malipo ya kwanza juu yake,

alisema, ‘Hatuna budi kubatilisha, kwa maana meneja alisema alikuwa tayari ameliahidia bendi moja usiku huo, ama asubuhi hiyo.’” Basi wasingeweza kulipata.

²³⁵ Kwa hiyo tukaenda kwenye Town and Country. Na asubuhi hiyo tulipoingia mle, na kusimama hapo ndani. Na—na Ndugu Carlson akasema, “Lipo jambo moja. Ninyi ndugu mnaweza msikubaliane na Ndugu Branham, lakini,” akasema, “yeye haogopi kusema yale anayoamini.” Akasema, “Yeye aliniambia mambo haya yangetukia jinsi hasa yalivyo.” Akasema, “Sasa huyu hapa. Acheni ajitetee.”

²³⁶ Nikachukua Maandiko, “Sikuliasi lile ono la kimbinguni,” kama vile Paulo alivyosema. Nikasema, “Mnanichukia, kwa sababu ya ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo. Zaidi ya mia tatu wenu mnajitambulisha kama Daktari *Nanii*, na Daktari *Nanii*.” Nikasema, “Mimi hata sina elimu ya shule ya upili. Bali ninampa changamoto mtu yeyote hapa ulete Biblia yako na kusimama hapa karibu nami, na kukanusha moja ya maneno yaliyosemwa.”

Mnayo kwenye kanda huko nje, kama mkitaka kuyasikiliza. Huo ulikuwa ndio umati mnyamavu sana uliopata kusikia. Nikasema, “Kuna shida gani?” Je! kuna mtu yeyote hapa, usiku wa leo, aliyekuwa kwenye mkutano ule wa asubuhi, hebu tukuone ukiuinua mkono wako. Naam. Vema, hakika, angalieni pande zote.

Nikasema, “Basi, kama hamwezi kuliunga mkono, basi achaneni na mimi.” Naam. Kupayukapayuka kwingi sana, wakati wakiwa pembeni. Lakini kukabiliana moja kwa moja na hoja, ni tofauti. Hiyo ni kweli. Ni. . . Hao watu wakatoka nje.

²³⁷ Tommy Hicks akasema, “Ninataka mia tatu za hizo kanda, kumtumia kila mhubiri mdai wa utatu nimjuaye.”

Hao watu wakinipa mkono, kasema, “Tutashuka tuje huko maskanini tukabatizwe tena.”

Wako wapi? Udhuru. “Siwezi kufanya hivyo. Dhehebu langu halitaniruhusu kufanya hivyo. Nimeoa mke. Nimenunua ng’ombe ya jozi, ama jozi ya ng’ombe, hasa. Ni—nilinunua shamba. Sina budi kwenda kulitazama.” Unaona? Baadhi ya mambo hayo, kama, udhuru. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! maisha hayo yanaistahili Injili? [“La.”]

Kama Injili ni sahihi, hebu na tuuze kila kitu tulicho nacho na tuiishie. Kuwa Mkristo. Naam, bwana. Amina. Angalia sasa, tunapofunga.

²³⁸ Bali udhuru wao ni kanuni zao za imani na madhehebu yao.

Ni kama vile mti. Nilikuwa nikimtaazama Ndugu Banks, hivi majuzi. Nilikuwa na m—msonobari. Niliupanda wakati nilipohamia pale kwa mara ya kwanza, karibu, loo, kama

miaka kumi na mitano iliyopita, ama zaidi. Nami ninaiacha hiyo mizabibu, matawi yakue kwenye msonobari huo, wala tusingeweza kuingiza mashine ya kukata majani mle. Wala hapakuwapo na unyasi wowote, hata hivyo. Ndipo nikaenda hapo, nikachukua msumeno na kuyakata matawi hayo, mpaka mti huo wa msonobari ukafikia *huku* juu kabisa, ambapo ungeweza kutembea chini yake ukiwa na mashine ya kukata nyasi. Na nyasi zilizo nzuri sana ulizopata kuona zipo chini yake sasa. Ilikuwa ni nini? Mbegu ilikuwapo pale. Ilibidi ipate mwanga.

²³⁹ Na mradi tu dhehebu hilo, udhuru wenu, unajaribu kufunika Mbegu hiyo ambayo unajua kweli inakaa mle, unamwakilisha Lutu. Vitupilieni mbali vitu hivyo, na mwache Nuru ya Injili iangaze pale, nguvu za Yesu Kristo. Naam. Ukizuia Nuru kupenya pale, itaifanya isiishi. Kwa kuwa, kama Nuru ikipata kuifikia, itachipuka ipate Uzima.

Hiyo ndiyo sababu watu wanasema, “Usihudhurie baadhi ya mikutano ya namna hiyo.” Wanahofu kiasi fulani cha Nuru itamwangazia mmoja wa wafuasi wao.

²⁴⁰ Mkumbukeni yule mwanamke pale kisimani. Yeye alikuwa ni kahaba.

Hapo walisimama hao makuhani. Walimwona Yesu akimwambia Nathanaeli, “Nilikuona karibu, ulipokuwa chini ya mtini.”

Ndipo hao makuhani wakasema, “Yeye ni Beelizebuli. Yeye ni mpiga ramli. Huyu ni ibilisi.”

²⁴¹ Maskini mwanamke huyu, wakati alipopanda kwenda kule, katika hali yake ya utovu wa uadilifu, akiishi na wanaume sita. Na alipopanda kwenda kule katika hali hiyo, katika hali hiyo aliyokuwamo. Na Yesu akasema, “Nipe maji ninywe.” Maongezi yakaanza. Yeye akasema, “Nenda kamwite mumeo mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

Kasema, “Ulisema kweli. Una watano, na huyo unayeishi naye, siye mume wako.”

Akasema, “Ninaona kwamba Wewe ni nabii, Bwana. Ninajua Masihi atafanya jambo hilo atakapokuja.”

Yesu akasema, “Mimi Ndiye.”

²⁴² Hilo lilitosha. Wakati Nuru hiyo ilipomulika kwenye Mbegu hiyo iliyokuwa ndani ya maskini malaya huyo, siku za umalaya zilikuwa zimekwisha. Huyoo akakimbia kuingia mtaani, akimtukuza Mungu, akasema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini kuwa Huyu Ndiye Masihi?” Ilikuwa ni kitu gani? Hiyo Nuru iliingia kwenye hiyo mbegu huko nyuma chini ya kivuli cha makazi ya malaya. Naam, bwana.

Sasa hebu na tufunge, katika kusema jambo hili. Sijui nina kurasa ngapi zaidi, bali ha—hakika sitazichukua zote. Kama kumi, bali hizo ni karibu tu kufikia nusu tulizopitia. Lakini hebu tufunge, katika kusema jambo hili.

²⁴³ Hebu na tulinganishe jambo fulani, wakati mmoja, la maisha yanayostahili. Hebu na tuyalinganishe maisha ya Mtakatifu Paulo na ya kijana mtawala tajiri. Nuru hiyo hiyo iliwigusa wanaume hao wote wawili. Wote wawili walikuwa na mwaliko ule ule kutoka kwa Yesu Kristo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wote wawili walikuwa wamefunzwa vizuri katika Maandiko. Wote wawili walikuwa ni wanatheolojia. Mnakumbuka, Yesu alimwambia—alimwambia huyo kijana mtawala tajiri, “Zishike amri.”

²⁴⁴ Akasema, “Nimeyashika haya, tangu utotoni mwangu.”

Alikuwa ni mtu aliyefunzwa. Vivyo hivyo na Mtakatifu Paulo. Wote wawili walikuwa wamefunzwa vizuri katika Maandiko. Lakini, wote wawili walikuwa na Neno. Mmoja alikuwa nalo kwa maarifa; huyo mwingine alikuwa na chembechembe ya Uzima ndani yake. Wakati hiyo Nuru ilipomulika, mbele ya Paulo, alisema, “Bwana, U Nani Wewe?”

Kasema, “Mimi ni Yesu.”

“Mimi hapa, basi.” Alikuwa tayari.

²⁴⁵ Nuru hiyo iliwigusa watu hao wawili. Mmoja alikuwa amerutubishwa; huyo mwingine hajarutubishwa. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi: kanisa la kiroho, kanisa la kimwili.

²⁴⁶ Huyu mwanamume tajiri alikuwa na udhuru wake. Asingeweza kulifanya. Alikuwa amelemewa sana na wingi wa marafiki wa ulimwengu. Hakutaka kuacha ushirikiano.

Hiyo ndiyo shida ya watu wengi sana siku hizi. Mnawazia, kwa kuwa ninyi ni wanachama wa nyumba ya kupanga, kamwe usingaliacha udugu huo. “Wote wanakunywa na vitu kama hivyo. Wanafanya *hivi*.” Vema, ambatana nao; hakuna kitu dhidi ya nyumba hiyo ya kupanga, hakuna kitu dhidi ya hilo kanisa. Ninazungumza juu yako. Unaona? Naam. Unaona? Hakuna kitu dhidi ya hilo. Kwa kuwa, ni sita kwa mmoja, na nusu dazani kwa hiyo nyingine. Ndiyo kwanza nimalize kuwaambia kanisa halikuwa kitu ila nyumba ya kupanga, dhehebu, kama wakilikana Neno la Mungu.

²⁴⁷ Angalieni. Yule tajiri alikuwa na udhuru wake. Kamwe hakuuacha ushuhuda wake, hata hivyo. Tunaona ya kwamba aliingia kwenye biashara kubwa. Yeye alikuwa ana maarifa. Naye alifikia mahali ambapo hata ikambidi kufanikiwa sana, hata ikambidi kujenga ghala jipya kuviweka vitu vyake. Ndipo alipokufa; na mseja fulani, huku ameupindua ukosi wake, alihubiri kwenye mazishi yake, hapana shaka. Na alipohubiri, huenda alisema...Walishusha bendera nusu mlingoti, na

kusema, “Ndugu yetu mpendwa, meya wa jiji hili, sasa yuko mikononi mwa Mwenyezi, kwa kuwa alikuwa ni mfuasi mkubwa wa kanisa. Alifanya *kadha*, na *kadha*.”

Na Biblia ilisema, “Akiwa jehanamu aliyainua macho yake, akiwa katika mateso makali.” Mnaona?

²⁴⁸ Basi kumbukeni, angali alitaka kushikilia imani yake katika jehanamu. Alimwona Lazaro, kifuani mwa Ibrahimu, naye akasema, “Baba Ibrahimu, mtume Lazaro huku chini.” Angali anamwita “baba.” Unaona?

Yeye aliyachukua maarifa yake, naye akaenda kwenye kanisa la kielimu. Wakati Nuru hiyo ilipomgusa, yeye aliikataa.

Kama huo si mwelekeo wa kisasa wa kanisa siku hizi, sijui. Haidhuru Mungu anamulikia nini njiani mwao, Nguzo ya Moto ama chochote kile; wao bado, kwa maarifa yao, wanaweza kulielezea vinginevyo, na kwenda kwenye kundi lao la kielimu, kwa hadhi ya kijamii.

²⁴⁹ Lakini Paulo tayari alikuwa kwenye hadhi ya kijamii, akiwa na maarifa mengi, mwanachuoni hodari chini ya Gamalieli, msaidizi mkuu wa kuhani mkuu, zaidi sana hata akawaendea makuhani na akapata kibali cha kuwafunga gereza hao watakatifu wanaojifingirisha. Bali wakati ile Nuru ilipoimulikia njia yake, na akaona ya kwamba Nguzo ya Moto ile ile iliyowaongoza Israeli kupitia nyikani ilikuwa ni Yesu Kristo, aliacha yote aliyopata kujua. Akapata Uzima.

²⁵⁰ Ungeweza kuyaita maisha ya tajiri huyo maisha yanayoistahili Injili aliyoisikia? Ingawa alikuwa ni mwaminio, ungeweza kuyaita maisha ya namna hiyo... Miongoni mwa wenye elimu na tafrija, usiku huo kule juu kwenye... wakati jua likishuka, wakitakiana heri kwa divai, na labda kuhani fulani akisema sala, pale juu. Naye alikuwa na tafrija, na mwombaji ameketi langoni mwake pale. Naye akatoa heri yake kwa divai, na kuzungumza juu ya imani yake kuu aliyokuwa nayo katika Mungu. Na kabla ya mapambazuko, kesho yake asubuhi, kabla jua halijachomoza, alikuwa jehanamu. Hiyo ni kweli. Hao hapo wenye elimu wako.

²⁵¹ Lakini Paulo, wakati ile Nuru ilipomshukia, hebu tuyalinganishe maisha yake tuone kama yanastahili. Ilikuwa? Wakati, Paulo, ile Nuru ilipomgusa, aliacha maarifa yake yote na kuliacha kundi hilo la kielimu, na akatembea katika Roho wa Yesu Kristo. Utukufu kwa Mungu! Huku akiwa mwerevu jinsi alivyokuwa, hata hakutumia maneno makubwa.

Wakati alipokuja miongoni mwa hao Wakorintho, yeye alisema, “Sikuwajia kwa hekima ya mwanadamu. Sikuwajia kwa maneno makuu mno, kwa maana mngeweka imani yenu juu ya hayo. Bali niliwajia katika urahisi, katika nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo, ili kwamba imani yenu iwe mle ndani.” Hayo hapo maisha. Yaangalie.

²⁵² Hakutumia elimu yake. Hakutembea na kundi la wenye elimu. Alitembea katika Roho wa Kristo, mnyenyekevu, mtiifu kwa Neno la Mungu, wakati lilipokuwa ni kinyume sana na kanuni zao za imani. Lakini Paulo aliiona ile Nuru na akatembea ndani Yake (hiyo ni kweli?), akiacha Maisha ya Kristo yamwakisi Yesu Kristo kwa wakati alioishi, kusudi watu wapate kumwona Roho wa Mungu ndani yake.

Na walio wanyenyekevu waliliamini, sana, hata walitaka kuleta lesa. Walizitoa kutoka kwenye mwili wake. Nao waliamini, sana, yeye ni mwakilishi mzuri sana wa Yesu Kristo, hata, chochote alichogusa, wanaamini, kilikuwa kimebarikiwa. Naam. Huyu alikuwa ni mtu wa jinsi gani, aliyetoa maisha yake, utajiri wake, na chochote alichokuwa nacho! Elimu yake; aliisahau yote, apate kutembea na wavuvi, na waombaji na ombamba mtaani, apate kuacha nuru zake ziuakisi upendo wa Yesu Kristo.

Yeye alisema, “Nimepigwa mijeledi mgongoni, mara arobaini na tisa; halinisumbui.” Kasema pia, “Ninachukua mwilini mwangu chapa Zake Yesu Kristo.” Maskini jamaa huyo mdogo akiwa katika hali mbaya sana, alisema, “Ninachukua mwilini mwangu chapa Zake Yesu Kristo.” Ni tofauti ya jinsi gani na huyu mheshimiwa mwenye cheo huku amezungukwa kote kote na makuhani.

²⁵³ Na wakati alipokuwa Rumi, na hakuna mtu anayesimama pamoja naye. Nao walikuwa wakitengeneza ubao, kukikata kichwa chake, huko nje. Hapo ndipo alipolielezea. Loo, jamani! Yeye alisema, “Nimewekewa tayari taji, ambayo Bwana, Hakim Mwenye Haki atanipa Siku ile; wala si mimi tu, bali sasa wote wanaopenda kufunuliwa Kwake.” Hayo hapo maisha yanayoistahili Injili, ama, mwana.

²⁵⁴ Yeye alimtetea Kristo. Aliacha Injili iakisi kupitia kwake. Kabla ya kufanya hivyo, alienda na kujifunza Injili. Akashuka akaenda Arabuni na kukaa huko miaka mitatu, na kulichukua Agano la Kale. Na akaonyesha, kwa Agano la Kale, ya kwamba Yeye alikuwa ni Yesu Kristo. Naye akamwacha aakisi kupitia kwake, kwa kundi la watu wanyenyekevu. Kwamba, yeye, wakati... Yeye alisema, “Ninajua jinsi ya kushiba, na ninajua jinsi ya kuona njaa na kupungukiwa.”

Mtu mwenye elimu kama yeye, na mwanachuoni kama yeye, akisimama karibu na... akiwa na utaalamu kutoka kwa Gamalieli, mmoja wa waalimu mashuhuri sana waliokuwapo wa siku hizo, na akasimama bega kwa bega pamoja na kuhani mkuu. Ndugu, angalipata mamilioni ya dola na kumiliki kila aina ya majengo. Hiyo ni kweli. Bali yeye alisema, “Mimi...”

²⁵⁵ Hata hakuwa ila na koti moja. Naye Dema alimwona mtu mwenye huduma kama hiyo! Timotheo wa pili, mlango wa 3, akasema, “Dema ameniacha, na watu wengine wote,

wakiupenda ulimwengu huu wa sasa.” Kasema, “Ujapo, niletee lile joho nililoacha huko. Baridi inaingia.” Mtu mwenye huduma kama hiyo, na ati angekuwa tu na joho moja? Utukufu kwa Mungu!

²⁵⁶ Inanikumbusha juu ya Mtakatifu Martin, wakati alipokuwa akijaribu kuitetea Injili, na kila kitu, kabla hajaongoka. Katika—katika kipindi Kabla ya Nikea, ama baraza la Nikea, *Wazee wa Nikea*, katika historia. Siku moja, alikuwa akipitia kule mlangoni. Alitoka Tours, Ufaransa. Na kulikuwako na watu... Maskini ombaomba mmoja ameketi pale, akifa, hana nguo. Na watu walipitia pale, ambao wangependa kumpa nguo, wala hawakumpa. Walimpita na kumpuuza maskini jamaa huyo. Ndipo Mtakatifu Martin akasimama pale na kuangalia hilo. Wakasema yeye...

²⁵⁷ Kila askari alikuwa na—alikuwa na mtu wa kuzipiga rangi buti zake. Na yeye alipiga rangi buti za mtumishi wake.

Ndipo akavua koti lake, akakitwaa kisu na kulikata, nusu, vipande viwili, upanga wake. Akamfunika ombaomba huyo katika hilo, kasema, “Sote wawili tunaweza kuishi.”

Akaenda nyumbani na kuingia kitandani. Akilala pale, akiwazia yule mzee alikuwa amelia. Moja kwa moja, kitu Fulani kikamwamsha. Akaangalia. Huyo hapo Yesu Kristo, amesimama humo chumbani, huku amefunikwa kwa maskini kipande kile kile cha joho alichomfunika nacho yule ombaomba. Kasema, “Kadiri mliyowatendea walio wadogo kuliko wote wa watoto hawa, mmenitendea Mimi.” Hayo ni maisha yanayoistahili Injili. Mnajua jinsi alivyoyatia muhuri maisha yake, pia, sivyo?

²⁵⁸ Mwangalieni Polycarp, akiutetea ubatizo kwa Jina la Yesu, dhidi ya kanisa Katoliki la Kirumi. Nao wakamchoma moto kwenye nguzo; wakaibomboa nyumba ya kuogea na wakamchoma moto. Mwangalieni Ireneo, hao wengine, walioteswa kwa ajili ya huduma hii. Hayo ni maisha yanayostahili.

²⁵⁹ Angalieni yale Paulo aliyosema katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 11. Kasema, “Walichanjwa kwa msumeno, wakatenganishwa vipande viwili; wakazungukazunguka, wamevaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, nao walikuwa nyikani, na wahitaji na kadhalika; maisha ambayo ulimwengu huu haustahili kuwa nayo.” Haya basi. Maisha hayo yanaistahili Injili. Yangu na yako yatasimamaje kwenye ile Siku ya Hukumu, kukiwako na watu kama hao?

²⁶⁰ Mwangalieni Paulo sasa. Tutaendelea mbele. Yeye aliitetea Injili, akamwacha Yesu amiminike sana kupitia kwake. Haidhuru ni jinsi gani, ni kitu gani, haidhuru yale mtu yeyote aliyowaza juu yake. Mahali ambapo, kuhani mkuu, mbona, alienda na kukatwa kichwa chake, kwa ajili ya jambo hilo. Yeye alikuwa ni mwakilishi mstahiki wa Injili. Akiacha... Angalieni pale. Haidhuru watu waliwaza nini, aliacha mkondo wa Uzima

wa Milele utiririke kupitia kwake, zaidi sana hata akasema, “Ningeomba niharimishwe na kutengwa na Kristo, kwa ajili ya ndugu zangu.”

Sasa mnajua jinsi mnavyofanya mnapoupata Uzima wa Milele. Hilo hapo swali lenu. Hilo hapo jibu lenu. Mnachukua upande wa kielimu; ama, mnachukua upande *Huu*, kama kweli mna Uzima wa Milele. Hivyo ndivyo inavyokuwa.

²⁶¹ Hivyo ndivyo ilivyotukia. Paulo, akiwa tayari kuharimishwa na Kristo, kuwawezesha watu wake... Vipofu, watu wajinga ambao wasingisikiliza Injili yake!

Ninafikiri, aibu kwangu mwenyewe. Nilikuwa tayari kuwaacha, kwa maana wasingenisikiliza. Ninajisikia kama kutubu. Nami nimetubu. Unaona?

²⁶² Angalia. Haidhuru wengine waliwazia nini, maisha ya aina hii yanaistahili Injili.

Sasa ninafunga.

²⁶³ Yule tajiri, kama vile wengi wetu siku hizi, alilifungia nje na kulikataa Neno la Uzima, kisha akawa mfuasi wa kanisa; ndipo akaonyesha maisha, yanayothibitika katika Biblia, hayakuistahili Injili ambayo aliombwa kupokea. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Injili ingewezaje kuangaza kupitia kwenye nuru iliyotiwa giza jinsi hiyo, kuzikataa nguvu za Mungu?

²⁶⁴ Sasa, jinsi tu ya kuishi maisha mastahiki, ni kumwacha Kristo na Neno Lake (ambapo, Yeye ni Neno) ajiakisi Mwenyewe kikamilifu kabisa ndani yako hata Mungu anathibitisha yale aliyosema kwenye Neno. Kwa kuwa, Kristo alikufa kusudi ajihudhulishe mbele za Mungu, Dhabihu. Na Hiyo ilirudi katika umbo la Roho Mtakatifu, apate kujiakisi Mwenyewe kupitia watu Wake, kuendeleza kazi Yake; akijiakisi kupitia kwako, apate kutimiza Neno Lake lililoahidiwa katika siku hizi za usoni.

Kama vile Yohana Mbatizaji alivyosikia, aliposikia Kristo akija. Na Kristo akajitokeza akaingia majini. Naye Yohana akasema, “Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu.”

Hakuna mtu mwingine aliyeiona. Lakini yeye aliiona, hiyo Nuru ikishuka kutoka Mbinguni, kama hua. Na sauti ikisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu ninayependezwa kuishi ndani Yake.” Yeye aliiona ikija.

Na Yesu akatoka majini, Imanueli, mbele za m—mhubiri aliyedhaniwa kwamba ni wa kimsingi sana. Akajitokeza akaingia majini, mbele za watu, na kusema, “Ninataka kubatizwa na wewe.”

²⁶⁵ Yohana akasema, “Bwana, ninahitaji kubatizwa na Wewe. Kwa nini Wewe unakuja kwangu?” Macho hayo mawili yalikutana, nabii na Mungu wake. Amina. Hivi ungeweza...

Mimi...Hivi si ningependa kusimama na kutazama jambo hilo? Niyaone hayo macho makali, yaliyoingia ndani ya Yohana yakitokeza yayaone hayo macho makali, yaliyoingia ndani ya Yesu; binamu wa pili mmoja kwa mwingine, katika mwili.

²⁶⁶ Yesu akasema, “Yohana, na iwe hivyo, kwa kuwa imetupasa. Sisi ndio Ujumbe wa wakati huu. Inatupasa kutimiza haki zote.”

²⁶⁷ Yohana akawazia, “Naam, Yeye ndiye Dhabihu. Dhabihu haina budi kuoshwa kabla ya kutolewa.” Kisha akasema, “Njoo.” Ndipo akambatiza. Amina. Kwa maneno mengine, “Inatupasa kutimiza haki zote.”

Yesu, akijua ya kwamba mtu huyo alikuwa ni wa kweli, alisema, “Hapajaondokea mtu katika wazao wa mwanamke, kama yeye. Yeye ni zaidi ya nabii; mnaweza kulipokea, huyu ni zaidi ya nabii.” Naye Yesu, akiangalia ndani ya moyo wake, na akijua hilo. Binamu Yake Mwenyewe alikutana naye pale, uso kwa uso.

²⁶⁸ Yohana akasema, “Bwana, ninahitaji kubatizwa na Wewe. Basi kwa nini Wewe unakuja kwangu?”

²⁶⁹ Kasema, “Ruhusu iwe hivyo, Yohana. Lakini, kumbuka, inatupasa kutimiza yote aliyoahidi Mungu. Nami Ndimi ile Dhabihu. Sina budi kuoshwa kabla ya kutolewa.” Loo, jamani! Jamani!

²⁷⁰ Na, leo hii, wakati Nuru za jioni zinapoangaza, wakati hapana mtu mwenye akili zake timamu ila yule asiyeweza kusema; msomi yeyote wa Biblia, akiangalia kwenye Biblia, anajua hii ndiyo siku ya mwisho. Basi, inatupasa tushuke kutoka kwenye kuta hizi kubwa, ama kuyaacha mambo haya, na kuingia kwenye haki ya Yesu Kristo katika siku hii ya mwisho, na kuuchukua Muhuri wa Mungu kabla ibilisi hajatupa alama ya mnyama. Loo, jamani. Naam.

²⁷¹ Mwombe Mungu aijalie Nuru ya siku hii ichomoze ndani yako, upate kuwa mtumishi mwaminifu kwa Mungu. Halafu acha tunda la Roho lidumu milele maishani mwako. Na hayo ni maisha yanayoistahili Injili.

²⁷² Hebu niseme jambo hili, katika kufunga. Njia pekee, njia pekee unayoweza kuishi maisha yanayoistahili Injili, ni kuiacha Injili Yenyewe, kila sehemu ya Injili, iingie ndani yako na kuakisi ahadi Zake, kuzifanya zithibitike. Acha Mungu aishi ndani yako, kuthibitisha ahadi za siku hii.

Kama tu vile Yohana, kama vile Yesu alivyomwambia Yohana, “Ruhusu iwe hivyo, Yohana. Hiyo ni kweli. Lakini sisi ndio wajumbe wa siku hii, nasi hatuna budi kutimiza haki zote.”

Na kama sisi ndio Wakristo wa siku hii, hebu na tumpokee Yesu Kristo moyoni mwetu. Naye ni Neno. Msikatae sehemu yoyote Yake. Useme, “Hilo ni Kweli.” Na uliweke moyoni mwako, angalia tunda la Roho juu yako, na utimize kila ahadi ambayo

aliifanya katika Biblia. Mungu anataka kulitimiza Neno Lake, Naye hana mikono yoyote ila yangu na yako. Hana macho yoyote ila yangu na yako. Hana ulimi ila wako na wangu, “Mimi Ndimi Mzabibu. Ninyi ni matawi.” Matawi huzaa tunda. Mzabibu hulitia nguvu tawi. Hayo ndiyo maisha yanayostahili.

²⁷³ Ombi langu ni kwamba, kwa wale walioko kwenye redio ama kwenye...kwenye maeneo ya kanda, na wale waliopo hapa. Mungu wa neema yote, wa Mbinguni, na atuangazie sisi sote Roho Wake Mtakatifu, kusudi sisi, tangu usiku huu, kuendelea, tunaweza kuishi maisha ambayo Mungu angesema, “Nimependezwa. Inieni katika furaha za Milele ambazo zimewekwa tayari kwa ajili yenu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Mungu wa Mbinguni na atume baraka Zake juu yenu nyote.

²⁷⁴ Ninaomba ya kwamba Mungu atawabariki ninyi wanawake, usiku wa leo, mlio na nywele fupi, hivi kwamba mtaona, na mwondoke kwenye mwelekeo huu wa kisasa wa siku hizi, na mtambue ya kwamba Biblia inasema kwamba hampaswi kufanya jambo hilo. Na kama mna hatia ya kuvaa nguo chafu, kwamba Mungu wa Mbinguni ataimimina neema yake moyoni mwenu, kusudi hamtafanya hivyo tena kabisa, kwamba kamwe hamtakuwa na hatia ya kitu kama hicho tena. Roho Mtakatifu na alifungue tu kwenu na kuwaonyesha. Naomba ninyi, msio na ubatizo wa Roho Mtakatifu...

²⁷⁵ Naomba ninyi wanaume mlio na wake zenu, na mnawaacha kuwa ndio bosi wa nyumba na kuwaongoza kwenye kila jambo, Mungu wa Mbinguni na awape neema kushindilia mguu wenu chini na kumrejesha mwanamke huyo kwenye akili timamu tena, naam, na mtambue ya kwamba hapo ndipo mahali penu katika Kristo. Sio bosi, sasa, bali wewe ndiwe kiongozi wa nyumba. Kumbukeni, yeye hata hayuko katika uumbaji asilia. Yeye ni zaotuka lakota tu, ulilopewa wewe, na Mungu, kukutunza, kuzisafisha nguo zako na kupika chakula chako, na kadhalika. Yeye si mtawala wako wa kimabavu.

²⁷⁶ Ninyi wanawake wa Kimarekani mnazurura huku mkiwa na kitonge cha rangi usoni mwenu, na pua yenu hewani (ingalinyesha, ingaliwazamisha), na kisha mnafikiri ninyi ni namna fulani ya mtawala wa mabavu. Ndivyo ulivyo, kwa dondoadume, bali si kwa mwana halisi wa Mungu. Kweli.

²⁷⁷ Mungu na awape ninyi wanaume neema, kama wana wa Mungu, kuukomesha upuuzi kama huo. Hiyo ni kweli. Na awape neema, kuzitupa hizo sigara chini, mwache kusikiliza hiyo mizaha michafu, upuuzi huo wote. Na tuwe wana wa Mungu, hivi kwamba tuweze kuenenda maisha yanayoistahili Injili.

Ndipo mtu akishuka kwenda barabarani, aseme, “Kama kulipata kuwapo na Mkristo, yule pale mmoja. Yule pale mmoja anaenda ambaye Mungu hujionyesha tu Mwenyewe moja kwa

moja kupitia kwake, na mtu yule ni Mkristo halisi, kama kuliwahi kuwako na Mkristo. Huenda ukafikiri anaonekana ni wa mtindo wa kale. Yeye ni mama halisi.” Hilo hapo.

²⁷⁸ Kuwa Mkristo mwenye sifa nzuri, kwa maana sisi ni wageni hapa. Haya siyo Makazi yetu. Makazi yetu ni huko Juu. Sisi ni wana na binti wa Mfalme, wa *yule* Mfalme. Hebu na tuache maisha yetu yawe ye—yenye sifa nzuri. Na tuishi maisha yatakayokiheshimu kitu hicho tunachodai kuwa, Mkristo. Na endapo huwezi kuishi maisha ya namna hiyo, basi acha kuitwa Mkristo, maana unaleta tu fedheha juu ya Imani hiyo.

²⁷⁹ Asanteni, enyi watu, usiku huu wenye joto, mnaoketi hapa. Ninatumaini ya kwamba hakutakuwako na mmoja wenu atakayepotea, kwenye Siku ile. Mimi—mimi—ninatumaini ya kwamba mimi na ninyi, pamoja, tutapata neema mbele za Mungu, ya kwamba daima nitaweza kutetea kwa kile ambacho ni Kweli, kamwe nisiwaudhi, bali kamwe nisiwachezee. Unaona? Kama ningewachezea, nisingekuwa aina ya baba mzuri, kama nikimwacha mtoto wangu afanye chochote. Nitawasahihisha. Upendo wowote utafanya hivyo. Upendo husahihisha. Ninakumbuka wewe ukiniandikia barua ile, siku ile, Pat. Ningali ninayo. Na upendo husahihisha. Biblia ilisema hivyo. Na kama si sahihi, hiyo ndiyo sababu Mungu hutusahihisha. Yeye anatupenda.

²⁸⁰ Naomba tuishi maisha, tangu sasa na kuendelea, yanayostahili, kwa uzuri na upole. Usisikilize, wakisema, “Vema, Mungu abarikiwe, ninajua anao. Alinena kwa lugha. Alicheza katika Roho.” Hiyo ni sawa. Bali kama hana tunda la Roho, Roho hayumo humo. Yeye anaiga tu namna fulani ya mhemko, ama kitu fulani, maana Roho Mtakatifu anaweza tu kuishi maisha ya tunda la Roho. Hivyo ndivyo tu anavyoweza kufanya.

²⁸¹ Mungu awabariki. Na tuinamishe kichwa chetu, kwa dakika moja.

Jalia ninii. . . Mungu, ambaye ameituma Nuru Yake katika siku hii ya mwisho, iliyo hapa mbele yangu, ya Biblia Yake; na picha ya Malaika hawa, Nuru hii ya kisiri katika umbo la piramidi, ambayo hata wanasayansi hawajui ilivyofika hapa. Hawawezi kuelezea jambo Hilo. Lakini, Baba, tuna shukrani. Ulitwambia, miezi kabla halijatukia, nasi tunakushukuru.

²⁸² Wajalie watu, wanaoitwa kwa Jina Lako, waache dhambi, usiku wa leo, Bwana, kutokuamini. Jalia, wakati. . . imenibidi kuhubiri kwa ukali sana dhidi ya dada zetu, sio kwa sababu siwapendi, Bwana, bali sitaki kumwona ibilisi akiwazungusha mpaka waanguke wafe, moja ya siku hizi, na halafu wajaribu kukulaki katika hali kama hiyo, baada ya kuisikia Kweli ya Mungu, namna hii. Jalia waone kwamba ni jukumu lao, kwenda kuyachunguza Maandiko, na kuona kama hiyo ni

kweli. Washuke magotini mwao basi, kwa uaminifu, na kusema, “Mungu, je! hiyo ni Kweli?” Basi hayo yatakuwa ni yote yanayohitajika, Bwana, kama watakuwa waaminifu kuhusu jambo hilo, kwa kuwa Neno Lako ni Kweli.

²⁸³ Watu hawa wameketi. Wengi wao, labda, walikuwa na mambo yaliyowaudhi. Bali Roho wa Mungu alisema nao, nao waliketi kimya na kusikiliza. Saa imeenda sana. Saa imeenda sana jioni, na pia imeenda katika wakati tunaoishi. Jua linatua. Ulimwengu unapoa. Mungu, giza litaingia karibuni, na halafu kule Kuja kwa Bwana, kulichukua Kanisa Lake. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hili, Bwana!

²⁸⁴ Tunaomba sasa ya kwamba utambariki kila mtu katika Uwepo wa Kiungu. Kila mtu atakayeisikia kanda hii. Bwana, kote ulimwenguni, jalia waondoke kwenye kanuni hizo za imani za kale na kadhalika, na waje na kumtumikia Mungu aliye hai, waje na kuwekeza Kwake, wafanye kama yule malkia wa Kusini alivyofanya. Alikuwa, ilimchukua miezi yake mitatu kufika mahali ambapo mtu mmoja alikuwa akimwakilisha Yesu Kristo, ama Mungu wa Mbinguni, Sulemani. Yesu alisema, “Alikuwa kutoka pande za mwisho za dunia, ili asikie hekima ya Sulemani, na tazama hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.” Nasi tunajua “aliye mkuu kuliko Sulemani” yupo hapa, Roho Mtakatifu Mwenyewe aliye mkuu yupo hapa, akitenda kazi kupitia kwa watu. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hili, Baba. Ninaomba baraka sasa.

²⁸⁵ Mbariki mchungaji wetu mpendwa, Ndugu Neville. Bwana, ninapo—ninapomwangalia na kuwazia juu ya kazi zake za upendo, moyo wangu unarukaruka tu. Ninampenda. Kumwona wakati akimwangalia mke wake na watoto wake wadogo, na—naomba, Mungu, ya kwamba utampa nguvu. Mpe ujasiri. Mbariki kwa muda wa miaka mingi, mingi zaidi ya huduma, shamba hili kuu la mavuno tulilomo.

²⁸⁶ Wabariki ndugu hawa wote wahudumu walioketi hapa usiku wa leo. Wengi wao ni wageni kutoka mahali pengine. Ninaomba ya kwamba utakuwa pamoja nao kule, Junie na Ndugu Ruddell, na hao watu wa thamani ambao ni makanisa shirika kwa kanisa hili hapa, wanaosimama na kuishikilia Nuru ya Injili katika sehemu mbalimbali za miji iliyo karibu, kwa ajili ya Nuru ii hii, kuishindania. Tunashukuru kwa ajili ya watu hao, Bwana. Watie moyo. Na uwape neema ya kustahimili majaribu makubwa na kadhalika yanayokuja juu ya nchi kuwajaribu Wakristo wote.

²⁸⁷ Waponye wagonjwa na wanaoteseka, Bwana. Uwe pamoja nasi kwenye juma hili lijalo sasa. Tupe ujasiri. Jalia masomo haya madogo, yaliyovunjika-vunjika ya shule ya Jumapili ya siku hii kamwe yasiuache moyo wao. Naomba wayatafakari, mchana na usiku. Tujalie baraka hizi, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba. Amina.

288 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaamini Hilo? [“Amina.”] Hebu na tuuimbe wimbo wetu mzuri tena, “Nampenda, Nampenda,” tunapoungana pamoja. Yu wapi Dada Ungren? Je! yupo hapa, mmoja wao, ama dada ambaye ameicheza piano, mmoja wa mama hawa hapa? Siuoni. Naam, huyu hapa, mama huyu hapa. Hiyo ni kweli.

289 Nilitaka, usiku wa leo, kwa heshima yote, bali sikumwona Ndugu Ungren. Nilimtaka aniimbie, usiku wa leo, *Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu!* Nadhani huyo ndugu alienda nyumbani. Unaona? Niliusikia wimbo huo asubuhi ya leo, na kwa kweli niliufurahia. Jamani, loo, jamani! Huo ulipiga tu kengele moyoni mwangu. Na mimi—mimi—mimi nilitaka kumsikia akiimba *Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu!*

290 Sasa hebu na tuimbe *Nampenda*, kila mtu, pamoja. Sasa fungeni tu macho yenu. Na hebu na tumwangelie sasa, tuseme, “Bwana, kama kuna yoyote ya mambo haya ya kimwili ndani yangu, yaondoe, sasa hivi. Yaondoe.” Nanyi, huko nje, mtakaoisikia kanda hii, mtakapousikia wimbo huu, imbeni pamoja nasi, basi, moja kwa moja kwenye kiti chako mahali umeketi.

Kama kuna jambo hilo, kama umehukumiwa na Neno, kama huoni ni Neno, yachunguze Maandiko, uone kama Hilo ni kweli. Inakupasa. Inamaanisha Uzima ama mauti.

Na basi tunapouimba wimbo huu, kama kukiwapo na mambo ya kimwili maishani mwako, naomba uuinue mkono wako, hapo kitini pako. Mwambie mke wako na watoto wako wainue mkono wao, wapendwa wako walio karibu nawe. Imba *Nampenda*, na uyatoe maisha yako Kwake. Useme, “Nisafishe, Bwana, na uovu wote.”

Tunapoimba sasa, na tusimame.

Nampenda, Na- . . .

Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utawaponya watu hawa, hawa watakazivaa lesa hizi. Ninazibariki, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

291 Sasa, katika baraka hii kuu! Endelea tu kuucheza, dada. Funga tu macho yako na kuwazia, kwa dakika moja sasa. Na tuombe, moyoni mwetu. “Bwana Yesu, nichunguze. Hivi kweli ninakupenda? Wewe ulisema, ‘Mkinipenda, mtayatii Maneno Yangu. Mkinipenda, mtalitii Neno Langu.’” Na kisha moyoni mwako, useme, “Bwana, jalia nilitii Neno Lako. Jalia nilifiche moyoni mwangu, nisije kamwe nikakutenda dhambi, hiyo ni kusema, kutokuamini chochote ambacho umesema.”

²⁹² Sasa wakati tukiimba *Nampenda*, hebu na tupeane mikono na mtu fulani aliye karibu na sisi. Nyosha tu mkono, useme, “Mungu akubariki, ndugu, ama dada.” Kwa utulivu sana sasa.

“Na...” Mungu akubariki, ndugu. “Na...” Mungu akubariki, dada yangu. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki. Mungu akubariki, dada. “Na kununu-...” Mungu akubariki, dada yangu. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki.” ...mtini-vari.”

²⁹³ Sasa na tumwinulie mikono yetu.

Na—Nampenda.

Kwani...

Una kitu fulani, kingine, unachotaka kufanya? Nakutaka uwaruhusu wafumukane.

...mimi

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

²⁹⁴ Mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye si ni wa ajabu? [“Amina.”] Ninamwombea kila mmoja wenu, enyi watoto. Ingenifaa nini kusimama hapa na kusema mambo haya kama mimi, moyoni mwangu, sikuona yangewasaidia? Wakati, nimechoka na ni mchovu. Ninasimama hapa kwa shida. Miguu yangu inauma. Na viatu vyangu, nimesimama navyo mpaka nimetoea jasho mle ndani, na kila kitu, mpaka miguu yangu imeganda. Pia nimechoka sana! Mimi si mtoto, tena. Nami nimehubiri mahubiri ya saa tatu ama nne, na kuwaombea wagonjwa, na ninaendelea mchana na usiku. Ninge kuwa ninasimama hapa kwa nini, kufanya hivyo?

Mwajua, miaka hii yote thelathini, kama ilikuwa ni kwa sababu ya kupendwa na watu, nimekataa hilo. Mnajua mimi sichukui fedha. Mnajua hilo. Sijazichukua. Je! nimewaambia jambo lolote katika Jina la Bwana ila lililotimia? Mnajua hiyo ni kweli.

Ninawapenda. Ni upendo wa Mungu ulio moyoni mwangu kwa ajili ya kila mmoja wenu. Laiti ningaliweza kuninii... Laiti ningaliweza kusimama mbele za Mungu, na kusema, “Mungu, jalia—jalia—jalia niwasaidie. Jalia—jalia nifanye *hivi*.” Siwezi kufanya hivyo. Kila mtu hana budi kusimama peke yake. Unaona?

²⁹⁵ Mimi—mimi—ninaamini sisi sote tunapaa juu sasa, moja ya siku hizi. Na ikitokea tulale kabla ya wakati huo, niondolewe kwenu, kumbukeni, nitakutana nanyi Huko juu. Ninajua Kuko. Maono yenyewe ambayo yamewaambia kila kitu, yakiwa ni makamilifu, yametimia jinsi tu Yeye alivyosema. Hakuna mtu, miaka hii yote, ambaye wakati wowote anaweza kusema hapa ya kwamba nilipata kuwaambia jambo lolote ambalo lingetimia ila lile lililotimia. Ulimwenguni kote, unajua hivyo.

Hamjapata kuliona jukwaani, ila kilichomwambia kila mtu Ukweli mtupu. Unaona? Daima imekuwa hivyo. Mungu yuyo huyo aliniruhusu kuangalia ng'ambo ya pazia la wakati. Niliwaona hao wanawake na wanaume wakinitupia mikono yao na kunikumbatia, wakisema, "Loo, Ndugu Branham."

²⁹⁶ Kamwe si—siwezi kuketi. Kwa hiyo, kama nimechoka, ninaenda, haidhuru. Mgongo wangu unauma. Nami, kila siku... Nina—nina—nina umri wa miaka hamsini na minne. Mwajua, unapata maumivu zaidi kila siku.

Maombi yangu ni, "Mungu, nishikilie imara. Nishikilie kwa uthabiti, kulihubiri Neno, nisimame kwenye hiyo Kweli, mpaka nitakapomwona mvulana wangu, Joseph, ana umri wa kutosha, na amejazwa na Roho Mtakatifu; ninaweza kuchukua Biblia hii ya kale iliyochakaa, niiweke mkononi mwake, niseme, 'Mwanangu, ibebe hata mwisho wa maisha yako. Usipatane juu Yake.'"

²⁹⁷ Nilidhani labda Billy angaliihubiri Injili. Mungu kamwe hakumwita.

Lakini ninaamini, Joseph, hata akiwa mvulana mkorofi jinsi alivyo, ninaamini ya kwamba Mungu amemwita. Hiyo ndiyo sababu watoto wadogo hawawezi kusikilizana naye, yeye ni kiongozi. Na mimi—mimi—mimi ninajua Mungu amemwita. Ninataka kumfunza katika njia ya Neno, njia ya Neno la Bwana, hivi kwamba hataliacha Neno hilo. Ninataka kufanya hivyo, mimi mwenyewe, kama Mungu akipenda. Na nitakapokuwa mzee na niketi nyuma, na ninaweza kumwona pale, amesimama mimbarani, kasema, "Injili ii hii, baba yangu aliitetea. Yeye ameketi pale, mzee na hawezi, usiku wa leo. Bali ninataka kupachukua mahali pake na kuichukua nafasi yake, nisimame pale."

²⁹⁸ Ndipo nitaangalia juu, na kusema, "Bwana, jalia mtumishi wako aondoke kwa amani." Hilo ndilo ninalotaka kuona, sana. Mpaka wakati huo utakapowadia...

²⁹⁹ Basi vipi kama ningefufuka katika kizazi kingine? Siwezi. Sina budi kuja pamoja na kizazi hiki. Sina budi kusimama pamoja nanyi. Ninyi ndio ninaopaswa kusimamia, na kutoa hesabu mbele za Mungu, ya Injili ambayo nimehubiri. Mnafikiri ningesimama hapa na kujaribu kuwavuruga-vuruga, kutoka kwenye jambo Fulani nililowaza kwamba ni kweli? Ngingekuwa nikiwatia moyo kwenda kufanya jambo Hilo. Lakini ninajua ya kwamba, ikiwa ni makosa, ninataka kuwaondoa kwenye hilo, kuwaingiza kwenye kilicho cha kweli. Hakika, kutoka moyoni mwangu, Mungu ananishuhudia, ninawapenda, kila mmoja, kwa upendo halisi wa Kikristo, wa Kiungu. Mungu awabariki. Niombeeni.

³⁰⁰ Sijui siku zangu za usoni zikoje, bali ninamjua Yeye anayeshikilia siku zangu za usoni, kwa hiyo ninatulia katika hilo.

³⁰¹ Ninaiacha ninii, mimbara hii kwa mtu ambaye nina imani kubwa mno naye, kama mtumishi wa Yesu Kristo, mchungaji wetu, Ndugu Neville.



JE! MAISHA YAKO YANAISTAHILI INJILI? SWA63-0630E

(Is Your Life Worthy Of The Gospel?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 30 Juni, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org